SUPA JACKPOT
TZS.1,051,207,683
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 19

**RIPOTI MAALUM**
Ushuhuda wanakijiji tope mgodi wa almasi lilivyovamia makazi



Ukurasa 17
Hongera ATCL kwa kuwabwa ...ga Ethiopian, KQ...

Ukurasa 16
Halmashauri yagawa ruzuku pembejeo bure kupagawisha vijana wakimbilie ajira kilimo

Ukurasa 18
TAWA yakabidhiwa visiwa vilivyosheheni utajiri wa utalii ukanda wa Ziwa Nyasa

BUFE
IJUMAA NOVEMBA 18, 2022
Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Kijue kikundi wabeba magunia chenye muundo kampuni, sasa mvuto wa mkoa

Neema Hussein, Mpanda

- Wanajijengea nyumba na kumiliki mashamba
- RC abaki hoi; msaada gerezani, sungusungu...

UKURASA 13

# Nipashe

Ijumaa Novemba 18, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581133

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## SAMIA APEWA TUZO UMAHIRI KATIKA UONGOZI

UKURASA 3

# KIZAAZAA

**NDEGE** ya ATCL yakwama kutua Bukoba, rubani aipeleka Mwanza ... *Endelea ukurasa 2*




Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Hamza Johari

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa

Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangira

# Mtoto afariki dunia, wazazi wake wagundua siku ya pili

UKURASA 2

**MICHEZO** | **PHIRI KWENYE RADA KIATU CHA DHAHABU** UK. 32 | **KATUNI** UK. 6

# Kizaazaa ndege ATCL kukwama kutua Bukoba

**Na Romana Mallya**

NDEGE ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), jana ilishindwa kutua katika Uwanja wa Ndege wa Bukoba mkoani Kagera, kutokana na hali mbaya ya hewa na rubani wake kulazimika kuipeleka Mwanza.

Hali hiyo imejitokeza ikiwa ni siku 11 tangu ndege ya kampuni ya Precision Air kushindwa kutua katika uwanja huo kutokana na hali mbaya ya hewa na kuanguka Ziwa Victoria na kusababisha vifo vya watu 19 na manusura 24.

Taarifa za kushindwa kutua kwa ndege ya ATCL, zilitolewa jana na Mbunge wa Viti Maalum wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Neema Lugangira, kwenye ukurasa wake wa twitter.

Mbunge huyo aliyepiga picha mbele ya ndege ya ATCL akiwa ameshika begi aliandika kuwa: “Still shaken” (bado nina mshtuko) lakini Mungu ni mwema. Nimepanda ndege asubuhi ya leo kwenda Bukoba. Safari ilikuwa na changamoto, tumefika lakini ndege ikashindwa kutua.

Baadaye tena aliandika: “Ninampongeza rubani kwa uamuzi sahihi wa kurudi Mwanza na sasa narudi Dar. Serikali ibebe kwa uzito suala la ‘airport’ (uwanja wa ndege) mpya Bukoba.

“Abiria wengine wamebaki Mwanza, wengine tumerudi Dar es Salaam. Airport (Uwanja wa ndege) ya Bukoba inajulikana kama uwanja wenye changamoto kijiografia na hali ya hewa ikiwa mbaya changamoto ya kutua inazidi. “Ninampongeza Rubani Emmanuel Msangi na Rubani Msaidizi Mhayyar Alnabhany kwa uamuzi sahihi.”

Mbunge huyo katika ukurasa wake huo, alionekana kwenye picha ya pamoja na rubani na msaidizi wake.

Akizungumza na Nipashe jana, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa uamuzi uliofanywa na rubani ni sahihi.

“Taarifa ya Mbunge nimeiona mtandaoni kama wewe. Kama amefanya hivyo (rubani) huo ni uamuzi sahihi kwa rubani na anatakiwa afanye hivyo.

“Kama kuna hali mbaya ya hewa, hata kiwanja kiwe kikubwa, hata kiwe na taa, ‘land instrument system’ (mfumo wa kuwezesha ndege kutua), kukiwa na kimbunga huwezi kutua. Ndiyo maana unasikia ndege inakwenda kwenye viwanja mbadala. ninafiri kilichofanyika ni uamuzi sahihi, amefanya kazi nzuri rubani,” alisisitiza.

Waziri Mbarawa alitolea mfano ndege ambayo ilitakiwa kutua Madagascar, lakini kutokana na hali ya hewa haikuwa nzuri, ikatua Dar es Salaam.

“Hayo ni mambo ya kawaida, lakini tumelichukua hili na tunalifanyika kazi. Siwezi kutoa kauli ya serikali kwa sasa lakini rubani akisema hatui kwamba uwanja una changamoto, mbona jana (juzi) alitua, juzi (Jumanne) alitua.

“Ninafikiri hii ni kutokana na hali ilikuwa si ya kawaida. Kama ingekuwa ya kawaida angetua, ninampongeza rubani kama amefanya hivyo ni jambo zuri.” alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Hamza Johari, alisema: “Ni kweli nimepata taarifa ndege ya Air Tanzania imeshindwa kutua kutokana na hali mbaya ya hewa, kulikuwa na ukungu, mvua, radi na giza uwanja ukawa hauonekani, kwa hiyo rubani akafuta safari na kurudi Mwanza na ametua salama.”

Siku tano baada ya ajali ya ndege ya Precision kudondoka Ziwa Victoria na kuwapo kwa malalamiko ya uwanja kuwa si salama, Johari, alifafanua kuwa uwanja huo ni salama na kumekuwa na safari mbalimbali uwanjani hapo.



Maji machafu yakiwa yametuama kwenye mfereji wa maji ya mvua kando ya Barabara ya Bagamoyo, eneo la Mwenge, mkoani Dar es Salaam jana na kusababisha usumbufu kutokana na harufu mbaya. Baadhi ya wafanyabiashara wa eneo hilo, walidai kuwa maji hayo humwagwa na mama lishe. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Diwani Kawe apotea tena

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limesema linafuatilia tukio la kupotea kwa Diwani wa Kata ya Kawe, Mutta Rwakatare, ambaye mke wake amedai kuwa haonekani nyumbani takribani miezi mitatu sasa.

Mwezi Februari mwaka huu, diwani huyo alitangazwa kupotea na Jeshi la Polisi Kanda Maalum lilimtafuta na kufanikiwa kumpata mwezi Mei nyumbani kwa Ashura Matitu, mkazi wa Tabata Darajani, ambaye alidai kuwa alimpokea diwani huyo akiwa kwenye hali ya ulevi uliopindukia.

Mke wa Diwani Mutta, wakati akizungumza jana jijini Dar es Salaam na EATV alithibitisha kuwa hajui ni wapi alipo mume wake, na kwamba hadi sasa unakaribia mwezi wa tatu bila kuonekana nyumbani, huku akieleza kuwa amechoka na tabia hizo na hatohangaika kumtafuta tena.

“Awali alipopotea alikutwa kwenye moja ya gesti zilizopo wilayani Kinondoni akiwa na mwanamke na walifanikiwa kumrudisha nyumbani, lakini baadaye alitoweka tena,” alisema.

Kaka yake Tibe Rwakatare, alidai kwamba baada ya kutomuona ndugu yao, walikwenda kumtafuta Tabata kwa Ashura, lakini hawakumkuta.

“Ni kweli hatujui alipo na tumejaribu kwenda kwa Ashura ambako alionekana mara ya kwanza, nako hatukumkuta na tunaomba yeyote atakayemuona atupe taarifa nasi tuko tayari kutoa ushirikiano kama familia,” alisema Tibe.

# Mtoto afariki dunia kwa kuangukiwa na ukuta

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MTOTO Esanto Mtewa (7) wa Kijiji cha Utilili, wilayani Ludewa mkoani Njombe, amefariki dunia baada ya kuangukiwa na ukuta wa boma la nyumba wakati akijikinga mvua.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema tukio hilo limetokea Novemba 10, majira ya saa 10 jioni wakati mtoto aliporudi shule na kukuta mlango wa nyumbani kwao umefungwa na kuamua kujinga kwenye boma hilo wakati mvua ikinyesha.

“Kulikuwa na mvua kubwa sana iliyoambatana na upepo, mtoto huyu alirudi kutoka shule na nyumbani kulikuwa hakuna watu akajisitiri kwenye ukuta wa pagale ambalo ni jirani na nyumba yao,” alisema Kamanda Issah.

Alisema pagale hilo lilipigwa na upepo wa mvua na kubomoa ukuta uliomwangukia mtoto. Kamanda alisema, wazazi waliporudi walilala mpaka asubuhi bila ya kuangalia mtoto wao yuko wapi na walipomtafuta baadaye waliona ukuta umeanguka huku mguu wa mtoto ukiwa umetokeza na kubaini ni mtoto wao. Kamanda Issah alisema huo ni uzembe wa wazazi kulala bila kujua mtoto alipo. “Kwa hiyo tunawasihi wazazi wengine ambao mnaweza mkaingia ndani mkalala bila ya kujua watoto wamelalaje hii ni namna fulani ya kauzembe, wazazi msiwe na hiyo hali ya kuwasahau watoto, kwetu sisi huu uzembe tunasema ni ukatili kwa hiyo tunawaomba msiwe na hiyo hali ya ukatili muwalinde watoto,” alisema.

## ACT yataka hatua zichukuliwe kuporomoka bei ya korosho

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali ishughulikie tatizo la kuporomoka kwa bei ya korosho kutokana na uhalisia wa umuhimu wa zao hilo kwenye uchumi wa kusini hususani mikoa ya Lindi na Mtwara .

Pia kimetaka serikali ichukue hatua za haraka kwa kupunguza ushuru, kodi na tozo hadi Sh. 650, ili kupandisha bei na kuwanufaisha wakulima.

Taarifa ya chama hicho iliyotolewa jana na Naibu Katibu Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma, Janeth Rithe, ilisema kiongozi wa Chama hicho, Zitto Kabwe aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi, wanachama na viongozi katika Kata ya Mahuta, Wilaya ya Tandahimba, mkoani Mtwara.

“Minada iliyotangazwa imeleta bei ya juu ya Sh. 2,011 na ya chini Sh. 1,480, imesababisha wakulima kugomea kuuza korosho zao kwa kuwa zinakwenda kuwakandamiza na kuwanyonya zaidi,” alisema.

Zitto alisema licha ya bei ya zao hilo kushuka na wananchi kuonyesha hazitowafaidisha na kuigomea minada hiyo, hakuna hatua zilizochukuliwa na serikali kuwanusuru wakulima.

“Badala yake serikali imeiachia Bodi ya Korosho kutumia nguvu kuwalazimisha wakulima wauze hivyo hivyo, hii haikubaliki. Serikali haijajielekeza kushughulikia changamoto ya bei na kuwasaidia wakulima hawa,” alisema.

Pia, alisema ni wakati wa kuhakikisha wakulima wanaunganishwa na hifadhi ya jamii ili kuwalinda na anguko la bei za mazao, uzalishaji kutokana na ukame, mikopo ya kuongeza uzalishaji na pensheni kwa wakulima wazee.

Alisema nchi imekuwa ikisafirisha korosho ghafi kwa muda mrefu na kutaka viwanda vya korosho vilivyokufa vifufuliwe na kuvutia uwekezaji wa vingine vipya, ili wasiwe watumwa wa bei kila uchwao. Kiongozi huyo alitaka wakulima wawezeshwe kupitia vyama vyao kutumia teknolojia rahisi, ili kubangua korosho zao.

Alisema kilio cha wakulima katika maeneo mengi ni mfumo kupoteza malengo na unatumika kuwakandamiza badala ya kuwasadaia kama ilivyotarajiwa.

Alisema wananchi wanalalamika na kuukataa mfumo huo kwa sababu za kucheleweshewa malipo, kupitia mfumo huo.

Alimwomba Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kushughulikia matatizo hayo kwa haraka na mfumo wa malipo ya korosho ufanyike kidijitali kwa mtu kupata papo hapo.

Novemba 7, mwaka huu, Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota bungeni jijini Dodoma, alisema miongoni mwa mikakati waliyonayo ni kuwawezesha wabanguaji wadogo ili kuongeza ubanguaji wa korosho ghafi na kutengeneza masoko ya uhakika ya korosho ambayo imechakatwa.



Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe (mwenye miwani katikati), akilakiwa na wanachama na wafuasi wa chama hicho, alipowasili katika kata ya Mchoteka, jimbo la Tunduru Kusini, mkoani Ruvuma juzi, akiwa kwenye ziara ya ujenzi wa chama na kuwasikiliza wananchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia apewa tuzo umahiri katika uongozi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

JUMUIYA ya Maridhiano Mkoa wa Mbeya inayoongozwa na viongozi wa dini, imekabidhi tuzo ya heshima kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutambua jitihada kubwa anazofanya katika kuwaongoza Watanzania.

Jitihada hizo ni kulinda amani na utulivu wa taifa, upatikanaji wa fursa za kibishara, mapambano dhidi ya UVIKO-19 na ujenzi wa miradi ya maji na afya inayowafikia wananchi wengi hasa wa vijijini.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alipokea jana tuzo hiyo kwa niaba ya Rais Samia na kuishukuru jumuiya hiyo kwa kutambua mchango wa kiongozi huyo katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Alisema tuzo hiyo inatoa fursa kwa serikali kuongeza kasi ya kukamilisha miradi ya maendeleo inayoendelea kujengwa katika maeneo mbalimbali nchini. “Rais Samia anawashukuru sana kwa kumpatia tuzo hii ya heshima ambayo inatoa tafsiri kwamba juhudi zinaonekana kama vile ujenzi wa miradi ya maendeleo kufungua fursa za kibiashara ndani na nje ya nchi, pamoja na kulinda amani na utulivu.

“Viongozi wa serikali tutaendelea kuisemea serikali kwenye mambo yote yaliyofanywa yanayolenga kuimarisha uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla,”alisema.

Pia alisema mkoa huo umenufaika na jitihada hizo kwenye sekta ya miundombinu na kwamba zilitolewa Sh. bilioni saba za ujenzi wa barabara ya mchepuko ya Inyala ambayo ni muhimu katika kukabili ajali.

Eneo la Inyala, alisema limegharimu maisha ya zaidi ya watu 30 katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba, mwaka huu, na kwamba fedha hizo zitasaidia kujenga barabara yenye viwango na kupunguza ajali.

Awali, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Mkoa wa Mbeya, Askofu wa Kanisa la Calvary Assemblies of God, Oscar Ongere, alisema tuzo hiyo ni sehemu ya kuunga mkono jitihada zilizofanywa na Rais.

Alisema Rais Samia amekuwa kiungo kati ya taasisi za kidini na serikali, na kwamba masuala kadhaa amekuwa akiwashirikisha kwa mustakabali wa taifa kama vile vita dhidi ya uharibifu wa watoto na Jumuiya hiyo imetumia nyumba za ibada kukemea vitendo mbalimbali vya ukatili.

Mjumbe wa Jumuiya hiyo, Askofu Erica Mwakyokile, alisema wanajivunia ujenzi wa Hospitali ya Wazazi Meta iliyoko jijini Mbeya ambayo imejengwa kukidhi mahitaji yote muhimu kwa ajili ya kumsaidia mjamzito kujifungua salama.

Mwakyolile alisema ujenzi wa Hospitali mpya ya Wazazi Meta umeleta matumaini kwa kinamama kuhusu usalama wao wanapojifungua kwa kuwa kuna miundombinu muhimu na mazingira rafiki .


## NGOMENI ENTERPRISES

### NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **crdb bank** makao makuu Dar es salaam tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) tu ili uweze kulipa deni lako lote unalodaiwa Pamoja na gharama za dalali. Kukaidi au kushindwa kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoweka bank kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA / MAHALI | TAREHE/ MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | BIUSI ANJELA MKUMBWA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KIBAGA KINYEREZI WILAYA YAILALA. DAR ES SALAAM. | 15.12.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI KUENDELEA |
| 2. | TITUS LAZARO MGIMBA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO PUGU BOMBANI WILAYA YA ILALA,DAR ES SALAAM. | 17.12.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| 3. | PAUL MREMI LYIMO | NYUMBA YA MAKAZI YENYE TITLENO. 142157, PLOT 304 ILIYOPO REGENT ESTATE KINONDONI, DAR ES SALAAM. | 8.12.2022 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 4 | ALTO LEONARD NGUNYALI | NYUMBA YA MAKAZI YENYE TITLENO.117163, PLOT 46 BLOCK 15 ILIYOPO MBWENI MPIJI, WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM. | 22.12.2022 KUANZIASAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA. |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Dhamana itauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya asilimia 25 ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na asilimia 75 atalipa ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la asilimia 75 katika muda uliopangwa hapo juu, hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa nyuma na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**MAWASILIANO:**
**CRDB BANK PLC, HEAD QUARTER. NGOMENI ENTERPRISES, DSM. SIMU: 0719974916/ 0784252048**

NIC Life House 4th Floor, Wing C
Sokoine Drive/Ohio Street
P. O. Box 6100
Dar es Salaam
Tel:+255 22 2112045
Fax: +255 22 2112045

Dev Recoveries Ltd

### NOTISI YA KULIPA DENI NA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **DEV RECOVERIES LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK TANZANIA LIMITED**, tunatoa notisi ya siku kumi na nne ya kulipa deni kwa hiari muda huo ukifika bila kulipa dhamana itauzwa kwa njia ya **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika siku na tarehe kama inavyoonekana hapo chini, mnada utafanyika kuanzia saa 6:00 mchana na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonyesha hapo chini.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA.**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | MANDHARI VILLA MATEMWE LIMITED | SITE PLAN 1135/2011. HOTEL YA MANDHARI VILLA, MATEMWE, UNGUJA KASKAZINI, ZANZIBAR (0.14) BEACONS 150,151, 153 AND 154. | 08/12/2022 kuanzia saa 06:00 Mchana |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa “kama ilivyo”.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine ni za mnunuzi.
4. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 02:00 asubuhi na kuendelea.
5. Kwa mawasiliano zaidi piga **simu No: 0788438640 / 0712390460**

# Washukiwa watatu wa ujambazi wauawa

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

WATU watatu wanaodhaniwa kuwa majambazi wameuawa kwa kupigwa risasi na polisi katika majibizano ya risasi katika kijiji cha Muganza, Ngara mkoani Kagera.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, William Mwampaghale, alisema jana kuwa kuuawa kwa watu hao kulitokana na operesheni maalumu inayofanywa na jeshi hilo katika maeneo mbalimbali ya mkoa hasa mipakani. Operesheni hiyo inayolenga kudhibiti uhalifu wa kutumia silaha, ilianza Septemba, mwaka huu.

Mwampaghale alisema wakati wakiendelea na operesheni hiyo Novemba 15, mwaka huu, walipata taarifa fiche kutoka kwa raia wema kuwa kuna kundi la watu wanajiandaa kufanya uhalifu kwa kutumia silaha.

Alisema ilipotimu saa 4:30 usiku, waliweka mtego katika barabara itokayo Bugarama kwenda Muganza na kufanikiwa kuwaona watu hao.

"Waliamrishwa na polisi kusimama lakini walikataa na kuanza kupiga risasi. Kwa kuwa kulikuwa na giza na ni usiku, polisi walijibu na kuwajeruhi watu watatu wenye jinsia ya kiume wanaokadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 25 na 35 ambao hawajatambuliwa kwa majina. Watu hao walifariki dunia wakati wakipelekwa hospitalini," alisema.

Kamanda Mwampaghale alisema watu wengine wawili walifanikiwa kukimbia na kwamba katika eneo la tukio ilipatikana bunduki moja aina ya AK 47 isiyokuwa na namba za usajili, ikiwa na magazine moja yenye risasi 12.

Alisema miili ya watu hao watatu imehifadhiwa katika Hospitali ya Nyamiaga Wilaya ya Ngara ikisubiri utambuzi na kwamba uchunguzi wa awali umebaini kuwa kikundi cha watu hao kimekuwa kikihusika katika unyang'anyi wa kutumia silaha katika maeneo ya Bugarama, Muganza na Murusagamba.

"Wamekuwa wakiwavamia wananchi katika biashara zao na maeneo ya barabarani wakati wakitoka kwenye shughuli zao na kuwapora fedha na mali. Tunatoa onyo kwa watu wote wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu wa aina yoyote kuacha mara moja kwani misako inaendelea na watakamatwa na kufikishwa mahakamani," alisema.

Kamanda alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo, ili wahalifu waweze kudhibitiwa kabla ya kusababisha madhara zaidi.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, William Mwampaghale, akionyesha kwa waandishi wa habari mkoani humo jana, bunduki aina ya AK 47 na magazine yenye risasi 12 baada ya tukio la majibizano ya risasi baina ya kundi la watu watano wanaodhaniwa kuwa ni majambazi na askari, katika kijiji cha Muganza kata Mursagamba wilaya ya Ngara, ambapo watatu kati yao walifariki dunia. **PICHA: LILIAN LUGAKINGIRA**

## 'Bila kubadili utaratibu kula, magonjwa yatazidi'

**Na Maulid Mmbaga**

MKURUGENZI Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza katika Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee (MOHCDGEC), Dk. James Kiologwe, ameeleza bila Watanzania kubadili utaratibu wa kula chakula magonjwa yataendelea kuwaandama.

Aidha, amesema ni muhimu kula kwa wingi vyakula vyenye virutubisho kama matunda na mboga ili kuimarisha afya zao.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali ya afya, alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la watu wanaosumbuliwa na magonjwa yasiyoambukiza na kwamba hali hiyo inasababishwa na tatizo la uelewa mdogo juu ya kuzingatia lishe bora.

Alibainisha kuwa watu wengi hawana utaratibu wa kupima afya zao mara kwa mara jambo linalosababisha wengi wao kwenda hospitali wakati ugonjwa ukiwa umefikikia hatua mbaya na tatizo kubwa lililoko ni asilimia 75 ya watu ambao hawajitambui kwamba wana magonjwa.

"Kuna tatizo kubwa la watu kujua namna ya kujikinga na la utambuzi wa mapema, magonjwa haya yana mzizi wake na tunajua ni namna gani utandawazi unasababisha magonjwa yasiyoambukiza na hata tafsiri ya chakula inabadilika na utandawazi," alisema na kuongeza:

"Tafsiri ya chakula bora imehama kutoka mboga sasa tumeenda kwenye chipsi na ya maendeleo imehama kwamba mtu aliyeendelea ni yule anayepanda bodaboda na sio yule anayetembea kwa miguu, hiyo inahitaji kazi kubwa ifanyike kueleza namna utandawazi unavyosababisha changamoto katika jamii yetu."

Aliongeza kuwa wanaelewa pia changamoto ya ikolojia inavyobadilika na namna ambavyo inaweza kuleta magonjwa yasiyoambukiza, huku akisisitiza wanahabari kutumia kalamu zao kuzungumzia umuhimu wa mazingira, ikolojia na jinsi ya kujikinga na magonjwa hayo.

Aidha, alibainisha kuwa wanawake na wanaume wanaathirika tofauti na magonjwa yasiyoambukiza, na pia wanamchango tofauti, akieleza kuwa kitaalamu kuna uwezekano kwa kila mtu alivyo ikawa ni matokeo ya namna alivyo bibi aliyemzaa bibi yake, na kwamba mwanamke anaumuhimu mkubwa katika kukinga magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Aliendelea kufafanua kwamba mama anayejifungua mtoto mwenye uzito pungufu, anauwezekano mkubwa wa kusababisha mtoto husika kupata magonjwa yasiyo ya kuambukiza mara nne zaidi na kuwezekano pia wa kupeleka tatizo hilo kwa kizazi cha tatu hadi cha nne.

"Tukizuia tatizo hili kwa mama ni tofauti na kwa baba, tunapaswa kuelewa ni namna gani tutaimarisha ushirikiano wa kijinsia katika suala la magonjwa yasiyoambukiza mzigo huu ni mkubwa, lakini vita hii ni lazima tuchague ni wapi ambapo kutakuwa na matunda makubwa zaidi yakiwamo kujenga uelewa na kuimarisha ushirikiano katika sekta mbalimbali.

## Mawakala CRDB sasa kufungua akaunti na kutoa kadi za benki

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imekamilisha utaratibu unaowawezesha mawakala wake zaidi ya 25,000 kumfungulia mteja akaunti na kumpa kadi ndani ya muda mfupi ili atumie huduma za benki.

CRDB imefanya hivyo kwa kutambua mchango wa mawakala katika kusogeza huduma za benki karibu zaidi na wananchi hususani waliopo maeneo ambayo hayana matawi ya benki.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa Wakala App uliofanywa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela alisema CRDB ilikuwa benki ya kwanza nchini kuanzisha huduma kupitia mawakala mwaka 2013.

Alisema katika kufanya hivyo iliwasajili mawakala 500 na sasa inajivunia kuwa nao zaidi ya 25,000 ambao wamesambaa kote nchini, hivyo kuifanya iongoze nchini na kuwa ya tatu Afrika Mashariki.

"Mfumo wa CRDB Wakala umekua na mchango mkubwa katika ufikishaji wa huduma za fedha kwa wananchi, taarifa zetu za utendaji zinaonyesha zaidi ya miamala milioni 100 yenye thamani ya Sh. trilioni 50 imekuwa ikifanyika kupitia CRDB Wakala kwa mwaka, mfumo huu pia umekuwa ukisaidia katika ukusanyaji wa mapato ya serikali ambapo takribani Sh. trilioni 1.3 hukusanywa kwa mwaka," alisema Nsekela.

Alifafanua kuwa mfumo huo wa CRDB Wakala unatoa huduma za fedha kwa watanzania milioni tatu kwa mwezi ambapo asilimia 40 ni wateja wa benki na asilimia 60 ni wananchi wengine.

Alibainisha kuwa mfumo wa CRDB Wakala umetoa zaidi ya ajira 35,000 kwa vijana wanaopokea kamisheni kwa miamala wanayoifanya.

"CRDB Wakala App ni mfumo mpya wa kisasa, salama na wa kidijitali unaotumika kwenye simu janja kutoa huduma za kibenki kwa ufanisi wa hali ya juu, hivyo kuongeza ufanisi, kasi ya utoaji huduma na kupunguza gharama za uendeshaji kwa watoa huduma hasa kwa mawakala wa benki.

"Huu ni mwendelezo wa juhudi za Benki ya CRDB katika kutambua umuhimu wa huduma za kidigitali katika kuleta ufanisi wa huduma jumuishi za fedha na maendeleo kwa ujumla.

"Kupitia huduma hii tunaamini tutawafikia watanzania wanaoishi vijijini na sehemu za pembezoni ili kuhakikisha makundi hayo hayaachwi nyuma," alisema Nsekela.

Akizindua mfumo huo, Waziri Nape alisema sekta ya fedha ina mchango mkubwa katika ukuaji na maendeleo ya uchumi, kujenga uchumi jumuishi na kupunguza umaskini ndio maana serikali nyingi duniani kote zinatilia mkazo suala la ujumuishi wa kifedha.

HABARI KITAIFA



Meneja Mwandamizi wa Afya, Usalama, Mazingira na Mafunzo wa kampuni ya Geita Gold Mining Ltd (GGML), Dk. Kiva Mvungi (kushoto), akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Peter Kisenge, kuhusu ufadhili wa GGML ulivyoisaidia Hospitali ya Kanda ya Chato kutoa huduma kwa watu wenye matatizo ya moyo, katika kliniki inayotembea ambayo ilitoa huduma kwa siku tano kwa watu 500 waliouchunguzwa magonjwa ya moyo, mishipa na magonjwa yasiyoambukiza, alipotembelea jana.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni bima zapongezwa kufanya kazi miradi ya gesi

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imepongeza umoja wa kampuni 22 za bima nchini kufanyakazi kwenye miradi mikubwa ya mafuta na gesi ili kuiwezesha nchi kupata pato la taifa kupitia ada ya kinga dhidi ya vihatarishi mbalimbali.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Chande, katika uzinduzi wa muungano huo ujulikanao kama Tanzania Energy co-insurance Consortium ya mafuta na gesi.

Alisema umoja huo ni wa kwanza Tanzania na serikali itaongeza pato la taifa kupitia ada za bima ambazo sasa zitabaki nchini tofauti na zamani.

Chande alisema awali uwezo wa mtaji wa kampuni mojamoja za bima nchini haukuweza kukidhi vigezo vya ada ya kinga dhidi ya vihatarishi na kufanya miradi mingi ya uwezekaji katika sekta hiyo kuingia mikataba na kampuni za nje ya nchi.

Alisema umoja huo utasaidia kuongeza pato la taifa kwa kuwa fedha za ada ya bima huchukuliwa na kampuni za nje ambazo zina uwezo mkubwa kifedha.

"Kupitia umoja huu, sasa kampuni za uwezekaji wa nje zitakata bima zao hapa nchini ili kujikinga na vihatarishi katika sekta ya mafuta na gesi," alisema Chande.

Alisema muungano huo unaongeza uwezo wa kuhimili vihatarishi hivyo na kusaidia ubakishaji (retention) fedha za ada nchini kwa maendeleo ya taifa.

"Uhitaji wa muungano huu ulianza mwaka 2019 kuelekea mwaka 2020 baada ya miradi mikubwa kama (East Africa Crude Oil Pipeline), wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 3.5 na mradi wa LNG (Gas Processing Plant) wenye thamani wa Dola bilioni 30, miradi mikubwa ya madini na kilimo," alisema na kuongeza:

"Kutokana na thamani ya miradi hiyo kuwa kubwa, bima ya kinga dhidi ya vihatarishi ilisababisha uhitaji wa bima mtawanyo ambayo kwa asilimia kubwa ilinunuliwa kwa kampuni ya bima mtawanyo za nje na kufanya fedha nyingi kama malipo ya ada ya kukinga miradi hiyo dhidi ya vihatarishi kuzinufaisha nchi hizo," alisema Chande.

Alisema kutokana na mtaji mdogo wa kampuni za bima nchini kulihitajika kuundwa kwa umoja huo, ili kuunganisha uwezo wa kampuni za ndani dhidi ya vihatarishi maalum ili kuhimili vihatarishi na kubakisha ada nchini.

Naye, Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (Tira), Dk. Baghayo Saqware alisema umoja huo unazifanya kampuni hizo 22 kuunganisha mitaji na kuwa na uwezo wa kuhimili vihatarishi vya miradi hiyo mikubwa na mradi gesi asilia wa Lindi wenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 30 ambao unatarajiwa kutekelezwa hivi karibuni.

Saqware alisema kuwa muunganiko huo utaleta faida mbalimbali kama kuwa na uwezo mkubwa wa kifedha na kitaaluma kwa kampuni za bima, kuongeza uhifadhi wa ndani na uendeshaji mzuri wa hatari miongoni mwa kampuni za bima na bima mtawanyo, kulinda maslahi ya watanzania na kuongeza uwezo wa ndani kulingana na mahitaji ya kisheria na kuongeza ajira.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Bima ya Phoenix Assurance, Ashraf Musbally, alisema wiki chache zijazo watatoa mwongozo kwa wadau mbalimbali kuhusu malengo yao ya muda mfupi na mrefu.

Musbally alisema wanajisikia fahari kubwa kuona wazo lao limeungwa mkono na wadau wa sekta hiyo na wanaamini litaleta tija katika maendeleo ya sekta ya bima hasa kwa upande wa gesi na mafuta.

# Makalla ataka mali DDC zilizoporwa zirejeshwe

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla amelitaka Shirika la Uchumi na Maendeleo la Jiji la Dar es Salaam (DDC), kubainisha mali zake zote zilizovaniwa au kuporwa, ili nguvu iwekwe kuhakikisha zinarejeshwa kwa mujibu wa sheria.

Makalla alitoa maelekezo hayo jana wakati wa uzinduzi wa mradi wa shirika hilo, DDC Millennium Lounge, uliopo Keko, Wilaya ya Temeke.

Akizungumza katika uzinduzi huo, kiongozi huyo alitaka bodi na menejimenti ya shirika, kubadilika kifikra na kimtazamo ili kuhakikisha DDC inajiendesha kibiashara.

Pia amelitaka kuandaa mpango mkakati wa kibiashara kwa kutumia vizuri rasilimali wanazomiliki kukuza uchumi.

"Rais Samia Suluhu Hassan, anataka kuona DDC yenye mafanikio makubwa kibiashara na kiuchumi, kulingana na lengo la Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere," alisema.

Katika hatua nyingine, Makalla aligawa vihifadhia taka (dustbin) 1,000 kwa daladala 1,000 zinazofanya shughuli zake mkoani humo kwa lengo la kuzuia utupaji taka ovyo unaofanywa na abiria wakati wakiwa kwenye magari hayo.

Katika kusisitiza hilo amepiga marufuku tabia ya abiria kutupa taka ovyo huku akiwataka madereva na utingo kuwakemea wale wote watakaojaribu kuzitupa barabarani wakati wakiwa safarini.

Makalla ameipongeza Kampuni ya Wese Tikisa Tanki Piga Bao, kwa kutoa vifaa hivyo ili kuunga mkono kampeni ya 'Pendezesha Jiji'.

# Kanuni biashara hewa ukaa zaiva

**Na Jenifer Gilla,** MISRI

OFISI ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, imepitisha kanuni na taratibu zitakazosimamia biashara ya hewa ukaa nchini kwa lengo la kuwanufaisha Watanzania na kutunza mazingira husan maeneo ya vijijini.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Hamisi Hamza Hamisi, kwenye Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mabadiliko ya Tabia nchi unaoendelea Sharm El Sheikh, nchini Misri.

"Hivi karibuni Waziri (Selemani Jafo) alisaini kanuni au taratibu ambazo zitasimamia biashara ya hewa ukaa ambayo sasa imekuwa ni biashara kubwa na kama tukiweza kuisimamia vizuri itatunufaisha," alisema. Alisema jambo linalofuata baada yakupitishwa kwa kanuni hizo ni kutoa elimu kwa wawekezaji wazawa na wasio wazawa kuhusu faida na fursa zinazopatikana katika biashara hiyo na namna Watanzania watakavyonufaika.

Vilevile, alisema mpaka sasa wameshakutana na wadau mbalimbali na wamekubali kuanza biashara hiyo ambayo itachangia kwa kiasi kikubwa kutunza mazingira. "Lakini pili tutanufaika, tutajenga shule, tutajenga zahanati tutajenga barabara, tutawasogezea wananchi maji, kupitia faida zitokanazo na hii biashara," alisema.

Dk. Elikana John, kutoka Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), alisema biashara hiyo pia itachangia kuhifadhi misitu ambayo inafaida nyingi ikiwamo, kuleta mvua na makazi ya bioanuai ambayo wanatishia kutoweka kwa kukosa mahali pa kuishi.

"Kupitia biashara hii, uhifadhi wa misitu utakuwa endelevu kwa kuwa utakuwa unamalipo ndani yake, kwa hiyo tunategemea itatupunguzia uharibifu unaoendela hasa kwa jamii wanaoishi kwenye maeneo yanayozunguka maliasili hiyo," alisema.

Alisema kwa kuona umuhimu wa kuwapo na biashara hiyo nchini, TFS imeamua kushiriki katika mkutano huo ili kutafuta wadau waje watakaokwenda kuwekeza ambapo mwitikio unaonekana kuwa mazuri.

"Kwa hiyo hii tunaiona kama ni nafasi nyingine pekee ambayo itatusaidia kupambana na uharibifu na upatikanaji wa rasilimali zetu kwa kuwa wananchi hawa wamekuwa wakitegemea uwepo wa hii misitu, na TFS tunataka kiasi kikubwa cha mapato yatakayopatikana yaende kusaidia wananchi, " alisema. Ofisa Mradi kutoka Shirika la International Union for Conservation of Nature (IUCN), Dk. Elinasi Monga, alisema biashara hiyo itakuwa na mafanikio makubwa nchini kwa sababu inashirikisha wazawa moja kwa moja.

Alisema wawekezaji wengi wamekuwa wakiwadharau azawa na matokeo yake miradi yao inakufa kwa sababu kuna mambo mambo mengi wazawa wanayajua kuhusu maeneo hayo ambayo yanachangia kukua au kufa kwa miradi hiyo.

"Ustawi wa miradi hasa ya vijijini mara nyingi upo mikononi mwa wazawa kwa sababu kuna mambo mengi wanayajua ikiwamo jiografia, hali ya hewa, wanyama na mimea, kwa hiyo unapowashirikisha unaongeza maarifa na ulinzi katika mradi huo," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua hii ya TRA ni ya kupongezwa

**HIVI** karibuni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ilitangaza kuachana na tabia ya ukusanyaji wa mapato kwa njia ya mabavu na kuahidi utaratibu wa sasa kodi itakusanywa kwa mazungumzo na walipa kodi.

TRA kupitia Mwenyekiti wake wa bodi, Mussa Uledi ilisema imeona tabia ya kukusanya kodi kwa kutumia mabavu na vikosi kazi imepitwa na wakati na haina tija kwa wakati huu.

Uledi alisema kwa sasa wafanyabiashara wenye madeni ya kodi wamekuwa wakifanya mazungumzo na mamlaka na kutatua changamoto baina ya pande hizo mbili kwa amani.

Uledi alisema pamoja na kuacha kutumia mabavu kukusanya kodi bado mapato ya mamlaka hiyo yamekuwa yakiongezeka mwezi hadi mwezi hali inayothibitisha utaratibu wa zamani wa kutumia nguvu haukuwa na maana.

Sisi tunaona hiyo ni hatua kubwa na ya kupongezwa kwani utaratibu mpya wa mazungumzo ni wa kujenga zaidi kuliko kubomoa kwasababu utasaidia Watanzania wengi kupata mwamko wa kulipa kodi kwa hiari yao.

Katika awamu ya tano tulishuhudia maduka mengi ya wafanyabiashara yakifungwa na mamlaka hiyo kwa madai kuwa wamiliki hawajalipa kodi hali ambayo ilisababisha wafanyabiashara kuiona TRA kama polisi.

Kikosi kazi kilichokuwa kikitumika kukusanya kodi kwa mabavu kilisababisha kwa kiasi fulani wafanyabiashara kuichukia Mamlaka na kushusha ari ya ulipaji wa kodi kwa hiari hivyo kuondoa vikosi kazi ni hatua nzuri.

Tunawapongeza TRA kwa uamuzi huo kwani kufunga maduka ya walipa kodi kwa madai hawajalipa ni utaratibu usio na tija kwa nchi, iwapo mfanyabiashara huyo ataachwa afanye biashara yake anaweza kulipa deni taratibu na hatimaye kulimaliza.

Hatua ya kumfungia duka au ofisi mfanyabiashara ambaye anadaiwa kushindwa kulipa kodi sio mwafaka kwa kuwa jambo hilo linaweza kutatuliwa kwa njia ya mazungumzo huku biashara zikiendelea.

Sisi tunaona ili kujenga misingi imara ya watu kulipa kodi kwa hiari, TRA inapaswa kuwa rafiki wa wafanyabiashara kuwa nao karibu, kujua maendeleo ya biashara zao badala ya kufanyakazi kama polisi hali inayosababisha uadui baina ya pande hizo mbili.

Wako wafanyabiashara wanaoshindwa kulipa kodi kutokana na kuanguka kwa biashara walizokuwa wakizifanya kutokana na baadhi ya biashara hizo kuwa za msimu.

Ni kweli wako wafanyabiashara wanaoweza kutumia mwanya huo kutaka kukwepa kodi hivyo mamlaka wafanye uchunguzi kubaini ukweli wa madai ya mfanyabiashara huyo kuhusu kushuka kwa mapato yake.

Hali hiyo itadumisha uhusiano mwema baina ya wafanyabiashara na mamlaka hiyo na kuongeza hamasa ya wananchi kulipa kodi kwa hiari.

TRA inawajibu wa kuwaelimisha watumishi wake kufanyakazi kwa diplomasia zaidi kwa kusikiliza shida za wafanyabiashara na kuzitatua au kuzifikisha kwa wakubwa zao zile walizoshindwa kuzitatua badala ya kuwanyanyasa wafanyabiashara.

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akiwahimiza TRA kukusanya kodi bila kuwafungia biashara wafanyabiashara wanaodaiwa wala kuwanyanyasa.

TRA wanapaswa kutembea kwenye maagizo ya Rais kwa kuhakikisha inawaongoza wafanyakazi wake nchi nzima kufanya kazi kwa weledi na kujenga urafiki na wafanyabiashara badala ya kujenga mazingira ya uadui.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wazazi, watoto wakimaliza mitihani nyinyi hamjamaliza kulea, bado sana!

Na Adam Fungamwango

**MARA** zote inapofikia tarehe hizi za mwisho wa mwaka, na hasa kwa wanafunzi, huwa inakuwa ni wakati wa hekaheka za mitihani ambayo mara nyingi huanza nayo tangu mwishoni mwa Septemba.

Hapo kwa ufupi, tunamtaja mwanafunzi wa darasa la nne, kaka na dada zake wenyewe tuliwaita sana kwa jina la 'LY'. na nimaamini jina hili halijaoza kwa wale wa , darasa la saba.

Hekaheka hiyo ya mitihani pia inatikisa kwa wakubwa zaidi wa kidato cha pili, hadi wa huko juu, kidato cha nne. Ni msimu wa kuvuna walichokipanda, hali kadhalika ndiyo mwelekeo wa maisha yao njia zake zinapokuwa dhahiri zaidi na wale wa darasa la nne na kidato cha pili, mzazi anaanza kushuhudia 'laivu' uzembe wa mwanaye au ubovu wa shule na mwalimu.

Ukirejea kwa mzazi, siyo siri kwa kiwango kikubwa cha familia zetu, hasa pale akihitimu darasa la saba au kidato cha nne, mzazi hupumua kwamba tayari ameutua mzigo, akinywa maji kutazama huku na kule asonge vipi kumvusha huyu kijana wake ambaye hawezi kumkwepa kwa lolote lile.

Na hata pale akithubutu hilo, sheria inamvuta kola la shati au dera lake kumrejesha tena kwenye njia yake hadi kituo msaada miaka 18, hapo atake asitake habari ndiyo hiyo.

Hata inapokuwa mzazi ameutua mzigo wa gharama ya shule, lakini bado kula kulala, mavazi na kesi ndogondogo analo hilo. Maana yake nini jamani? Hapo kwa kifupi hata mtoto anapomaliza mtihani jukumu la kumfutilia kinidhamu na njia ya maisha iko pale pale kwako mzazi.

Sanasana tofauti ni namna tu ya kuhudumia, wote pamoja, baba au mama mnapotegeana majukumu. Hapohapo, najua mtaani wapo kunguru wengi tu wanamuweka mtoto hatarini ambaye anajinasibu eti na yeye ni mkubwa, kumbe thubutu!

Upeo wake mdogo, uwezo wake hivyo hivyo, hana chochote anachomudu hata hiyo miaka 18 ya serikali akiifikia, safari bado ni ndefu tu.

Na ndiyo maana mama yetu wa Taifa aliliona hilo, hata akawapa mbeleko wazazi waendelee kwa kadi zao za bima ya afya, wawahudumie watoto wao mpaka miaka 21, walau hapo anakua kijimtu.

Kutokana na hilo, wazazi tuendelee na hawa watoto kumaliza licha ya mtihani tusijisahau, tunahitaji kuwachunga pale pale ila kwa staili tofauti, maana nje ya tu ya geti au nyumba, kuna vibanda umiza, mawakala kibao wa shetani.

Iwe vyovyote vile, kipindi ambacho watoto wamemaliza kufanya mtihani na wanapumzika nyumbani wakisubiri mhula mwingine ni cha hatari sana kama wazazi hawakuwa makini.

Kuna wakati hata watoto wenyewe wanajisahau na kujikuta kama siyo, badala yake wanaanza kufanya mambo kama watu wazima.

Ni kwa sababu hawapo shule kwa wale wa zile za mabweni na wale wa shule za kwenda kila siku hawaendi wako likizo na wapo mbali na 'mnoko' mwalimu wa nidhamu. Hivyo kujisahau na kuingia kwenye mitego ambayo hawakutegemea.

Hiki ndicho kipindi cha hatari zaidi kwa wanafunzi kuharibikiwa kama hawatoangaliwa vizuri.

Kwa wale watoto wa kike ambao wana miaka 18 kwenda juu wananasa na kuanza staili mpya ya maisha.

Ni kipindi ambacho kwa mabinti hupata vishawishi kutoka kwa manyang'au, lakini wao wenyewe kudanganyana na kwenda kwenye sherehe mbalimbali za kijamii na huko hukutana na mambo mengi, bila kusahau mavazi yasiyokuwa na adabu.

Pia wapo wazazi wanawafanya watoto wao kujiingiza kwenye maeneo hatarishi kama vile kuwatuma kufanya biashara ndogo ndogo ambazo hukutana na watu wanaowapa vishawishi na hatimaye kudharau masomo, inafikia binti kupata ujauzito, mama kijana kuwa bibi.

Kwa wavulana nao pia huu ni wakati wa kuwaangalia zaidi kwani hujiingiza kwenye makundi hatari ya kuvuta bangi, dawa za kulevya, au kamari, kesho na kesho kutwa anakuwa teja 'skuli mwanangu is not good.'

Najua kuna wazazi ambao mtoto akimaliza kidato cha nne yeye amemaliza, hana tena uwezo wa kumsomesha, ni zamu ya mtoto kupambana mwenyewe.

Salamu kuu hapo ni nini? Wazazi, watoto wakimaliza mitihani, nyinyi hamjamaliza kulea "Kazi Iendelee".

## HABARI KITAIFA

# PPRA: Maofisa maendeleo jamii daraja muhimu makundi maalum

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAMLAKA ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), imewakumbusha maofisa maendeleo ya jamii nchini, umuhimu wa kada yao kama daraja la kusaidia makundi maalum kupata fursa za zabuni za umma zilizotengwa kwa ajili yao.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Eliakim Maswi, alisema hayo alipokuwa akizungumza katika kikao kazi cha wakuu wa vitengo na Idara za Maendeleo ya Jamii, Mamlaka za Serikali za Mitaa, kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.

Maswi aliwaambia maofisa hao kuwa ili makundi hayo maalum ambayo ni wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu yaweze kupata fursa za serikali ni lazima wapate usajili kutoka katika halmashauri zao na moja ya wasajili hao ni Maofisa Maendeleo ya Jamii.

"Ni kweli fursa za zabuni zipo, serikali inatenga fedha hizo katika mpango wa mwaka wa ununuzi wa kila taasisi nunuzi, hata hivyo ni lazima makundi hayo yawe mmeyasajili ninyi Maofisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za halmashauri," alisema. Maswi alisema kwa sasa PPRA ipo katika kampeni maalum ya kuhamasisha makundi maalum kujitokeza katika fursa za zabuni za serikali. Hata hivyo, Mamlaka imebaini kuwa hatua ya usajili wa makundi maalum imekuwa na ombwe kati ya maofisa maendeleo ya jamii na wananchi.

Ofisa Mtendaji Mkuu huyo alisema, kupitia kampeni hiyo iliyofanyika katika mikoa ya Rukwa, Tabora, Mwanza, Dodoma, Arusha, Mtwara na Manyara, wamebaini kuwa maofisa hao wengi hawakuwa na uelewa kuhusu uwapo wa fursa hizo hali iliyosababisha kuwa na vikwazo na urasimu katika baadhi ya halmashauri, hatua ambayo inafifisha juhudi za serikali kuwawezesha wananchi kupitia makundi maalum. "Uzoefu tuliopata kupitia kampeni ya elimu kwa umma kuhusu hizi fursa za makundi maalum, ambapo mwaka huu wa fedha kuna zaidi ya Shilingi trilioni tisa (9,000,000,000) zilizotengwa kwa ajili ya haya makundi maalum, tumebaini kulikuwa na vikwazo na urasimu ambao unakwamisha usajili," alisema Maswi na kuwataka maofisa hao kuboresha utendaji wao wa kazi katika eneo hilo. Alisema anatarajia endapo wataboresha utendaji wao katika usajili wa vikundi, kutakuwa na ongezeko la vikundi nchini vitakavyoorodheshwa na PPRA kwa ajili ya fursa hizo, kwa kuwa hadi sasa kuna vikundi 195 pekee nchi nzima vilivyoorodheshwa, idadi ambayo haiendani na uhitaji na ukubwa wa nchi.

Aliwataka maofisa hao kuiga mfano wa wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa na viongozi wengine katika mikoa waliyotembelea walionesha ushirikiano mzuri kufanikisha kampeni hiyo ambayo itaongeza fursa za ajira na kusaidia kuboresha maisha ya wananchi kupitia ununuzi wa umma.

Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura ya 410 inaitaka kila taasisi nunuzi kutenga asilimia 30 ya bajeti yake ya mwaka ya ununuzi wa umma kwa ajili ya makundi maalum ambayo ni vijana, wanawake, wazee na watu wenye ulemavu.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange (wa pili kushoto), akiwa na Mbunge wa Same Mashariki, Anne Kilango (wa tatu kushoto), walipotembelea kukagua majengo ya kituo cha Afya kata ya Vunta, wilayani Same, mkoani Kilimanjaro jana, ambapo waziri huyo, hakuridhishwa na hadhi ya kituo hicho na kutoa Sh. milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa awali wa kituo kipya kitakachokuwa na majengo ya upasuaji pamoja na chumba cha kuhifadhia maiti. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Wizara yataka miongozo TCU kupitiwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeutaka Umoja wa Makamu Wakuu na Marasi wa Vyuo Vikuu vya Binafsi (TAPU), kupitia vizuri miongozo mbalimbali inayotolewa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), ili waielewe na kuizingatia.

Akizungumza na Umoja huo jijini hapo hivi karibuni, Katibu Mkuu wizara hiyo, Dk. Francis Michael, aliutaka kushirikiana na TCU kuandaa mitaala inayojibu mahitaji ya soko la ajira na kujenga uwezo wa wahitimu kujiajiri na kuajiriwa.

Vile vile, alisema TCU ni chombo cha serikali chenye jukumu la kusimamia utoaji wa elimu ya juu, kilichoundwa kisheria huku akiitaka TCU kufanya kazi kwa kuzingatia sheria ya uanzishaji wake bila kuonea au kubagua.

"Tutafanikiwa katika hili iwapo tutakuwa na rasilimali watu ya kutosha na mazingira bora na rafiki ya kutolea elimu. Nitoe wito kwa TCU kuhakikisha wanaweka mazingira rafiki na sawia ya miongozo ya kutolea elimu iliyo bora kwa vyuo vikuu vyote nchini bila kujali aina ya chuo, hadhi na umiliki wa chuo," alibainisha Katibu Mkuu huyo.

Akitolea ufafanuzi kuhusu ombi la TAPU kuona uwezekano wa serikali kupandisha hadhi zahanati, vituo vya afya na hospitali za vyuo vikuu binafsi, zisaidie kama hospitali za kujifunzia, Dk. Michael alisema suala hilo linatekelezwa na wizara nyingine na TCU ina maelekezo maalumu ya aina ya hospitali inayokidhi kutolea mafunzo.

Aliishauri TAPU kuingia mikataba ya makubaliano (MoU) na hospitali za serikali ama za binafsi zenye sifa na hadhi ya kuwezesha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa udaktari na masomo yanayofanana na hayo, ili kupunguza gharama huku akitafuta utatuzi endelevu wa changamoto hiyo kwa kuwa na mpango wa uwekezaji katika ujenzi wa hospitali za kufundishia kama takwa la msingi na la lazima la chuo kikuu chochote kinachotoa programu za afya.

Alitoa rai kwa umoja huo kuweka utaratibu mzuri wa kutoa taarifa kuhusu mikopo hususani mwaka wa masomo unapoanza ili kuondoa malalamiko kutoka kwa wanafunzi kuhusu mikopo.

"Naomba mtusaidie kuondoa ama kupunguza malalamiko kutoka kwa wanafunzi kwa kuhakikisha wanapata taarifa kamili, sahihi na kwa wakati kuhusu suala la mkopo kwa kila mwanafunzi na namna ya fedha hizo zinavyomfikia mwanafunzi kwa haraka zaidi," alisisitiza Dk. Michael.

Kwa Upande wake, Mwenyekiti wa Umoja wa Makamu Wakuu na Marasi wa Vyuo Vikuu Binafsi, Pius Peter aliishukuru wizara kwa kukubali kukutana nao na kujadili kwa pamoja changamoto wanazokabiliana nazo katika uendeshaji na usimamizi wa vyuo hivyo.

Alisema wameridhishwa na majadiliano waliyofanya na serikali na baadhi ya hoja zao zimepata utatuzi huku nyingine zikiendelea kufanyiwa kazi.

Alisema wana imani kuwa serikali itatua changamoto zote ili kuwezesha watoto wa kitanzania kupata elimu ya juu bora kupitia vyuo vikuu vya binafsi ambavyo vina dahili asilimia 32 ya wanafunzi wote wa elimu ya juu.

## KABWELA






Gavana wa Klabu ya Rotary Kanda ya Uganda na Tanzania, Peace Teremwa (wa pili kulia), akimkabidhi Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwananyamala B, Modesta Mushi (wa pili kushoto) dawati wakati wa hafla ya makabidhiano ya madawati 100 yaliyotolewa na klabu hiyo. Kushoto ni Mbunge wa Kinondoni, Tarimba Abbas na kulia ni Rais wa Klabu ya Rotary ya Dar es Salaam, Nikki Aggarwal. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rotary yapiga jeki maendeleo ya elimu

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Rotary ya Dar es Salaam, imekabidhi mchango wa madawati mapya 100 kwa Shule ya Msingi Mwananyamala na kutimiza idadi ya jumla ya madawati 1,700 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 250 ambayo klabu hiyo imeshatoa kwa shule mbalimbali hapa nchini.

Madawati hayo yalikabidhiwa na wanachama wa klabu hiyo wakiongozwa na Gavana wa Klabu za Rotary kwa nchi za Uganda na Tanzania, Peace Teremwa na kupokelewa na Mbunge wa Kinondoni, Tarimba Abbas, Novemba 16, mwaka huu.

Akizungumza wakati wa kukabidhi madawati hayo, Rais wa Klabu hiyo, Nikki Aggarwal, alisema klabu hiyo imekuwa ikishirikiana na jamii katika kuboresha huduma za jamii kwa kuendesha miradi mbalimbali ya kijamii ambapo kwa sasa mradi wao mkuu ni wa kutoa madawati kwa shule zenye uhitaji.

Alibainisha kuwa mradi huo unakwenda sambamba na upandaji miti ili kuhifadhi mazingira.

"Hadi sasa mradi huu umeshatoa madawati takribani 1,700 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 250 kwa shule mbalimbali. Tunafurahi sana kuona kuwa mradi huu umekuwa wa manufaa makubwa kwani umewatoa wanafunzi wapatao 5,000 kwenye adha ya kukaa kwenye sakafu wakati wakiwa darasani," alisema.

Alisema kwa kuwa moja ya malighafi katika kutengeneza madawati ni mbao, mradi huo unakwenda sambamba na upandaji wa miti ili kutunza mazingira.

Akizungumza wakati wa hafla ya kupokea madawati hayo, Mbunge wa Kinondoni, Tarimba Abbas, alisema Kinondoni ni miongoni mwa majimbo yanayohitaji madawati kwani kumekuwa na ongezeko la wanafunzi wanaoandikishwa shuleni kutokana na sera ya serikali ya kutoa elimu bure.

Kwa mujibu wa Tarimba, msaada huo wa madawati ni muhimu sana kwa kuwa umekuja kwa wakati muafaka na utaisaidia serikali kutumia fedha ambazo zingenunulia madawati kuimarisha miundombinu mingine katika shule zetu.

Tarimba aliipongeza klabu ya Rotary kwa kazi kubwa inayofanya kusaidia jamii katika sekta mbalimbali za kijamii na ameihakikishia ushirikiano wa hali na mali ili kufanikisha malengo ya kuleta maendeleo kwa jamii yetu.

# UWT yakumbushwa kuchagua viongozi bora

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Christine Mndeme, amewataka viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), kuchagua viongozi bora watakaowatumikia Watanzania kwa usawa na kusimamia uhai wa chama.

Akifungua mkutano wa uchaguzi wa UWT, Mkoa wa Dodoma jana jijini hapo, Mndeme alisema Watanzania wote ni wa kwao wanatakiwa kuwatumikia kwa usawa. Aidha, alisema viongozi hao wanapaswa kusimamia suala la kuongeza wanachama, ulipaji ada ya uanachama, kusajili kwa mfumo wa kielektroniki na kushiriki vikao.

"Tusimamie ilani ambayo inaendelea kutekelezwa na Rais Samia Suluhu Hassan, twendeni tukasimamie chama chetu maana kipo imara na kinasonga mbele," alisema.

Alisema mwelekeo wa chama ni mzuri watembee kifua mbele.

Naye Katibu wa CCM, Mkoa wa Dodoma, Pili Augustino, aliwataka wajumbe kuchagua viongozi watakaosaidia kukijenga na kuimarisha chama ili kufanya vizuri uchaguzi wa serikali za mitaa 2024 na Mkuu 2025.

Kwa upande wake, Katibu wa UWT Taifa, Dk. Philis Nyimbi, aliwataka wajumbe kuchagua viongozi bora watakaokitumikia chama vizuri.

"Tutaendelea kukitetea chama katika ngazi mbalimbali kuelekea kwenye chaguzi mbalimbali zijazo, hivyo kila mmoja wetu ajue ana jukumu la kuendelea kumuunga mkono Rais Samia na serikali kwa ujumla, tuwaunganishe wanawake ngazi zote ili tushikamane tuwe kitu kimoja," alisema.

# Jamii yashauriwa kufuata maelekezo ya wataalamu

**Na Halfani Chusi**

MKURUGENZI Msaidizi wa Tiba Wizara ya Afya, Dk. Gerald Horumpende, ameishauri jamii kufuata ushauri unaotolewa na wataalamu wa afya ili kujikinga na magonjwa ambukizi.

Horumpende alitoa ushauri huo jana jijini Dar es Salaam, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, katika hafla iliyowakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya afya, wakiwamo wabunifu kujadili namna teknolojia ya habari inavyoweza kuboresha huduma za afya.

Alisema kama jamii ikitambua namna ya kutumia teknolojia hiyo itasaidia kujua namna sahihi ya kujikinga na magonjwa ambukizi ambapo wengi wao wameyapata kwa kukosa taarifa sahihi.

"Wizara ya Afya imejikita katika kutoa huduma bora na namna ya kutoa taarifa sahihi juu ya magonjwa ya kuambukiza yanayoweza kudhibitiwa kupitia teknolojia

Pia itasaidia kuepusha gharama kwa sababu mtu akijua namna ya kujikinga na magonjwa ya kuambukiza anaweza kuepuka gharama za kwenda hospitalini kutibu vitu ambavyo vinaepukika

Kila mwaka serikali kwa kushirikiana na Chuo cha Afya cha Muhimbili (MUHAS), imekuwa ikiandaa maonyesho kwa ajili ya wabunifu mbalimbali waliobuni vifaa tiba na kuhamasisha watu kutumia TEHAMA kupata taarifa sahihi.

Aidha, aliwataka Watanzania, kupuuza taarifa za upotoshaji zinazotolewa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu sekta ya afya.

"Mitandaoni watu wengi wanaongea taarifa nyingi kuhusu masuala yanayohusu sekta hii lakini kabla hujaziamini ni bora ukajiridhisha, ili kujua kama zinatoka katika vyanzo vya kuaminika," alisema.

Kama mnavyojua mtandaoni kila mtu anatuma ujumbe wa kile anachojisikia mwenyewe, kwa hiyo hilo nalo jamii inapaswa kuliangalia kabla ya kuamini kile alichokiona kwenye mtandao," alisisitiza.

**MBUNIFU ANENA**

Awali mratibu wa mradi unaojihusisha na uokoaji wa maisha ya mama na mtoto kutoka Hospitali ya Kilutheri ya Haydom iliyoko Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, ambao wanajihusisha na ubunifu, Beatrice Githiri, alisema kwa miaka miwili ya mradi huo wamefanikiwa kuokoa mamia ya watoto kupitia ubunifu wao.

"Siwezi kukumbuka idadi ya watoto ambao tumewaokoa kwa miaka hii miwili tangu tulipoanza kujihusisha na utoaji wa huduma hii, tumeokoa mamia ya watoto kwa kutumia vifaa tiba vya ubunifu,"alisema.

Sasa tumebuni kifaa kinachoitwa moyo ambacho kazi yake ni kutambua mapigo ya moyo kwa mtoto aliyeko tumboni mwa mama hiki kinawasaidia wakunga kujua kama mtoto anapokuwa tuboni anapumua kwa ufasaha au kuna tatizo.

# Aeleza jinsi alivyowakamata wachukuzi na misokoto ya bangi

**Na Mwandishi Wetu**

ASKARI Koplo Ramadhani wa Kituo cha Bandari Dar es Salaam, ameieleza mahakama jinsi alivyowakamata wachukuzi wawili wakisafirisha robota la nguo za mitumba ndani likiwa na misokoto 4,491 ya bangi kuelekea Zanzibar.

Shahidi huyo wa kwanza wa Jamhuri alidai hayo jana katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, mbele ya Hakimu Mkazi Rehema Liana, wakati akitoa ushahidi katika kesi ya kusafirisha dawa za kulevya.

Alidai Januari 6, 2021 saa 12 jioni alikuwa kazini maeneo ya Azam Marine na askari mwenzake mwenye namba H9493 PC Jose.

Alidai walifanya ukaguzi wa abiria na mizigo katika meli ya Azam Sea Link 1 iendayo Zanzibar, baada ya kupata taarifa kuna robota la nguo za mitumba litapitishwa ndani yake lina bangi.

"Tukiwa katika ukaguzi tulimuona mtuhumiwa Abeid Ismail, kajitwisha robota la mitumba anapeleka katika meli ya Azam, nilipomuhoji alisema yeye ni mbebaji, mzigo wa Twaha Sultani.

"Alidai alilipwa Sh. 25,000 kwa kubeba, tulimtaka ampigie simu Twaha aje eneo la tukio, alifanya hivyo na Twaha alifika, alidai mzigo aliutoa Kariakoo," alidai Koplo Ramadhani.

Aliendelea kudai kuwa aliwafahamisha watuhumiwa kuwa ndani ya robota la nguo kuna dawa za kulevya aina ya bangi, waliita mashahidi huru wawili, Hassan Saidi na Ramadhani Iddi.

"Tulifungua robota la nguo tukakuta vifurushi tisa, tulipotoboa vifurushi tulikuta vifurushi nane kila kimoja kilikuwa na misokoto 500 na kifurushi cha tisa kilikuwa na misokoto 491, jumla ya misokoto ni 4,491."

Aidha, alidai kupeleka kielelezo kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ikabainika kuwa ni bangi kilo 26.86.

Shahidi aliomba kutoa hati ya ukamataji na bangi kama vielelezo mahakamani, washtakiwa hawakupinga, vielelezo hivyo na vilipokelewa.

Washtakiwa walipanda kizimbani wakiwa na 'counter book' yenye vifungu vya sheria.

Huku akisoma kwenye daftari, Abeid alidai shahidi anakiuka Kifungu cha Sheria namba 38(3) cha Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) kinachotaka hati ya ukamataji mali iwe na saini tatu.

Alidai hati hiyo haina kibali cha kufanya upekuzi kama mwongozo wa Jeshi la Polisi (PGO) namba 229 unavyoelekeza.

Washtakiwa pamoja na hoja hizo waliruhusu kesi iendelee na walikubali vielelezo pia vipokelewe na mahakama ilipokea. Kesi iliahirishwa hadi tarehe nyingine itakayopangwa.

# RC ataka mkakati kuondoa daraja sifuri mitihani ya elimu sekondari

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewaagiza viongozi wa idara ya elimu kujipanga kuhakikisha wanaondoa matokeo ya daraja la sifuri kwa mitihani ya taifa ya kidato cha nne katika shule za sekondari mkoani hapo.

Akizungumza katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) jana, Serukamba alisema ili kuhakikisha kiwango cha elimu kinapanda mkoani hapa, maofisa elimu wa kata wasiachiwe jukumu la kusimamia elimu pekee yao na badala yake viongozi wa halmashauri na kata wawajibike katika jukumu hilo.

"Natamani mitihani ya 'form four' (kidato cha nne) tuondoe divisheni ziro. Tutaitisha kikao na ma-DC (wakuu wa wilaya, wakurugenzi, maofisa elimu, wenyeviti wa halmashauri na wazazi tujadiliane tuone ni namna gani tutainua kiwango cha elimu mkoani Singida," alisema.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dorothy Mwaluko, alisema mkoa ulifanya tathmini ya utoaji elimu katika shule za msingi na sekondari Februari, mwaka huu ambayo tathmini ilibaini mafanikio na changamoto, hivyo kuandaliwa kwa mkakati wa kuboresha mazingira ya utoaji elimu kwa miaka mitatu. Alisema katika kipindi cha miaka hiyo, mikakati imebainisha mambo yatakayotekelezwa kuwa ni kuboresha mahudhurio ya walimu na wanafunzi shuleni, kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo na kuimarisha uwajibikaji na ushiriki.

Mwaluko alisema katika kuboresha mahudhurio kwa wanafunzi shuleni huduma ya utoaji wa chakula shuleni imeanzishwa ambapo katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2022 shule 187 kati ya 609 za msingi zinatoa chakula kwa wanafunzi. Alisema kwa shule za sekondari zinazotoa chakula ni 146 kati 168 sawa na asilimia 87 na shule hizo zinatoa chakula hicho kupitia michango ya wazazi, walezi na shule 12 zenye wanafunzi wa bweni zinapata ruzuku ya serikali. Aidha, Katibu Tawala wa Mkoa alizitaka shule zianishe miradi ya elimu ya kujitegemea ili kuwezesha upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi shuleni.




Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, Abdallah Possi (katikati), akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wakubwa Benki ya CRDB, Jacob Nangi (kushoto), alipotembelea banda la benki hiyo, katika maonyesho yanayoenda sambamba na Mkutano wa Rais Samia Suluhu Hassan na Mabalozi, Unguja Zanzibar juzi. Benki hiyo ni mmoja wa wadhamini wa mkutano huo. Kulia ni Meneja Mwandamizi Uhusiano wa Biashara wa benki hiyo, Lulu Melo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kortini madai wizi, udanganyifu na kughushi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WAFANYAKAZI watano wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato na mkandarasi wa Kampuni ya Resa Roofers, wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Chato mkoani Geita kwa mashtaka matano.

Mashtaka hayo ni kutumia nyaraka kwa lengo la kumdanganya mwajiri, kughushi, matumizi mabaya ya madaraka, ufujaji na ubadhirifu, kitendo ambacho kimedaiwa kuwa ni kinyume cha sheria.

Washtakiwa waliofikishwa hapo mahakamani ni Jovith Katambi (41) ambaye ofisa ununuzi msaidizi wa halmashauri, Samweli Richard (29) ambaye ni mkandarasi wa Kampuni ya Resa Roofers iliyoko Mwanza na Walter Ndimbo (52) mjumbe wa Bodi ya Zabuni Halmashauri ya Wilaya ya Chato.

Wengine ni David Sinyanya (45), Martine Ndamo (43) na Gastone Missungwi (43) ambao wote ni wajumbe wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Chato.

Washtakiwa hao wote kwa pamoja walipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Amalia Mushi, na baada ya kusomewa mashtaka yanayowakabili, walikana kuhusika nayo. Mushi alisema washtakiwa ambao watakuwa nje kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ya dhamana ni Katambi, Ndimbo, Sinyanya, Ndamo (43) na Missungwi huku Richard ambaye ni mkandarasi akipelekwa katika mahabusu ya Gereza la Wilaya ya Chato baada ya kukosa wadhamini.

Katika kesi hiyo upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Antidius Rutayuga, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Mushi alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Novemba 30, mwaka huu.

Akisoma hati ya mashtaka, Rutayuga alidai kuwa katika shtaka la kwanza, Katambi (41) akiwa ameajiriwa na Halmashauri ya Wilaya ya Chato kama ofisa ununuzi msaidizi, Mei 11, 2021 aligushi nyaraka kwa lengo la kumdanganya mwajiri wake.

Rutayunga alidai kuwa mshtakiwa huyo alitumia nyaraka za uongo ambazo ni hati ya kupokea vifaa yenye namba GRN 2021000337 ya Mei 11, 2021 ya kuonyesha kwamba alikuwa amepokea mabati 714 kutoka Resa Roofers Ltd yenye thamani ya Sh. 19,992,000 kitu ambacho alijua ni cha uongo.

Katika shtaka la pili, alidai kuwa Richard ambaye ni mfanyabiashara wa Kampuni ya Resa Roofers, Februari 23, 2021 huku akijua na kwa nia ya kudanganya, aliwasilisha nyaraka za uongo ambayo ni P.I.NO.C.T.O/KDC OF/003 ya Aprili 23 mwaka 2021 aliwasilisha kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chato akijifanya kuwa alikuwa na uwezo wa kufanya ukandarasi wa kuleta mabati 714 yenye thamani ya Sh. 19,992,000 kwa jina la Kampuni ya Resa Roofers Ltd yenye TIN namba 125-619-819 huku akijua kuwa yeye hakuwa amesajiliwa kama kampuni.

Shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa Katambi, Ndimbo, Sinyanya, Ndamo na Missungwi, Aprili 23, 2021 walitoa zabuni kwa mtu aliyejiita Resa Roofers Ltd bila ushindani kitu ambacho kilimfanya Richard kupata manufaa yasiyokuwa ya halali.

Katika shtaka la nne, alidai kuwa washtakiwa wote kwa pamoja, Aprili na Juni, 2021 wakiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato na wakiwa wameajiriwa na halmashauri hiyo, walisababisha Richard kulipwa Sh. 19,992,000 zilizokuwa zimekasimiwa kwao kama watumishi wa umma kupitia na kuipa Kampuni iitwayo Resa Roofers Ltd ambaye ni mkandarasi kwa njia isiyo kuwa na shindani na kufanya fedha hizo zilizokuwa zimeandaliwa kwa ajili ya mabati ya kusababisha halmashauri kushindwa kupata mabati hayo.

Wakili huyo alidai kuwa shtaka la tano ni kwa mshtakiwa Richard ambaye akiwa mfanyabiashara kwa jina la biashara ya Resa Roofers, Aprili 23, mwaka 2021, kwa lengo la kudanganya, alighushi P.I.NO.C.T.O/KDC OF/003 ya Aprili 23, 2021 akijifanya kuwa yeye ni wa kampuni ya Resa Roofers Ltd wakati kampuni hiyo haikuwapo.

# Ukerewe waomba chakula cha msaada

**Na Vitus Audax,** UKEREWE

WANANCHI wilayani Ukerewe mkoani Mwanza wameiomba serikali kutatua changamoto ya upatikanaji wa chakula wilayani humo kwa kupeleka chakula kwa gharama nafuu ili kuokoa maisha ya wakazi wa wilaya hiyo.

Ombi hilo linakuja kufuatia mfumuko wa bei za vyakula unaozidi kuwaelemea kutokana na hali ya ukame inayosababishwa na ukosefu wa mvua kwa kipindi kirefu, huku mazao yakikauka na kusababisha ukosefu wa mavuno.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wananchi hao pamoja na madiwani katika wilaya ya Ukerewe wamesema bei za vyakula zimekuwa juu kulinganisha na misimu mingine na kuiomba serikali kuingilia kati kuwasaidia wananchi hao kupata chakula.

Fortunatus Ndasilo ni mkazi wa Kisiwa cha Nansio wilayani Ukerewe, alisema majira kama haya wakulima wilayani humo wanakuwa wanavuna husussani mazao ya muda mfupi, ikiwa ni pamoja na mahindi na viazi lakini kutokana na hali ya hewa hawajafanikiwa kupata mavuno yoyote kwa kipindi hiki.

Naye, Dickson Chaundi, Diwani wa Kata ya Busya alileleza gazeti hili kuwa bei ya chakula imepanda kwa kasi zaidi ya misimu yote, na kwamba mahindi kipimo cha 'shambani' (sawa na Kg 2.5) ni Sh.5,000 mpaka Sh.5,500 kwa maeneo ya visiwa vya ndani zaidi huku awali viliuzwa kwa Sh.2,500 hali inayowatesa wananchi wilayani humo.

Akizungumza na gazeti hili juu ya mipango ya serikali katika upatikanaji wa chakula wilayani humo, Kaimu Mkurugenzi wa Wilaya hiyo, Mangoha Maginga , alisema katika hatua za awali serikali tayari imepeleka tani 100 za mahindi ya ruzuku ambazo zitauzwa Sh.920 kwa kilo moja, ili kuinusuru hali ya wananchi wilayani humo.

Aidha, alitoa rai kwa viongozi mbalimbali ambao watafikishiwa mahindi hayo kwa ajili ya kuyasambaza katika maduka husika kuwa waaminifu na kuhakikisha zinawafikia wananchi wote wenye uhitaji, huku serikali ikiendelea kufanya mpango wa kuwafikishia wananchi hao tani nyingine 200 ili kukidhi mahitaji yao.

"Tayari tumewaagiza maofisa kilimo kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi na wakulima wote kuhakikisha wanakuwa na uelewa wa mazao gani wapande katika kipindi hiki ambacho mvua hazitabiriki ili kujinusuru na baa la njaa pamoja na kuzalisha kwa wingi ili kukabiliana na mfumuko wa bei za vyakula," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi kutokutegemea mahindi hayo ya misaada kwa asilimia kubwa bali watumie fursa ya mvua hizi zinazonyesha kuhakikisha wanapanda kwa wakati na kufuata utaalamu katika kilimo ili kujipatia mazao ya kutosha.




Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia), akionyesha kitabu kipya cha Novice kinachohusu jinsi ya uendeshaji wa Bodi za taasisi na mashirika kwa ufanisi, baada ya kukizindua jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mtunzi wa kitabu hicho, Ntangeki Nshala (katikati) na Waziri wa zamani wa Ardhi, Prof. Anna Tibaijuka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shahidi aieleza mahakama alivyomhoji mshtakiwa anayedaiwa kumuua daktari

**Na Grace Gurisha**

SHAHIDI Sajenti Hamad Rashid ameieleza Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kuwa wakati anamhoji mshtakiwa, Julius Chacha alikubali kuhusika na mauji ya Dk. Honoratus Mbunda wa Zahanati ya Miko aliyepigwa risasi Novemba 30, 2017.

Aidha, Rashid amesema hayuko tayari maelezo aliyomchukua mshitakiwa Chacha kupokelewa kama kielelezo kwa sababu hayajakidhi vigezo.

Rashid alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Elizabeth Nyembele wakati akitoa ushahidi dhidi ya Chacha anayetuhumiwa kumuua Dk. Mbunga akiwa katika eneo lake la kazi, Kijiji cha Chakenge Kata ya Msongola, Ilala, Dar es Salaam.

Alidai kuwa Desemba Mosi, 2017 majira ya saa sita mchana akiwa katika Kituo chake cha kazi Chanika alipokea jalada la mauji kutoka kwa mkuu wake wa kazi ASP Abubakar Zebo kuwa aendelee kufanya uchunguzi. Alidai kuwa alikwenda eneo la tukio na kuchora ramani Desemba Mosi, 2017 huku akioneshwa mazingira na mwenyeji wa eneo hilo Chacha Mwita, alikuta damu imechurizika kutoka mlangoni hadi nje ya zahanati hiyo.

Shahidi huyo alidai kuwa Desemba 13,2017 mshitakiwa alikamatwa eneo la Bolole ndani ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam na alipomuhoji alikiri kuhusika na mauaji ya daktari huyo huku akishirikiana na wenzake wawili.

Alidai kuwa mmoja wa wenzake hao aliwaeleza kwamba kuna kazi wanatakiwa kwenda kuifanya kwa Dk. Mbunda ambapo kuna mteja anampelekea fedha nyingi, kwa hiyo wanatakiwa kwenda kuzichukua.

Alidai alibaki kwenye baa iliyopo karibu na zahati hiyo kwa ajili ya kuangalia mazingira, aliposikia mlio wa risasi akajua kazi tayari akaondoka kwenda kukutana na wenzake walimueleza kuwa tayari waliyokuwa nayo haikuwa sahihi daktari hana fedha.

Ilidaiwa kuwa mshitakiwa aliachana na wenzake hao hadi siku aliyokamatwa, ambapo wenzake hao hadi leo bado hawajakamatwa. Januari 20, 2018 mshitakiwa alifanyiwa gwaride la utambulisho akatambuliwa na shahidi.

Wakati shahidi anaulizwa maswali na Wakili wa Mshitakiwa, Mohamed Majaliwa alidai alichukua maelezo ya mshitakiwa na alipoulizwa kwa nini hakuyatoa mahakamani kama kielelezo?.

Akijibu swali hilo, Rashid alidai kuwa hakuyatoa mahakamani kama kielelezo kwa sababu hayajakidhi vigezo, ambapo Majaliwa alimueleza kwamba anataka amuombee Mahakama iyapokee maelezo hayo kwa sababu yeye anayo.

"Sipo tayari maelezo hayo yapokelewe kama kielelezo kwa sababu hayajakidhi vigezo,"alidai Shahidi Rashid. Kesi imeahirishwa hadi leo kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa.

# FEMINA Hip yaadhimisha miaka 20 ya Klabu za Fema

**Na Frank Monyo**

FEMINA Hip kwa kushirikiana na Ubalozi wa Denmark na Sweden, wameadhimisha miaka 20 ya Klabu za Fema tangu kuanzishwa kwake.

Klabu za Fema ni klabu za nje ya darasa ambazo zinafanya kazi katika shule za sekondari na vyuo vya kati kote nchini ambazo ni mahali vijana hujitolea, kushirikishana na kujifunza stadi za maisha kupitia mafunzo mbalimbali.

Akizungumza jana katika maadhimisho hayo, Balozi wa Denmark nchini, Mette Norgaard Dissing-Spandet alisema:

"Imekuwa nafasi ya heshima kubwa kufanya kazi na Femina Hip katika kubadilisha maisha ya vijana nchini Tanzania."

"Kupitia ushirikiano huu, tumeona vijana wakianza kuishi mitindo bora ya maisha na kutoa mchango chanya kwenye ukuaji wa kiuchumi na kijamii." alisema Balozi Dissing-Spandet.

Mwenyekiti wa Bodi ya Femina Hip, Anna Mwasha, alisema vijana wanahitaji taarifa sahihi za kuwaongoza katika maisha yao kwa maana hiyo Femina Hip imekuwa ikifanya kazi hiyo tangu kuanzishwa kwake.

"Vijana nchini na kote duniani, wanahitaji taarifa sahihi ili ziweze kuongoza maisha yao, na nina furaha kushuhudia kwamba Femina Hip imetoa huduma hiyo kwa zaidi ya miongo miwili," alisema Mwasha na kuongeza:

"Katika siku zijazo, tunatarajia kufikia hata shule za msingi, kwa sababu ujuzi unaotolewa kupitia vyombo vya elimu ya Femina Hip (majarida ya kuchapisha, redio, mitandao ya kijamii, na majukwaa mengine ya kidigitali) ni muhimu kwa watoto wadogo pia." Alisema.

Aliongeza kuwa Femina Hip imesajili zaidi ya klabu 2,370 katika shule za sekondari na vyuo vya kati, ikiwa na zaidi ya wanachama 230,000 kwa sasa.

Alisisitiza kuwa klabu za Femina zinapewa msaada na walimu washauri zaidi ya 2,720 wanaojitoa na kujitolea, ambao ni walimu katika shule husika, pamoja na mtandao wa waliowahi kuwa wanachama wa Klabu za Fema. "Walimu washauri wa klabu hawafanyi kazi peke yao; wameungana kuunda mitandao 81 Tanzania nzima," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Femina Hip, Ruth Mlay alisema: Leo, tunayo furaha kutangaza kwamba ni miaka 20 sasa tangu klabu yetu ya kwanza ilipoanzishwa pale Liwale, mkoani Lindi. Katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, Klabu za Fema zimewashirikisha moja kwa moja na kuwainua zaidi ya vijana milioni 15 ambao wamebeba maadili, mitazamo, na ujuzi waliojifunza katika klabu na wakaingia nao katika taaluma zao, familia, na maisha ya kijamii," alisema Ruth.



# Wataalamu fedha waonya ubadhirifu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WIZARA ya Fedha na Mipango, imesema haitasita kuchukua hatua kali, ikiwamo kuwafukuza kazi wataalamu wa fedha na hesabu nchini ambao wanauweka pembeni weledi wao na kujiingiza katika masuala ya ubadhirifu wa fedha za umma.

Badala yake imewakumbusha kuwa waadilifu wanapotekeleza majukumu yao kwa kuwa washauri wazuri kwa jamii inayowazunguka katika kufanikisha dira ya maendeleo ya taifa.

Kamishna Msaidizi wa Uendelezaji wa Sekta ya Fedha kutoka Wizara hiyo, Janeth Hizza, aliwaonya wataalamu hao wakati akizungumza katika Siku ya Wahasibu Duniani, iliyofanyika katika Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA).

"Wataalamu mnapaswa kuwa waadilifu na kutanguliza weledi katika utendaji kazi wenu, kwa sababu idara hii ni muhimu kwa maslahi ya taifa. Ndugu zangu wahasibu ili kufanikisha kuhakikisha haya mnao wajibu wa kujifunza udhibiti wa fedha haramu. "Nawaombeni mkajifunze kupata huduma jumuishi za fedha na mkatumie elimu zenu kufundisha jamii, kuhusu elimu juu ya matumizi ya fedha na nidhamu ya fedha kwa ujumla. Nyie ndio mnaotegemewa katika jamii nzima inayowazunguka," alisema.

Naibu Mkuu wa Chuo, Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu wa IAA, Prof. Epaphra Manamba, alisema wahasibu wanatakiwa kufanya kazi kulingana na sheria na taratibu zilizoko, huku wakifuata maadili na matumizi sahihi ya fedha.

Katika maadhimisho hayo, Prof. Manamba aliwafunda wanafunzi akiwasihi kufanya kazi kulingana na elimu na maadili waliyopata chuoni hapo ili wakawe mfano wa kuigwa katika jamii.

Naye Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Uhasibu wa IAA, Dennis Hyera, alisema Siku ya Wahasibu duniani imekuwa na manufaa makubwa kwa kujenga mtandao na kufungua fursa mbalimbali kwa wahasibu nchini, hivyo chuo kitaendelea kuiadhimisha siku hiyo.

Pia alihimiza wahasibu kuendelea kudumisha kanuni na taratibu za kiuhasibu na kufuata viwango vyote vilivyoanzishwa na Bodi ya Wahasibu Tanzania, ili waendelee kuwa wahasibu bora wenye kuleta chachu ya maendeleo kwa Taifa zima na kuleta maendeleo katika sekta ya fedha na uhasibu.

Makamu wa Rais wa Serikali ya Wanafunzi (IAASO), Shazma Edward, alisema kupitia siku ya wahasibu duniani wamejifunza mambo mengi ikiwamo kutanguliza maadili na uzalendo katika utendaji kazi wao wa kila siku ili taaluma hiyo iendelee kuboreka zaidi.

# Madereva mabasi mikoani wafungiwa leseni

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MADEREVA watano wa mabasi ya abiria yaendayo mikoani, wamefungiwa leseni zao kati ya miezi mitatu hadi sita, kutokana na kuwa sugu wa makosa ya usalama barabarani ikiwamo kuendekeza ulevi.

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi (ACP) Justine Masejo, alisema kuwa uamuzi wa kufungia madereva hao, unalenga kukomesha matukio ya ajali za barabarani hasa tunapoelekea kipindi cha mwisho wa mwaka wa sikukuu za Krismasi na Mwaka mpya.

Aliyataja makosa hayo yanayowakabili madereva waliofungiwa kuwa ni mwendokasi na kusababisha ajali. Pia alisema madereva hao wamebainika kuwa na makosa yanayojirudia ikiwamo kuyapita magari mengine sehemu ambazo zimekatazwa kisheria.

"Mwisho wa mwaka kumekuwa na makosa ya ajali barabarani na hii tunaona sababu ya baadhi ya madereva kuwa na makosa mengi, hivyo sisi mkoa huu imejipanga kukomesha ajali hizi ili wananchi washerehekea sikukuu za mwisho wa mwaka salama,"alisema.

Kamanda Masejo alisema pamoja na adhabu hiyo, jeshi hilo limetoa elimu katika nyumba za ibada, vituo vya mabasi, shuleni, vijiwe vya bodaboda na masoko, ambako jamii imepata uelewa wa kutosha kuhusiana na sheria mbalimbali za usalama barabarani.

Baada ya kutangaza kufungia madereva hao, Kamanda Masejo, alionya madereva wanaoendelea kuvunja sheria za usalama barabarani, akisema jeshi hilo halitomwonea huruma dereva yoyote kwa makosa ya uvunjifu wa sheria za usalama barabarani.

Hivi karibuni, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini Inspekta Jenerali (IGP) Camilius Wambura, alinukuliwa akisema matukio ya ajali za barabarani, yanashika nafasi ya nane duniani kwa kusababisha vifo.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 40 ya waathirika wa ajali za barabarani ni watembea kwa miguu nchini na asilimia 60 ikibakia kwa watumiaji wengine wa barabara, kama vile waendesha bodaboda, baiskeli na magari.

"Barabara zimekuwa machinjio ya waendesha bodaboda wasio makini na hata wale wanaojitahidi kumakinika.

Na hili linaufanya usafiri huo ulioajiri idadi kubwa ya Watanzania wa kipato cha chini kuwa si salama zaidi.

"Moja ya sababu za ajali ni tabia ya baadhi ya madereva pikipiki hao kutokufuata matumizi sahihi ya barabara na sheria zinazoongoza usalama barabarani kuwa moja ya sababu hatarishi za ajali hizo," alisema IGP Wambura.



Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona (kushoto), akiteta jambo na Mkurugenzi Mtendaji Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, baada ya kikao cha wafanyabiashara kutambua fursa zilizoko katika kilimo cha zao hilo, jijini Tanga juzi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Serikali yaongeza nguvu uzalishaji mkonge

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba, amesema serikali imeweka mkazo zaidi katika usimamizi na uzalishaji wa mkonge nchini kwa kuwa ndio zao pekee lenye fursa nyingi za uwekezaji wa viwanda na kuajiri idadi kubwa ya watu.

Kwa mujibu wa Mgumba, aina ya viwanda vinavyohimizwa uwekezaji wake kwa sasa kutokana na kuwa na fursa zaidi, ni vile vya kutengeneza vifungashio ambavyo ni rafiki kwa mazingira.

Alikuwa akizungumza jana jijini Tanga alipozungumza na wakulima wa mkonge, wafanyabiashara, wajasiriamali na wadau mbalimbali wanaonufaika na mikopo ya uwezeshaji inayotolewa na Benki ya CRDB.

"Wataalamu wako hapa kwa ajili ya kuelezea fursa zipi zilizoko Tanga na namna gani Benki ya CRDB ilivyojipanga kutoa mikopo kwa wakulima. Kwenye kilimo, kuna mazao mbalimbali yanayolimwa kwa wingi Tanga, lakini linalotambulika zaidi hapa kwetu ni zao la mkonge.

"Na kwenye uendelezaji wa viwanda vya mkonge, kuna uzalishaji wa magunia kwa ajili ya kubebea mazao ya kilimo, usokotaji wa kamba na uzalishaji wa mazulia. Nafahamu Benki ya CRDB inatoa mikopo ya ununuzi wa mitambo ya kuchakata mkonge (korona) na ununuzi wa zana bora za kilimo hususani matrekta kwa ajili ya kulima na kubeba mkonge.


"Nawapongeza na ninaomba beki hii iendelee kuongeza jitihada kutafuta suluhisho la fedha katika mnyororo wa thamani kwenye kilimo cha mkonge, kwa manufaa ya Watanzania wenzetu, ambao ninyi kwenu ni wanahisa," alisema.

Baada ya kauli hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona, aliipongeza CRDB kwa kuona umuhimu wa kuwakutanisha wadau hao na kuwapatia elimu kuhusu fursa mbalimbali walizonazo ambazo zinachangia na kuchochea shughuli za maendeleo ikiwamo kilimo cha mkonge.

"Sasa hivi tunaona Mkoa wa Tanga unafunguka, bandari imepanuliwa na uwezo wa kuchukua mzigo mkubwa umeongezeka sana. Kwa hiyo zile shehena za mkonge zinazopitishwa katika Bandari nyingine, watambue kwamba sasa fursa imekuja karibu ya kupitisha mkonge na bidhaa nyingine zinazotokana na mkonge," alisema Kambona.

Aidha, Kambona alisema Bodi ya Mkonge Tanzania itahakikisha inaongeza uzalishaji na kutumia hiyo fursa vizuri zaidi katika kuongeza pato la mkoa wa Tanga.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema semina hiyo iliyoandaliwa mahususi kwa ajili ya wafanyabiashara, wajasiriamali na wadau wa CRDB mkoa wa Tanga, itawawezesha kutambua fursa zilizoko kwenye mkoa huo na benki hiyo imejipanga vipi kuwasaidia.





# Wataka uchunguzi magonjwa mpunga

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAKULIMA wanaojishughulisha na uzalishaji wa mpunga katika Skimu ya Kahe iliyoko Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wameiomba serikali kutuma timu ya wataalamu kuchunguza tatizo la magonjwa sumbufu ya zao hilo, ambayo yameanza kuathiri uzalishaji na kusababisha hasara kubwa kwa wakulima.

Magonjwa yanayosumbua zaidi na tishio kwa zao la mpunga ni 'Bacterial Leaf Blight (Kuungua kwa Majani), Rice Yellow Mottle Virus (kimnyanga), Rice Brown Spot (Baka Kahawia) na Rice Blast (Ukungu Mkuu).

Kwa nyakati tofauti jana, wakulima wa skimu hiyo, walielekeza kilio chao kwa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wakimwomba kuwaelekeza wataalamu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwenda kufanya uchunguzi kuhusu magonjwa hayo na kutoa elimu ya namna gani ya kuyakabili ili wasiendelee kupata hasara, kabla ya mazao yao kukomaa.

Kuhusu tishio la magonjwa ya mpunga linavyowatesa kwa sasa, Anangisye Athony, alisema mpaka sasa hawajui ni aina gani ya ugonjwa unaoshambulia mazao yao shambani, kabla ya kukomaa.

"Tunaomba serikali ituletee haraka maofisa ugani na wataalamu wa utafiti waje waone hali tuliyonayo. Wasikae ofisini jamani waje watembelee wakulima mashambani ili kubaini tatizo tunalolalamikia, kabla ya kuleta madhara makubwa," alisema Anangisye.

Aidha, Veronika Alex, alisema licha ya mamia ya wananchi na hasa vijana kuhamasika kujihusisha na kilimo cha mpunga na mahindi, kutokana na maeneo hayo kupata maji ya uhakika ya umwagiliaji, masoko na pembejeo za kilimo ikiwamo mbolea ya ruzuku, kinachowatesa kwa sasa ni magonjwa ya mpunga yanayoshambulia mazao.

Akizungumzia magonjwa hayo, Ofisa Ugani Mwandamizi anayefanya kazi na mashirika ya binafsi ya kilimo katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Robert Minja, alisema tishio la magonjwa hayo linapaswa kudhibitiwa haraka na serikali, kwa kuwa yana athari kubwa katika uzalishaji.

# Jaji ashauri kutafutwa suluhu migogoro katika bara Afrika

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Jaji Imani Aboud, amesema iko haja kwa Chama cha Majaji wanaoshughulikia masuala ya wakimbizi na wahamiaji Afrika, kutafuta mwarobaini wa migogoro inayosababisha kuongezeka kwa wakimbizi katika nchi za Afrika.

Jaji Aboud aliyasema hayo jana wakati wa mkutano wa kimataifa wa Chama cha Majaji Wanaoshughulika na Masuala ya Wakimbizi na Wahamiaji, unaoendelea jijini hapo.

"Tatizo la kuongezeka kwa wahamiaji katika nchi za Afrika sasa linazidi kuota mizizi. Sababu kubwa ni kutokana na migogoro ya kisiasa pamoja na mabadiliko ya tabianchi ambayo husababisha wananchi wengi kukimbia nchi zao na kwenda nchi zingine kutafuta amani, ajira na chakula.

"Kutokana na tatizo hili, ni lazima nchi za Afrika, zijitafakari na kutafuta suluhu ya jambo hilo. Kupitia mkutano huu, tutakaa chini kuangalia vyanzo vinavyosababisha kuwapo kwa wahamiaji hao na tutaweka mikakati ya namna gani ya kuondokana na tatizo. Itabidi na tuwaangalie ndugu zetu hawa kwa jicho la huruma na haki za watu, kwa kuwa wanavyofanya hivyo hawafanyi makusudi bali ni mazingira ndio yanachangia wao kufanya hivyo," alisema.

Aidha, Rais huyo alisema ni vizuri washiriki wa mkutano huo wakaangalia na kujadili kwa pamoja migogoro ya kisiasa jinsi inavyoathiri Bara la Afrika na kuja na mikakati ya kukabiliana na migogoro hiyo.

Awali, Rais wa Chama cha Majaji wanaoshughulikia masuala ya Wakimbizi na Wahamiaji Afrika (IARMJ), Jaji Isaac Lenaola, alisema lengo la mkutano huo ni kupanua uelewa wa masuala ya wakimbizi kwa maofisa wa serikali, majaji, mahakimu na watoa uamuzi wengine barani Afrika. Alisema IARMJ inaratibu kwa karibu tatizo hilo na litakuja na ufafanuzi wa kina kuhusu sheria ya wakimbizi na namna bora ya kuwahudumia pamoja na kutambua kwa kina umuhimu wa hifadhi ya wakimbizi na namna bora ya kuboresha mazingira.

Pia Jaji Lenaola alisema kupitia mkutano huo, majaji hao watazungumzia kuhusiana na haki za wahamiaji na kuangalia namna ya kukabiliana na matatizo yanayowakabili na kuwafanya kukimbia nchi zao.

Alisisitiza kuwa kupitia mkutano huo, wataongeza ujuzi na ufanisi katika masuala ya wakimbizi na wahamiaji ndani ya Tanzania na barani Afrika kwa ujumla pamoja na kuwa na uratibu wa pamoja kuhusu namna bora za kushughulikia changamoto masuala ya wakimbizi ndani na nje ya ukanda wa Afrika Mashariki.



Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Cleophace Maharangata (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jana, wakati wa mapokezi ya magari mawili ya kuchimba visima yaliyotolewa na serikali. Wengine ni Katibu wa CCM Wilaya, Simon Leng'ese (kushoto), Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Laick Gugu (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa Halmashauri, Erasto Mhina. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mwongozo ulinzi vyanzo maji waiva Kilimanjaro

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SERIKALI mkoani Kilimanjaro, imesema mchakato wa kutengeneza mwongozo maalum wa ulinzi wa vyanzo vya maji umeiva, ambao pamoja na mambo mengine, utahakikisha kila kijiji kinawajibika kuzuia shughuli za kiuchumi kuzunguka vyanzo hivyo.

Shughuli za kiuchumi, hasa kilimo na ufugaji zinatajwa kuathiri kwa kiasi kikubwa ikolojia pamoja na vyanzo vya maji katika wilaya za Hai, Moshi, Rombo na Siha ambazo zinaizunguka Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro.

Akizungumza jana baada ya kupokea taarifa ya vyanzo vya maji vya chemchemi za Mawala na Lyakombila vilivyoko wilaya ya Moshi, Katibu Tawala wa Mkoa huo, Willy Machumu, alieleza kushangazwa kwake na serikali za vijiji kushindwa kudhibiti shughuli za kiuchumi katika vyanzo vya maji. "Kuna kibano kikali kinakuja kwa wanaovamia vyanzo vya maji na kuharibu mazingira kwa makusudi, huku wakijua kufanya hivyo ni kosa kisheria. Watanzania ni mashahidi kwamba shughuli za kiuchumi katika vyanzo vya maji, zimekuwa zikisababisha ukame mkali na maji kupungua. Ni jukumu la kila mwananchi mkoani Kilimanjaro kuhakikisha anashiriki kikamilifu kwenye shughuli za utunzaji vyanzo vya maji na hasa kuzunguka Mlima Kilimanjaro.

"Nawaomba sana wananchi na viongozi wa vijiji wa Mkoa wa Kilimanjaro, vilindeni na kuvitunza vyanzo vya maji na mazingira yanayozunguka Mlima Kilimanjaro, ambao ndio chanzo kikubwa cha maji ya chemchem yanayotumika kwa ajili ya matumizi ya binadamu, wanyama na sekta ya kilimo," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Moshi (MUWSA), Edes Mushi, akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa miundombinu ya maji yanayotokana na chemchem za Mawala na Lyakombila, alisema ujenzi wa mradi huo unaigharimu serikali zaidi ya Sh. bilioni mbili.

"Mradi huu ni mahusisi kwa ajili ya kuwahudumia wananchi kata mbili za Njiapanda na Kimochi katika Halmashauri ya Moshi, ambazo zinakabiliwa na tatizo la uhaba wa majisafi na salama kwa miongo zaisi ya mitatu sasa kutokana na uharibifu wa miundombinu ya maji," alisema Mushi.

Akizungumza katika ziara ya kukagua miradi hiyo, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya MUWSA, Stewart Nathaniel, alisema bodi hiyo imeweka mikakati ya kuhakikisha wananchi wanapata majisafi kwa asilimia 100 ikiwa ni pamoja na kuendelea kutafuta vyanzo vipya vya usambazaji maji, hususani katika eneo la Moshi Vijijini.




Ukurasa 17

**Hongera ATCL kwa kuwabwa ga Ethiopian, KQ...**



Ukurasa 16


Halmashauri yagawa ruzuku pembejeo bure kupagawisha vijana wakimbilie ajira kilimo


# BUFE

IJUMAA NOVEMBA 18, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ukurasa 18

**TAWA yakabidhiwa visiwa vilivyosheheni utajiri wa utalii ukanda wa Ziwa Nyasa**

# Kijue kikundi wabeba magunia chenye muundo kampuni, sasa mvuto wa mkoa

- Wanajijengea nyumba na kumiliki mashamba
- RC abaki hoi; msaada gerezani, sungusungu...

**Na Neema Hussein,** Mpanda



Kijana wa Trans Cargo, akiwajibika kazini. **PICHA: NEEMA HUSSEIN.**

KISWAHILI kina usemi 'Asiefanya Kazi Asile'.Pia, lugha hiyo hiyo, inabeba msamati mwingine ikihanikizwa na ujumbe kwa kauli 'mchagua jembe si mkulima' ikihitimishwa na kauli 'aibu yako ndio umasikini wako'.

Hayo ni baadhi tu ya maneno ya wahenga, waliyoyatumia sana kuhamasisha watu kufanya kazi, pasipo kubagua aina ya kazi.

Ni dhana ambayo hata mwasisi wa taifa, Mwalimu Julius Nyerere, katika nadharia aliyobuni miaka sita baada ya kupatikana uhuru wa nchi, 1967 inayoitwa 'Elimu ya Kujitegemea akisisitiza Watanzania na hasa wasomi, kutochagua kazi.

Sasa, wakati vijana wengi wakisubiri kusajiliwa na wakilalamika kuwa ajira hazipatikani, hata baadhi yao wakijitosa kwenye uhalifu kama wizi na ubakaji, zao lake ni kuona kuna jamii inayotisha.

Hapo ndiyo ziara ya Nipashe ilipoguswa kuona vijana wa mfano waliojikusanya mjini hapa, wameunda kikundi na kuchagua kazi yao, kuhudumia kupandisha na kushusha mizigo katika viwanda vya Mpanda, pia hoteli, idadi yao wapo 60 wakikipa kikundi chao kilichosajiliwa rasmi kwa jina 'Trans Cargo' wakipandisha na kushusha mazao hasa ya mchele, kwenye magari ya mizigo viwandani Mpanda.

**MLEZI NA MWASISI**

Donald Makori, ni mlezi wa kikundi anayesimulia asili yake, wamekianzisha mwaka 2014, kikiwa na vijana 30. Yeye aliona umuhimu wa kutoa elimu na kuwaunganisha wafanya kazi, kutokana na mahali anakoishi kuwepo uhalifu wa vijana uliokithiri.

Anasimulia, katika kata ya Mpanda, Mtaa wa Mpanda Hoteli, kulikuwa na sura ya chaka la wezi, vijana wengi wasiokua na kazi hivyo walitenda hayo, hata yeye binafsi akaingilia kati kunusuru hali hiyo ndani ya kata yao.

Makori anasema, mageuzi yaliyoko sasa vijana hao ndio viongozi wa kupinga wizi, maana walikaa na kuchambua 'chenga na mchele' kwa sasa waliobaki wote ni 'mchele' akiwasifu kinidhamu, hata ikitokea mtu kaibiwa, wao ndio wa kwanza kumsaidia.

Anasema hitaji kubwa kwa sasa kwa vijana hao, ni kupata mikopo kutoka serikalini kwani wanalalamika wamekuwa wakizungushwa kila wanapojitahidi kuomba mikopo hiyo.

Joyce Rashidi, ni mama mlezi wa kikundi hicho, anakisifu kimeonyesha mfano wa kuigwa katika utendaji kazi wao wa mizigo na walimpendekeza yeye kuwa mama mlezi, baada ya kuvutiwa na namna anavyowatumia vijana hao kama mfano kwa jamii ya karibu naye.

**KAULI YA WENYEKIKUNDI**

Evarist Katoto, ni mwana kikundi hicho anayerejea alikotoka kwamba, kabla ya kujiunga na kikundi hicho, alikuwa anafanya kazi ya kuanika mpunga katika viwanda, pamoja na kubeba magunia stesheni ya treni- TRC.

"Kipindi hicho tulikuwa tunafanya kazi kwa 'kusetiwa', maana tulikuwa tunajaza behewa la tani 40, tulikuwa tunalipwa kati ya Sh. 2000 na Sh.3000 kutokana na mtu aliyekupa kazi hiyo. Kama hana huruma, anakupa hiyo 2000 kama hutaki unaacha.

"Baada ya manyanyaso hayo, kuna ndugu yangu mmoja alikuwa kaishajiunga kwenye kikundi cha Trans Cargo, akanipa kama somo kuwa wanahitaji wanachama na kama niko vizuri, naweza nikatoa hela na nikajiunga.

"Kuna vitu nilikuwa navyo ndani, radio na solar' nikawa nimeviuza, ndio nikapata hela ya kujiunga hapa. Maana kiingilio kilikua ni Sh.200,000 ,"anasimulia Katoto, akiendeleza sumulizi:

"Kwanza, naishukuru sana Trans Cargo! Kulikuwa kuna watu Mpanda Hoteli (Mtaa wa Mpanda Hoteli) ni balaa! Hutembei kwa raha, ukitembea kidogo unashangaa tu ngwala, kofi umenyang'anywa simu umesachiwa umechukuliwa hela, unabaki unapiga kelele na hamna mtu atakayekuja kukusaidia! Atakayekuja kukusaidia, kazi anayo!

"Kwa hiyo, hii imetatua mabonde mengi sana, tunachoomba ni uongozi uendelee kutupa sapoti sisi kwa kufukia mabonde kama haya."

Mdau, Edesi Roman, anasimulia sasa wanapakia mchele na kushusha kwa bei ya shilingi 1000 kwa gunia moja na kupitia kazi hiyo, umoja wao umeshanunua viwanja vya kujenga makazi ya wanachama, pia wanalima mazao.

Ibelatus Nzelani, ni mwanachama mwingine, anayesimulia kwamba, kabla ya kuanzisha kikundi chao walikua na changamoto ya kubaguliwa, kwa sababu ya dai hawakuwa na nguvu za kutosha kubeba magunia hayo.

"Yaani, ilikuwa kama huna msuli wa kubeba, huwezi ukafanya kazi. Sasa hiki kikundi kimewekwa hakibagui mtu kufanya kazi na kubeba gunia.

"Mimi nilikuwa siwezi, kwa sababu nilikua mdogo, nilikuwa

**INAENDELEA UK.14**

BIASHARA

# Kijue kikundi wabeba magunia chenye muundo kampuni, sasa mvuto wa mkoa

INATOKA UK.13

bado mwanafunzi, kwa hiyo nilikuwa nikitoka shule nakuja kwenye kazi kubeba mizigo. Baada ya kumaliza elimu yangu ya kidato cha nne, niliingia rasmi kwenye hii kazi," anajieleza Nzelani.

Simon Mathayo ni mwana - kikundi, anayeeleza namna wamejiwekea malengo mbalimbali, ikiwemo kusaidiana kwenye shida na raha, binafsi akitumia mfano alivyo saidiwa:

"Mimi nilipata matatizo ya msiba. nikikosa msaada wowote sikuwa na sehemu ya kwenda kulia shida lakini vijana wenzangu hawa walinichangia hela, nikaenda msibani, hata magonjwa tunasaidiana. Nilipata ajali, pia ofisi ilinisaidia kutokana na utaratibu tuliojiwekea," anaeleza Mathayo.



Kinachoendelea hapo nacho ni sehemu ya jukumu lao. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

**KUTOKA MWENYEKITI**

Ibrahim Mzanda, ni Mwenyekiti wa kikundi cha Trans Cargo, anayesimulia zamani walipokuwa wakifanya kazi pasipo kusajiliwa, kulikuwapo ugomvi baina yao kugombania kazi.

Hapo ndio waliona umuhimu wa kusajili kikundi, ili kiwe rasmi na kujiweka kwenye utaratibu maalumu wa kazi hivyo Agosti 30, 2014 walifanikisha hilo na hadi sasa kikundi kina miaka nane tangu kuanzishwa.

Anataja malengo ya kuanzishwa, ni kuunganisha nguvu ya vijana wafanye kazi kwa bidii, wainuane kiuchumi, kuichangia kodi serikali na kusaidiana kwenye matatizo mbalimbali.

Mbali na kupakia mizigo, Mzanda anasema wanafanya shughuli za ufugaji, kilimo na wananunua mazao, mtaji wao ukitokana na kubeba mizigo.

"Kila kinachoitwa maendeleo, kwetu ndio fursa ambayo tunaikimbilia. Matarajio yetu ifikapo Desemba 2023, kikundi kiwe kinamiliki bajaji nne, Aprili 2023 pia kila mwanakikundi awe anamiliki nyumba moja, yako mengi hayo ni machache tu!" anajinasibu mwenyekiti huyo.

"Mimi niseme tu naishukuru serikali, akiwemo Rais wetu, kwani ameonyesha moyo wa kutuunga vijana kupitia zile asilimia 10 (mikopo ya vijana kupitia halmashauri zao).

"Pia, tunashukuru uongozi wetu wa mkoa, umekuwa bega kwa bega na sisi wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Katavi (Mwanamvua Mrindoko)," anasema Mzanda.

**WANASAIDIA GEREZANI**

Pia, vijana hao hujitoa katika masuala ya kusaidia jamii, ukweli akiukiri Mkuu wa Gereza la Mahabusu Mpanda. Mrakibu Mwandamizi (SSP) Moses Mbesela. anasema vijana hao wamekuwa baraka katika gereza hilo, kwa kupeleka bidhaa mbalimbali kwa wafungwa kama vile sabuni na mafuta ya kupaka.

"Mimi najivunia kuwa na vijana wa aina hii wa Kitanzania. Sio mara moja wala mara mbili wamekuwa wakiguswa na ndugu zao ambao wako magerezani na kuona wanahitaji mahitaji muhimu ya kibinadamu, kwa hiyo mimi nawashukuru sana.

"Niliwapa fursa ya kuzungumza angalau na wafungwa watatu na kuwaelezea shughuli wanazofanya nao, wakaahidi kuwa kumbe tukitoka tunaweza tukafanye kazi kama wanazofanya hawa na tukaepukane na uhalifu. Kwa hiyo, hawa wamekuwa mfano katika gereza letu kwa namna ya kipekee sana," anasema Mkuu huyo.

**POLISI JAMII YANENA**

Vitusi Jovin, ni Ofisa wa Polisi wa kata ya Mpanda, ambako kunapatikana mtaa maarufu wa Mpanda Hoteli unaosifika kwa uhalifu, anasema baada ya kuripoti kazini katika kata hiyo, alikutana na vikundi mbalimbali vya kijamii ikiwamo Trans Cargo, akawaeleza lengo lake katika kata hiyo moja ni kuhakikisha usalama wao.

"Waliniambia wako tayari kushirikiana na mimi kuhakikisha tunaondoa yale makundi ya damu chafu, Manyigu, Kaburi Moja, Wafu, ambayo ni makundi ya wahalifu. Lakini, kabla hatujaanza kuondoa yale makundi, kwanza niliwaomba wanisaidie kuongeza nguvu kazi katika kikundi chao.

"Kwa maana kwamba tutoe mianya kama kuna watu wanahitaji kujiunga wajiunge, walikubali na kusema pia wako tayari kufanya kazi kama ulinzi shirikishi, wakiona mtu anamuibia mwenziwe wanamkamata.

"Mimi kama polisi Kata naenda kumchukua, pia mtu anayevunja wako tayari kumkamata na kunitaarifu mimi. Yaani hawa vijana, ni walinzi wa wenzao!" anasema Afande Jovin.

**MKUU MKOA MRINDOKO**

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, anadokeza anavyoguswa na kikundi cha vijana hao, kwa hatua walizofikia na kutumia nguvu zao kufanya kazi ya halali.

"Ajira sio lazima ukae ofisini kuandika mafaili, ajira sio lazima serikali ije ikuambie sasa fanya hiki! Nyie mmeonyesha ubunifu, ndio kinachotakiwa kwa vijana wote wafanye hivyo," anatamka.

Anatoa maagizo kwa wakuu wa wilaya na idara za maendeleo ya jamii Katavi, kuangalia wanachofanya vijana anasema, ili kuwapatia mwelekeo chanya.

"Kundi la vijana sio la kuacha holela, hatujui wanachokifanya. Tunawaacha tu, matokeo yake wanatafuta hizo nguvu wakazitumie wapi? Ndio wanajiingiza kwenye wizi na hizo Damu Chafu na makundi mengine yasiyofaa.

"Tuanze kuwatazama vijana wetu wanapomaliza shule ya msingi, sekondari, kidato cha sita, vyuo wanakwenda wapi na wanafanya nini? Tukikuta kama wanatangatanga hawajielewi, tuwape mwongozo na huo ni wajibu wa viongozi na watumishi wote wa serikali.

"Mimi nataka nikwambie tu sisi viongozi msituone hivi tunapokea maombi mengi kweli! Yaani anaweza tu kukaa kijana ana nguvu zake kabisa, anatuma ujumbe kwa mkuu wa wilaya, mkuu wa mkoa, ofisa tarafa anasema 'leo nimeamka sina kitu nisaidie hata elfu tano ya kula!'.

"Lakini anasema hana kitu, sio kwamba ni mlemavu, labda ana matatizo fulani. Ni mzima kabisa na nguvu zake, lakini 'anabomu' (anaomba) wao wanaita' wana - tubomu' . Wakati mwingine tunapata shida mtu anakuomba elfu tano ya kula. Haya, leo ntakupa na kesho je, ukikosa si utakaba?" anahoji mkuu wa Mkoa.

Kutokana na mustakabali huo anaouanika, Mkuu wa Mkoa anajenga dira, akisema inapotokea mtu anaomba pesa kwa kiongozi, aitwe ofisini aangaliwe kama ana tatizo lolote kiafya, kimwili, kimaumbile au kingine kikwazo na likiwepo, apewe fursa ya kuwezeshwa, aachane na utegemezi.

Anatoa mbadala kwa wasio na matatizo, anaunganishwa na vikundi vya kiuchumi ndani ya jamii, kama vile vijana wa kikundi cha Trans Cargo abebe mizigo.

Mrindoko ameahidi kutoa pampu itakayowasaidia kwenye kilimo cha umwagiliaji vijana wa Trans Cargo, sambaba na ofa ya tofali 20,000 za kuchoma, kwa ajili ya nyumba wanazojenga za wanachama.

Pia, ameagiza wahudumiwe ombi lao la mikopo, wajue nini kilicho kikwazo cha vijana hao kutopata mikopo.



Kazi inaendelea, vijana wakibeba mizigo.

BIASHARA

# Hifadhi Nyerere ni mpya, jina na jiografia kubwa, inafanya mazito sokoni yabebwa na bidhaa adimu

**Na Ashton Balaigwa**

**JANA safu hii ilikuwa na simulizi ya historia, ikolojia na mazingira ya Hifadhi ya Nyerere. Lakini, je inafanyaje biashara? Endelea na undani wake:**

=

NI hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akihamasisha utalii nje ya Tanzania, hata sasa unashuhudiwa unaanza kuzaa matunda ndani ya nchi, baada ya treni iliyobeba watalii kutoka Afrika Kusini, kuwasili katika Hifadhi ya Nyerere, kuona vivutio, vikiwamo vya kihistoria.

Treni hiyo iliwasili katika Stesheni ya Fuga, ikiwa na watalii kutoka Afrika Kusini na waliambatana na wasaidizi wao kwa ajili ya kutembelea hifadhi hiyo ya Nyerere, ambayo kwa sasa ndio kubwa zaidi barani Afrika.

Mhifadhi, Charles Mpeka,anasema kufika watalii hao kumetokana na hamasa kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kutangaza vivutio mbalimbali vya nchini.

Anasema Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ina vivutio vingi vya wanyama na maziwa na inahamasisha kuangalia, akiongeza ni treni ya kwanza tangu kupungua kwa ugonjwa wa Uviko 19 ulioathiri biashara hiyo.

Kwa mujibu wa Mhifadhi Mpeka, kabla ya ugonjwa huo, Hifadhi ya Nyerere ilikuwa ikipokea watalii wengi zaidi wa ndani na nje ya nchi.

"Kwa sasa wageni wengi wanaofika katika hifadhi yetu wanaanzia Visiwa vya Zanzibar kwenye utalii wa fukwe na baadaye kuja kwetu kuangalia wanyama," anasema Mpeka, akieleza kwamba ujio wa watalii kutoka Afrika Kusini, ni kielelezo cha ongezeko lao nchini.

Pia, anataja kupokewa watalii, ni mwendelezo wa makundi ya wageni kutoka nchini Afrika Kusini, ambako wamekuwa wakivutiwa sana kwenda katika hifadhi hiyo, ili kujifunza historia mbalimbali.

### MAWAZIRI WANENA YAO

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, anafafanua kuwa mkakati wa serikali sasa ni kuhakikisha hifadhi hiyo imekuwa kivutio cha watalii wengi zaidi, kutokana na kubeba jina la muasisi wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Masanja anasema, tayari hifadhi hiyo imepata fedha kupitia Mradi wa Kusimamia na Kuendeleza Utalii Nyanda za Juu Kusini (REGROW), ikiwemo kutatua changamoto zinazoikabili hifadhi, zipate ufumbuzi.




Ofisa Uhifadhi Mwandamizi, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere (TANAPA), Seth Mihayo, akiwaeleza kuhusu hifadhi hiyo wanafunzi wa Shule ya Msingi Mloka, wilayani Rufiji Pwani, walipotembelea kama sehemu ya kumbukizi ya hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere **PICHA ZOTE: MPIGAPCHA WETU.**



Ndege ikiwa imetua na watalii ndani ya Hifadhi ya Nyerere.

Anasema tayari Benki ya Dunia imeshatoa mkopo wenye masharti nafuu Dola za Marekani milioni 150 (Sh. bilioni 340) kwa ajili ya kuboresha hifadhi nne, ambazo ni za; Nyerere, Mikumi, Udzungwa zote za Morogoro na Ruaha mkoani Iringa.

Naibu Waziri anasema fedha hizo zitatumika kuendeleza maliasili na kukuza utalii katika hifadhi na ukanda huo. Anaendelea: "Tayari mradi umeshapokea fedha kwa ajili ya ununuzi wa mitambo,vifaa, magari na vitendea kazi vingine muhimu katika kuboresha miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na shughuli nyingine za uhifadhi."

Wito wake ni kwamba, Watanzania wajitokeze kutembelea vivutio, akitoa mfano wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, yenye utalii wa michezo, kuvua samaki na Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, akizungumza wakati wa kukabidhi malori 44 kwa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), anasema serikali imeweka mkakati maalumu kwa ajili ya kuvutia watalii katika ukanda wa kusini mwa Tanzania, kupitia hifadhi za Nyerere, Mikumi ,Udzungwa na Ruaha.

Anafafanua kuwa malori hayo yaligharimu shilingi bilioni 14.77 kupitia utekelezaji wa Mradi wa Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, kwa mkopo wa masharti nafuu uliofafanuliwa.

"Kwa sasa hayo maeneo ndiyo yenye idadi kubwa ya watalii, lengo letu ni kuboresha miundombinu yake kutasaidia kuongeza watalii na mapato kwa ajili ya kuimarisha vivutio vingine vilivyopo kusini," anasema Dk. Chana.

> **Kwa sasa wageni wengi wanaofika katika hifadhi yetu wanaanzia Visiwa vya Zanzibar kwenye utalii wa fukwe na baadaye kuja kwetu kuangalia wanyama," anasema Mpeka, akieleza kwamba ujio wa watalii kutoka Afrika Kusini, ni kielelezo cha ongezeko lao nchini.**

Anasema mradi huo ulianza mwaka 2017 na changamoto hizo serikali na Benki ya Dunia walikubaliana kuongeza muda wa ukomo wa utekelezaji kutoka Desemba 2023 hadi Februari 2025, ili kufidia muda uliopotea kutokana na kuzuka janga la ugonjwa Uviko 19.

Waziri, pia anataja baadhi ya mambo utekelezaji yamekamilika, katika ununuzi wa magari ya doria, mitambo 18 ya kutengeneza barabara, usimamizi wa utalii ikolojia na huduma za magonjwa yatasaidiwa na magari hayo.

Waziri Dk. Chana anasema takwimu zinaonyesha kwamba masuala ya utalii yanachangia pato la Taifa takribani asilimia 17, pia fedha za nje takribani asilimia 25 na masuala ya utalii yanaleta ajira zisizopungua takribani milioni 1.5.

### MKUU MKOA MOROGORO

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa, anasema mkakati uliopo sasa, ni kuzilinda hifadhi; Nyerere, Mikumi na Udzungwa na kuweka sheria kwa watu watakaotupa taka ndani ya hifadhi kuchukuliwa hatua kali.

Anasema tayari mkoa umeiomba serikali kuangalia uwezekano wa kujenga barabara itakayopita nje ya hifadhi ya Mikumi, ili kuepusha wanyamapori kugongwa na magari yanayopita kwa mwendokasi, licha ya kuwepo alama mbalimbali zinazoongoza mwendo unaotakiwa.

### MAKAMU RAIS

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, anasema utalii, ni miongoni mwa sekta zinazochangia robo ya fedha zote za kigeni zinazotokana na mauzo ya bidhaa na huduma, hata kuipa picha kwamba inasaidia ukuaji wa uchumi nchini.

Dk. Mpango anasema, endapo sekta ya utalii itasimamiwa vizuri, ina uwezo wa kutoa mchango mkubwa katika ukuzaji uchumi wa nchi na kuleta maendeleo yatakiwayo kwenye vivutio vingi adimu vya duniani.

Akizungumzia mradi wa REGROW, Makamu wa Rais anabashiri utasaidia kukuza utalii kanda ya kusini kutokana na kuwepo fursa nyingi kuliko ziliozoko kanda ya Kaskazini, lakini zilikuwa hazipati nafasi ya kutangazwa.

Dk. Mpango anahitimisha kwa angalizo kuwa serikali iendelee kuboresha miundombinu yake katika sekta utalii, ikiwamo kununua ndege zaidi, kujenga viwanja vya ndege vya hifadhini, kukarabati barabara, kambi za watalii na njia za watalii kutembea kwa miguu .

Mwisho.

UCHUMI

VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA...

# Halmashauri yagawa ruzuku pembejeo bure kupagawisha vijana wakimbilie ajira kilimo

• Tija mara nne zaidi...ofisa ugani swahiba kupanda hadi mavuno

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MIAKA ya hivi karibuni serikali imekuwa ikihimiza mfumo wa elimu uhamie katika sura ya vijana kujiajiri na si kutegemea kupata kazi katika taasisi za kiserikali, kwani huko fursa ziko kwa wachache.

Hali inayoendelea sasa ni mtazamo wa kufumua mtaala uzame katika falsafa ya kujiajiri, ikizingatiwa wasomi wanaongezeka kuliko fursa za ajira.

Kuna mambo mengi ya kufanywa na vijana hata wakaondokana na umasikini. Sehemu mojawapo kunatajwa ni kuwapo asilimia 10 za mikopo ya vijana kupata mitaji ya biashara au ile ya kilimo, kupitia fedha hizo katika halmashauri mbalimbali nchini, hata kuwasadia katika kupunguza umasikini ndani ya jamii na familia kwa ujumla.

Fursa mojawapo inatajwa ni kutumia maeneo mengi yenye rutuba yanayofaa kwa kilimo. Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kupitia mapato yake ya ndani, imekuwa ikihamasisha hilo kwa kutenga fedha na kununua pembejeo, kisha wanazigawa bure, kwa vijana wenye uwezo na utayari wa kulima ekari tano au zaidi.

Matarajio hapo ni kupanuka sura na tija ya uzalishaji mazao ya chakula na biashara katika eneo hilo, lengo likiwa ni kujitosheleza kwa mazao, pia kuondoa wimbi la vijana mitaani wasio na ajira.

Baadhi ya vigezo ambavyo vijana wa Kahama wanatakiwa kuwa navyo hata wakanufaika na pembejeo hizo, ni pamoja na "kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa bidii na kuwa tayari kusimamiwa na maofisa ugani katika hatua ya kwanza ya kilimo hadi mavuno."

Sifa nyingine inatajwa ni "kuwa mpenzi wa sekta hiyo ya kilimo, kuwa tayari kujifunza kupitia maofisa kilimo waliopo katika kata zao; kuwa na eneo la kulima ukubwa wa ekari tano na zaidi; pia kuhakikisha analima mazao ya chakula na biashara."

**NENO LA WANUFAIKA**

Martha Mwandiki, ni mkulima kutoka kata ya Mwendakulima, akinena katika kipindi kilichopo cha kilimo kuanza, anasema pembejeo hizo zitawasaidia kupandisha kilimo na kuongeza tija ya sekta kilimo, kwa kupata mavuno mengi ya chakula na biashara, hata ikawakwamua na njaa.



Ofisa Kilimo wa Manispaa ya Kahama Richard Hegela, akitoa taarifa ya utoaji wa pembejeo za kilimo bure kwa wakulima vijana 71 wa kulima mazao ya chakula na biashara. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

> **Bundala anasema, kwa sasa mbolea inauzwa shilingi 140,000, lakini serikali imechukua jukumu la kulipa nusu ya fedha hizo, ili kumuwekea thamani mkulima hususani kijana, ili azalishe kwa tija.**

Anasema, awali walikuwa wanalima na kupata mazao machache, kwa sababu ya kukosa pembejeo za kukuzia na kupandia mazao, hivyo sasa katika mageuzi ameandaa shamba ekari 20 za kulima mahindi pekee yake.

Mkulima mwingine wa kata ya Bukondamoyo, Boniphace Renterenge, anasema utoaji wa pembejeo hizo kwa vijana, utasaida kupata fedha za kutosha.

Clement Masanja, mkulima kutoka eneo la Kitwana, anapongeza hatua ya halmashauri yao kugawa ruzuku hiyo muhimu ya mbolea, kwani imegusa kila kata iliyopo pembezoni mwa Manispaa ya Kahama, hata anawasihi vijana wenzake wajitoe kulima kwa tija na wajiingizie kipato zaidi.

**OFISA KILIMO**

Ofisa kilimo wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Richard Herege, anasema utoaji pembejeo za ruzuku bure kwa vijana wenye uwezo wa kulima ekari tano na zaidi, ulianza tangu katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa kutenga fedha kiasi cha shilingi milioni 54.

Anasema, mwaka huo walinunua mbolea za kupandia (NPK) kilo 139, mbegu za mahindi kilo 360 na mbegu za alizeti kilo 75 na kuwagawia wakulima vijana 27 kutoka kata 12 za pembezoni, ambao wakalima mashamba makubwa ekari 139 za mazao.

Pia, Herege anasema katika mwaka wa fedha uliofuata 2019/2020, manispaa ilitenga Sh. milioni 17.7 na kununua mbolea za kupandia kilo195, mahindi kilo 550, alizeti kilo 90 na sumu ya kuua wadudu wanaoshambulia zao la pamba chupa 90 ambazo wakazigawa kwa wakulima 39 na, zikalimwa mashamba jumla ya ekari 195.

Vilevile, Ofisa Kilimo huyo anasema, mwaka wa fedha 2020/2021, walitenga kiasi cha shilingi milioni 72 zilizotumika kwenye ruzuku za pembejeo za shilingi milioni 24, ambazo ni: Mbegu za mahindi kilo 785, alizeti kilo 45, dawa za pamba chupa 20, mbolea za kukuzia na kupandia mifuko 225 na mbegu za mtama kilo 1,500 na kila mwaka vijana wamekuwa wakijitokeza kwa wingi zaidi kuzihitaji.

Herege anasema, tangu wameanza kutoa pembejeo hizo jumla ya wakulima vijana 172 wamenufaika na kiasi cha Sh. milioni 115.7 kimeshatumika.

Anasema, mwaka uliopo wa fedha wameshatoa mbolea mifuko 680, mbegu za mahindi kilo 1,500, mbegu za alizeti kilo 300 pamoja na lita 225 za viuatilifu kwa wakulima vijana 71 kati ya wakulima 312 walioomba kutoka kata 12.

Huku akieleza kuwa vyote hivyo walivitoa mwaka huu vina thamani ya shilingi milioni 66.8, anasema vitatumika kuhudumia mashamba ekari 415 za mahindi, mpunga, alizeti na pamba.

Anasema, katika mpango huo hadi kufikia sasa, mafanikio yameanza kuonekana, kwani kabla ya kufadhiliwa, pembejeo hizo walikuwa wakipata magunia manne ya mahindi kwa ekari moja tofauti na sasa wanapata wastani wa magunia 25 ekari moja.

Vilevile Herege anasema, zao la mpunga walikuwa wakipata wastani magunia matano kwa ekari moja. Lakini sasa wanapata magunia 25; alizeti imepanda kutoka magunia nne hadi 12 kwa ekari; hali kadhalika pamba ni kutoka kilo 200 hadi 800 kwa ekari moja.

Hata hivyo, anasema eneo ambalo halijafikiwa hadi sasa, bajeti inayokidhi mahitaji hayo bado iko chini, vilevile namna ya kuwafikia vijana wengi na hamasa ya kupata tija wakijiunga kwenye vikundi vya uzalishaji mali.

**MEYA WA MANISPAA**

Yahaya Bundala, ni Meya wa Manispaa ya Kahama, anayewaasa wakulima hao vijana kutumia pembejeo hizo za ruzuku kwa ajili ya kilimo chenye tija.

Bundala anasema, kwa sasa mbolea inauzwa shilingi 140,000, lakini serikali imechukua jukumu la kulipa nusu ya fedha hizo, ili kumuwekea thamani mkulima hususani kijana, ili azalishe kwa tija.

Anasema kabla ya manispaa kutoa ruzuku hizo ilikuwa ikiwawia vigumu kwao uongozi kuingia kilimo, kutokana na changamoto ya kupanda bei za mbolea, hali inayowakatisha tamaa kujikita kwenye kilimo.

Pia anawataka wakulima kuacha tabia ya kuuza pembejeo hizo na kutumia fedha katika anasa kama vile ulevi, badala yake wajikite katika kilimo chenye tija, nidhamu na kujiongezea kipato.


.



Mwenyekiti wa Manispaa ya Kahama Yahaya Bundala, (kushoto) akimkabidhi viuatilifu vya mazao, mkulima Martha

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Hongera ATCL kwa kuwabwaga Ethiopian, KQ...






**NA JOSEPH KULANGWA**
+255 713 410008
kulangwasos@gmail.com

DUNIANI kote kwenye familia huwa kuna taratibu za kukubaliana au kujitakia, pia zipo zinazojitokeza kutokana na hisia tu. Mathalan, zipo za kuchukiana au hata kupendana na kupendeleana.

Hizo ni tabia za kawaida kabisa, utaweza kushuhudia wazazi wanapenda, kuchukia au kupendelea baadhi ya watoto na hata kama ni wawili, basi anaweza kupendwa au kupendelewa mmoja na mwingine akachukiwa tu.

Na hiyo pengine hutokea bila kujitambua na huendelea hivyo, mpaka watoto kujihisi kuwa yawezekana kuwapo tatizo linalofanya kupendwa, kuchukiwa au kupendelewa.

Mara nyingi, hususan katika familia za Kiafrika, watoto wenye uwezo kiuchumi hupewa kipaumbele katika masuala mbalimbali yakiwamo ya uamuzi katika mwelekeo wa familia, hata kama kiumri ni wadogo au mdogo.

Tabia hiyo imekuwa ikienda mbali, ikivuka mipaka ya kifamilia mpaka kiukoo au hata kijamii na hata katika makundi ya kampuni, mashirika au jumuiya yoyote.

Hiyo huwa ni sehemu ya maisha na huzoeleka, bila kusahau kuwapo maslahi chanya ndani yake, ambayo kwa wasiopendelewa kwa kuwa na maslahi hasi na wakati mwingine, kusababisha malalamiko.

Ukienda katika michezo, suala la upendeleo huwa lipo tena wazi kabisa na mpaka wengine kuita mbeleko, kwamba mathalan kwenye soka timu moja hubebwa na waamuzi au hata viongozi wa mchezo husika.

Nilibaini na kuthibitisha tabia au mwenendo huu, hasa katika mchezo wa masumbwi ambao hivi ssa unashamiri nchini, achezapo Mtanzania na mgeni, kama asipopatikana mshindi wa 'Knock Out' (KO) au 'Technical Knock Out' (TKO), basi mshindi atakuwa Mtanzania.

KO ni pale mshindwa anapopigwa na kuanguka chini akahesabiwa na kushindwa kuinuka au akainuka, lakini akashindwa kuendelea kutokana na mawenge na TKO, ni pale inapotokea mshindwa amepigwa akaumia na kushindwa kuendelea au akajitoa.

Nikasikia siku moja wadau wa ndondi wakisema kwamba, anapokuja mchezaji mgeni nchini, asipompiga mpinzani wake ambaye ni Mtanzania kwa KO au TKO, basi ajue ameula wa chuya, lazima mwenyeji atapewa ushindi.

Nilipata kuthibitisha hilo kwa kutazama jinsi siku moja Mtanzania anavyoteseka ulingoni, lakini akaja kutangazwa mshindi na majaji kwa kuwa tu mpinzani wake mgeni hakumshinda kwa KO au TKO.

Hii kwangu mimi huona kama ni aibu, pia nahisi hali ya kudekezana na kujiua kimichezo, kwamba mshindi bandia huyu anajiamini kashinda, lakini kumbe kabebwa tu na akiendelea hivyo, kuna siku hatashinda kabisa akitarajia kubebwa.

Tabia kama hii ikiendelea, binafsi nahisi itasababisha nchi kupoteza sifa ya kuwa na washindanaji wazuri na kupigwa chapa ya Taifa linalotegemea majaji au waamuzi kulibeba katika mashindano na hivyo kuonesha taswira mbovu.

Awali nilitarajia kuwa mbeleko hii huonekana kwenye michezo tu, kumbe sasa imevuka mipaka na kuingia katika mashindano mengine makini yanayoweza kuipa nchi sifa nzuri au mbaya katika medani za ushindani kibiashara.

Hivi karibuni tulishuhudia mashindano ya 'Mlaji' yakiitwa kwa Kiingereza 'Consumer Choice Awards Africa 2022', yakifanyika jijini Dar es Salaam, kwa kushirikisha makundi mbalimbali yaliyoshiriki kupigiwa kura na kupatikana washindi.

Katika kundi la Kampuni za Huduma ya Usafiri wa Anga, washindani walikuwa ni mashirika ya ndege ya Tanzania, Ethiopia, Kenya, Afrika Kusini, Misri, Shelisheli, Mauritius, Rwanda na Shirika lisilo maarufu linalojulikana kama Air Peace.

Mshindi katika kundi hilo, akaibuka Air Tanzania, shirika letu pendwa, kwa kweli nilishangilia kwa mshituko, kuona mshindi ni mwanetu, kaibuka mshindi wa Bara la Afrika na kutangazwa kuwa alipata asilimia 66.

Alipoitwa Ofisa Mtendaji Mkuu, Ladislaus Matindi kupokea tuzo yake akasema: "Niseme nini, hii ni changamoto katika safari yetu ambayo sijui mwisho ni wapi...ni safari ngumu lakini hatutakuangusheni, tunaweza kuwa kama Ethiopian Airlines siku moja."

Nikatafakari hivi inakuwaje mathalan kwenye soka, Ihefu itangazwe bingwa, lakini kiongozi wake apande jukwaani afurahie ushindi huo wa kutangazwa, lakini baadaye aseme siku moja tutakuwa kama Simba au Yanga?

Mpaka sasa sijaelewa ni vigezo vipi vilivyofanya ATCL kuzishinda Ethiopian Airlines, Kenya Airlines, Egypt Air, South Africa Airlines, Rwanda Air na midude mingine mikubwa katika huduma hiyo ya safari za anga! Kama nilielewa vibaya, basi nafuta yote hayo juu! Alamsiki!

BIASHARA

# TAWA yakabidhiwa visiwa vilivyosheheni utajiri wa utalii ukanda wa Ziwa Nyasa

**Na Gideon Mwakanosya – Nyasa**



Kisiwa cha Lundo, ambacho tayari TAWA imeshaanza kuwekeza. **PICHA ZOTE: GIDEON MWAKANOSYA**

SERIKALI mkoani Ruvuma, kwa kutambua umuhimu wa uhifadhi imewakabidhi Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) hati ya kukabidhiwa visiwa vya Lundo, Mbambabay na milima ya Mbamba na Tumbi, yenye jumla ya ekari 597 kwa ajili ya uhifadhi.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, amekabidhi hati ya kumilikishwa eneo hilo, pia amezindua uwekezaji wanyamapori katika kisiwa cha Lundo, ambacho tayari wamewekwa wanyamapori jamii ya swala na ndege.

Kanali Laban amesisitiza kuwa, kupelekwa kwa wanyama katika kisiwa hicho, maana yake kutasaidia kuongeza vivutio kwa watalii kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii vinavyopatikana katika wilaya ya Nyasa na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla.

Mkuu wa Mkoa, pia amewaagiza wadau wa utalii na uhifadhi wakiwemo TAWA na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kuchukua jukumu la kutoa elimu ya uhifadhi na utalii kwa wananchi hasa wa mkoa wa Ruvuma, kuhusu umuhimu wa sekta ya utalii katika kuchochea uchumi, sanjari na kufungua vituo vya utoaji taarifa za utalii katika kila Halmashauri.

**HISTORIA YAKE**

Akizungumzia historia ya kivutio hicho cha utalii, kisiwa cha Lundo chenye ukubwa za hekta 20, Mganga Mkuu Mstaafu wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Dk.John Paparika, ambaye pia wazazi wake wametokea katika kisiwa hicho, anasema kimepewa jina la Lundo, kwa sababu watu wa kwanza waliovuka kisiwa hicho kwenda ng'ambo ya pili walifikia kijiji cha Lundo.

Anasema, kisiwa hicho tangu zamani kilikuwa na manufaa makubwa kwa wananchi wa vijiji vya Lundo, Ngindo na Chinula kwa sababu wakati wa vita ya majimaji iliyotokea kati ya mwaka 1905 hadi 1907, watu walikuwa wanakimbilia kisiwani humo kwa ajili ya kujificha.

"Baada ya vita ya Majimaji kuanzia mwaka 1908, kisiwa hiki kilitumika na wakoloni wa kijerumani kuwahifadhi watu waliopata ulemavu kutokana na ugonjwa wa ukoma ambao baadaye walihamishiwa katika kisiwa cha Puulu,"anasimulia Dk.Paparika.

Hata hivyo, anasema watu hao wenye ukoma walipandiwa matunda ya aina mbalimbali katika kisiwa hicho yakiwemo maembe, mapera, mananasi, machungwa na migomba ambayo hadi sasa kisiwani humo kuna masalia yake, hali kadhalika makaburi yao. Anasema licha ya watu hao wenye ukoma kutengwa katika kisiwa hicho, bado ndugu zao kila wiki walikuwa wanafika katika kisiwa hicho kuwatembelea na kuwaletea vyakula, kwa sababu ulemavu waliopata, walikuwa hawawezi kufanya kazi hivyo walihitaji msaada.

> **"Milima na visiwa hivi vimejaliwa kuwa na uoto mzuri wa miombo, mawe yanayozunguka visiwa hivi na milima kando kando ya ziwa yana hifadhi samaki adimu wa mapambo zaidi ya aina 400",anasisitiza Challe.**

Historia ya kisiwa hicho, inaonyesha kwamba kilisaidia wakati wa mgogoro wa kutoelewana baina ya kabila la Wamatengo wa wilaya ya Mbinga na Wanyasa wa Mwambao mwa Ziwa Nyasa.

Inaelezwa Wamatengo walipokuwa wanashuka na silaha zao wakazi wa kata za Lundo na Mbambabay, walikuwa wanakimbilia kujificha katika kisiwa hicho.

"Kwa kuwa Wamatengo hawana uwezo wa kuogelea wala kuendesha mitumbwi, walikuwa wanashindwa kuwapata wanyasa ambao walikuwa wanapiga kasia na kujificha katika kisiwa cha Lundo," anasimulia' Dk.Paparika.

**UTAJIRI ULIOPO**

Anaeleza, kisiwa hicho kina utajiri wa aina mbalimbali za samaki wa mapambo ambao wanapenda kuishi sehemu za mawe. Inakadiriwa samaki mmoja wa mapambo katika nchi za Ufaransa, Ujerumani na Afrika ya Kusini anauzwa kati ya dola za Marekani 400 hadi 500 sawa na zaidi ya shilingi milioni moja.

Mshauri wa Maliasili na Utalii Mkoa wa Ruvuma Afrikanus Challe anasema hifadhi ya Mbambabay ina ukubwa wa eneo la hekta 597 na kwamba maeneo hayo yanafaa kwa kufuga wanyamapori na ndege.

Hata hivyo, anasema kati ya hekta hizo, mlima Mbamba una eneo ukubwa wa hekta 40, Mlima Tumbi hekta 110, kisiwa Mbambabay kina hekta 27, kisiwa cha Lundo kina ukubwa wa hekta 20.

"Milima na visiwa hivi vimejaliwa kuwa na uoto mzuri wa miombo, mawe yanayozunguka visiwa hivi na milima kando kando ya ziwa yana hifadhi samaki adimu wa mapambo zaidi ya aina 400",anasisitiza Challe.

Kwa mujibu wa Challe, eneo la hifadhi ya Mbambabay ni muhimu sana kwa upande wa Tanzania hususan katika matumizi ya shughuli za utalii kama vile utalii wa kuvua samaki, kupiga mbizi, utalii wa kuendesha mitumbwi na kuweka kambi kwenye fukwe.

Mtaalamu huyo wa uhifadhi, anasema eneo hilo likihifadhiwa litatumika kwa ajili ya mazalia ya samaki na hivyo kuongeza kipato kwa wananchi wanaotegemea shughuli za uvuvi.

"Mbambabay ikihifadhiwa inaweza kuleta ushindani kibiashara kwa sababu katika nchi yetu hakuna eneo linaloweza kutoa mchanganyiko mzuri wa huduma za kitalii kama zitakazotolewa katika eneo hili," anasisitiza Challe.

Wilaya ya Nyasa inaongoza katika Mkoa wa Ruvuma kwa kuwa na vivutio vya aina mbalimbali vya utalii.

Kwa upande wake Mkurugenzi mtendaji wa Halmshauri ya Wilaya ya Nyasa, Jimson Mhagama, anaiambia Nipashe kuwa maeneo ya mwambao mwa Ziwa Nyasa yako vizuri na yana fursa nyingi kwa wawekezaji wa sekta ya utalii, hivyo anawahimiza kuona umuhimu wa kufika nyasa kuwekeza kwa kujenga hoteli za kitalii kwenye maeneo hayo, kwani kwa sasa kuna miundombinu bora, barabara ya kiwango cha lami kutoka Songea mjini hadi Mbambabay



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, akimkabidhi rasmi Kamishna Mwandamizi wa TAWA Kanda ya Kusini Mashariki, Abrah Juuru, hati ya umiliki wa Hifadhi ya Mbambabay inayojumuisha visiwa viwili na sehemu ya Ziwa Nyasa, katika hafla iliyofanyika Mbambabay wilayani Nyasa.

**RIPOTI MAALUM**

# Ushuhuda wa wanakijiji tope la mgodi lilivyovamia makazi

## •NEMC na Mkemia Mkuu wa Serikali watoa tamko
## •Wadau mazingira wataka chombo huru kuchunguza

**Na Marco Maduhu, aliyekuwa**
KISHAPU

ILIKUWA majira ya saa nne asubuhi, Jumatatu ya wiki iliyopita, wakazi wa vijiji vinavyozunguka Mgodi wa Almasi Mwadui wakiwa majumbani mwao, waliposhuhudia tope likivamia kwenye makazi yao.

Hao ni wakazi wa vijiji viwili vya Ng'wanholo na Nyeze, Kata ya Mwadui Luhumbo wilayani Kishapu wanaoishi jirani na mgodi huo ambao bwawa lake la kuhifadhi maji machafu limebomoka na kusababisha mtafaruku uliogeuka ajenda ya kitaifa.



Wananchi wa vijiji vya Ng'wang'olo na Nyenze Kata ya Mwadui Luhumbo, wilayani Kishapu wakiangalia tope lililovamia makazi yao na kufunika mashamba na visima. **PICHA: MARCO MADUHU**

Wanakijiji hao wanawasilisha kilichojiri kwamba walipigwa na butwaa walipoona tope linazingira nyumba zao na kufunika visima vya maji na mashamba, na katika kujiokoa, walilazimika kuyakimbia makazi yao.

Tungu Kwinyalija, mkazi wa Nyenze, anasimulia kilichojiri, akitamka: "Siku ya tukio nilikuwa nyumbani na familia yangu, ghafla niliona tope likiyavamia makazi yetu mithili ya mvua ya mafuriko, uamuzi wa haraka tuliouchukua ni kutimua mbio na watoto wangu kwenda sehemu salama.

"Vitu vyote ambavyo vilikuwa ndani tuliviacha kwa sababu ilikuwa ni ghafla, na nyumba yetu ikazingirwa na tope zito pamoja na shamba langu lenye ekari nane nalo limefunikwa na tope."

Ni hasara inayopata ushuhuda zaidi kutoka kwa Mahona Rufufu, mkazi wa Kijiji cha Ng'wanholo, anayesema familia yake yenye watoto watatu imepoteza kila kitu, yakiwamo mashamba yake yenye ukubwa wa ekari 20 yaliyofunikwa na tope na hawana eneo lingine la kufanya shughuli za kilimo.

Mkazi mwingine wa kijiji hicho, Meya Ndolwe pia anasema amepoteza makazi na mbuzi wake wawili na sasa anajiona kurejea kwenye umaskini, akiomba serikali iwasaidie ili kupata haki zao kutokana na kuathiriwa na tope la Mgodi wa Mwadui.

Mwanakijiji mwingine Mbuke Jilala anasema licha ya majibu kutoka vyombo vya uchunguzi wa kemikali serikalini kudai tope hilo halina madhara, hawana imani tena na maeneo hayo yaliyofunikwa tope la mgodi huo, akiomba ufanyike uchunguzi wa kina ili wasije kupata madhara baadaye.

**HATUA SERIKALINI**

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Manai, Kijiji cha Ngw'anholo Ester Seni, anasema: "Ni jambo la kumshukuru Mungu bwawa limebomoka mchana, lingebomoka majira ya usiku lingeleta madhara makubwa kwa wananchi vikiwamo vifo.

"Huu ni msimu wa kilimo na mashamba mengi ya wananchi yamefunikwa na tope hakuna tena kulima, sijui itakuwaje, maana sisi wananchi wa vijijini maisha yetu tunayaendesha kwa kilimo. Tunaomba serikali iliangalie suala hili ili tusije kufa kwa njaa kutokana na ukosefu wa chakula."

Francis Manyanda, Diwani wa Mwadui Luhumbo, Francis Manyanda anasema wameshtushwa na tukio hilo la tope la bwawa la mgodi kuvamia makazi ya wananchi huku Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo akiutaka mgodi na serikali kufanya tathmini na kuwalipa fidia wananchi ambao makazi, visima na mashamba yao yamefunikwa na tope hilo.

"Visima vya maji ambavyo walikuwa wanavitumia wananchi hawa vimefukiwa na tope na sidhani hata kama tope likiondolewa kutakuwa na usalama, hivyo ninaomba wananchi wakirudi kwenye makazi yao kama zamani watekelezewe miradi ya maji safi na salama ya bombani.

"Pia huu ni msimu wa kilimo na mashamba mengi ya wananchi yamefunikwa na tope, hili nalo liangaliwe kwa mapana kwa sababu wananchi hawatapata mavuno, fidia iangaliwe kwa hali ya juu ili wananchi wasiishie kuumia na kuanza kulia njaa," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema anasema taarifa aliyoletewa na kamati yake aliyoiunda kuchunguza tukio la bwawa hilo, inabainisha bwawa lilianza kutumika kujazwa maji machafu tangu mwaka 2002, yaani miaka 20 iliyopita.

Anasema tathmini ya awali iliyofanywa na kamati yake, imebaini nyumba 13 zimezingirwa na tope. Wakazi wake 115 sasa wanaishi kwa muda ndani ya Mgodi wa Mwadui wakati taratibu zingine za kisheria zikifuatwa ikiwamo kulipwa fidia.

"Wananchi 115 wameathiriwa na tope kutoka bwawa la Mgodi wa Almasi Mwadui lililobomoka, tunamshukuru Mungu hakuna kifo hata kimoja," anasema Spohia.

Meneja Mkuu wa Mgodi wa Almasi Mwadui, Ayubu Mwenda anasema kuwa baada ya kutokea kwa tukio hilo, uamuzi wa kwanza wa mgodi ulikuwa kujali usalama wa wananchi na ndiyo sababu wamewachukua wananchi wote 115 ambao wameathiriwa na tope hilo na wanaishi nao kwa muda ndani ya mgodi huku wakiwatimizia mahitaji yao, ikiwamo watoto wao kupelekwa shuleni.

"Tumesitisha pia shughuli za uzalishaji wa almasi hadi pale tutakapomaliza kujenga bwawa lingine jipya, kikubwa hapa tunajali usalama wa wananchi kwanza," anasema Mwenda na kubainisha tathimini inaendelea kufanyika ili kuwalipa fidia huku wakiangalia namna ya kutoa tope kwenye mashamba yao na ikishindikana itabidi watafutiwe mashamba mengine.

Vilevile, Meneja Mkuu huyo anadai tope hilo halina madhara kwa binadamu, akizama katika utetezi kwamba uzalishaji wa almasi ni tofauti na dhahabu, ambao wenyewe hutumia kemikali hatarishi kwa afya na mazingira.

**JICHO LA NEMC**

Meneja wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Ziwa, Kayombo Jarome anasema kuna uharibifu mkubwa wa mazingira uliosababishwa na tope hilo, licha ya kuunga mkono hoja ya Mwenda kwamba tope hilo halina sumu.

Katika hilo la hofu ya kemikali hatarishi, Jarome ana ufafanuzi kwamba kemikali ambazo mgodi huzitumia katika shughuli za uzalishaji wa madini ya almasi hazina madhara kwa binadamu, akizitaja kuwa ni silcon, iron na frogrant.

Mkurugenzi Mkuu NEMC, Dk. Samweli Gwamaka anasema sampuli za tope ambazo walizipeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali zinaonesha tope hilo halina madhara kwa binadamu na viumbe hai wengine.

"Hata hivyo, kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira, mgodi utalazimika kulipa fidia wananchi pamoja na kurekebisha miundombinu yote zikiwamo nyumba za waathirika, visima vya maji na mashamba," anaagiza Dk. Gwamaka.

**KAULI YA MKEMIA**

Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Ziwa (Mwanza), Mussa Kazumila anasema uchunguzi wa maabara yao baada ya kuchukua sampuli za tope hilo, umebaini tope halina kemikali hatarishi, hivyo wananchi wasiwe na hofu juu ya afya zao.

"Tulianza upimaji wa sampuli za tope hili la mgodi tarehe 9 Novemba mwaka huu na tukio lilitokea tarehe 7 Novemba mwaka huu. Majibu ambayo tumepata kutoka katika maabara zetu, tope halina kemikali hatarishi ya aina yoyote ile", anasema Kazumila.

**WAZIRI: NI UZEMBE**

Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko anasema kupasuka kwa kingo za bwawa hilo ni uzembe mkubwa ambao umefanywa na mgodi kwa kuwa Septemba mwaka huu lilianza kuonesha dalili za kubomoka lakini wakaendelea kulitumia.

"Taarifa nilizonazo juu ya bwawa hili, lilianza kupata hitilafu tangu mwezi wa tisa (Septemba), lakini ninyi mkapuuza na kuendelea kulitumia na sasa limeleta madhara kwa wananchi. Huu ni uzembe wa hali ya juu," alisema Dk. Biteko alipozuru mgodini, pia kutembea maeneo yaliyoathirika wiki iliyopita.

Alibainisha kuwa kisheria mabwawa hayo yanapaswa kuwa yanafanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara, ili kudhibiti maji yasije yakaingia kwenye makazi ya wananchi na kuleta athari.

"Tushukuru migodi ya almasi huwa haitumii kemikali zenye madhara kwa binadamu, hapa ungekuwa mgodi wa dhahabu ndiyo bwawa lake limepasuka, tungekuwa tunazungumza mengine," alisema Biteko.

Alisema kuwa kwa kuzingatia uzembe ambao umefanywa na mgodi huo, lazima wapewe adhabu kali ili liwe fundisho kwa migodi mingine ili janga kama hilo lisitokea tena na kuhatarisha maisha ya wananchi.

Mhandisi Mkuu wa Mgodi wa Mwadui, Shagembe Mipawa anakiri bwawa hilo kupata hitilafu Septemba mwaka huu, akidai walikuwa wameshaanza kuziba mianya ambayo ilikuwa ikivuja na wakijiridhisha lipo salama, lakini wakashaghaa Novemba 7 likabomoka kingo kisha tope kuvamia makazi ya wanakijiji.

**CHOMBO HURU**

Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT) hakiko mbali katika kufuatilia kinachojiri mgodini Mwadui, kikisema kilichotokea katika Mgodi wa Almasi Mwadui "kiamshe serikali kuwajibika na kufuata Sheria ya Utunzaji wa Mazingira ya Mwaka 2004 na viwango vya kimataifa vya usimamizi wa mabwawa yenye sumu".

Ofisa Miradi wa LEAT, Clay Mwaifani anasema serikali inapaswa kuunda bodi huru ya mapitio ya mabwawa yote ya taka sumu kwa kufuata viwango vya kimataifa vya usimamizi wa mabwawa hayo, ambayo itakuwa ikiyakagua mara kwa mara ili kuona uimara wake na yasilete madhara kwa wananchi.

"Tatizo la kupasuka bwawa la taka sumu lilitokea pia mwaka 2019 huko Brazil kwenye mgodi wa uchimbaji madini, ambapo watu 270 walipoteza maisha, hivyo serikali inapaswa kuwajibika pamoja na kuwa na bodi huru ya mapitio ya mabwawa ya taka sumu kwenye migodi ili isije ikajitokeza kwenye migodi mingine," anashauri.

Mwaifani pia anasema LEAT haiungi mkono majibu ambayo yametolewa kuwa tope la mgodi huo halina sumu, akisisitiza kuundwe tume huru ya kuchunguza zaidi ili baadaye kusije kutokea madhara kwa wananchi.

"Sisi kama timu ya wanasheria na watetezi wa mazingira kwa vitendo, hatukubaliani na majibu ambayo yametolewa na NEMC, Tume ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga na Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa tope la mgodi halina sumu, wasitoe majibu mapesi, bali iundwe tume huru ya kuchunguza," anasema.

Ofisa huyo wa LEAT pia anasema mgodi unapaswa kuwajibika kwa wananchi, kwa kufuata viwango vya kimataifa kwa kuweka hatua za dharura na muda mrefu namna ya kuwahudumia wananchi ambao wameathiriwa na tope hilo badala ya kuishia kuwapatia msaada wa chakula tu na malazi kwenye kambi za mgodi, bali uwajibike zaidi kunusuru hali zao kijamii na kiuchumi.

Mgodi wa Almasi Mwadui (Williamson Diamond Ltd) ulianzishwa mwaka 1940 baada kugunduliwa na Dk. John Williamson, Gwiji wa Jiolojia na raia wa Canada.

# Benki TCB yaingiza bil.100/- za serikali kupitia tawi la TPA

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara Tanzania (TCB) imezindua rasmi tawi la TPA lililoko makao makuu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) linalofanya kazi saa 24 kila siku ili kusaidia kufanikisha shughuli za uchukuzi bandarini.

Akizungumza kwenye hafla ya uzinduzi wake uliofanyika juzi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Sabasaba Moshingi, alisema tawi hilo linaendeshwa na lipo kimkakati.

Moshingi alibainisha kuwa pamoja na kutoa huduma zingine za kibenki, Tawi la TPA ni mahususi kwa ajili ya kusaidia kukusanya malipo ya serikali zikiwamo kodi na tozo mbalimbali. Pia alisema tawi hilo limekuwa ni uwekezaji wa thamani unaolipa vizuri na ambao umekuwa na ufanisi mkubwa kibiashara.

Tangu kufunguliwa kwake takribani miaka miwili iliyopita, alisema Tawi la TPA limeiwezesha Benki ya TCB kusaidia kukusanya mapato ya serikali yenye thamani ya Sh. bilioni 100.

Kwa mujibu wa Moshingi, kiasi hicho kinatokana na makusanyo ya fedha za Kitanzania Sh. bilioni 57 na yale ya fedha za kigeni ni kama Sh. bilioni 42 kwa viwango vya kubadilisha fedha vya sasa.

"Tawi la TPA ni moja ya matawi yetu mawili ambayo yanafanya kazi saa 24 kila siku. Lipo kimkakati kusaidia kukusanya malipo mbalimbali ya serikali katika Bandari ya Dar es Salaam," alisema Moshingi.

Tawi jingine la TCB linalokuwa wazi masaa 24 liko kwenye Uwanja wa Ndege Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Dar es Salaam.

Akielezea utendaji kazi wa tawi hilo kabla ya kuzinduliwa rasmi, Meneja wa Tawi la TCB la TPA, Anastela Kabudi, alisema makusanyo ya mwezi ni kati ya Sh. bilioni 1.5 na Sh. bilioni tatu.

Kuhusu fedha za kigeni, Kabudi alisema wanakusanya wastani wa zaidi ya dola 500,000.

Moshingi alisema kimsingi lengo la mkakati wa uendeshaji wa saa 24 kwa siku kuwahudumia vyema wateja wa TCB wanaoitumia Bandari ya Dar es Salaam na kuwawezesha kufanya malipo ya serikali kwa urahisi wakati wowote.

Aliwachagiza watumiaji wengine wa bandari hiyo ambayo ndiyo kubwa kuliko zote nchini na kitovu cha shughuli za uchukuzi majini kuanza kulitumia tawi hilo kikamilifu.

Pia alisema Tawi la TPA linawapa nafasi ya kuhudumiwa na taasisi kongwe ya fedha kuliko zote nchini na ni fursa kwao kuweza kuzitumia suluhisho bora na za kisasa za benki hiyo.

Kwa sasa, TCB ambayo dira yake inaelekeza iwe benki kiongozi ya huduma rahisi za kifedha na kinara wa huduma jumuishi, ina matawi 82 nchi nzima yanayosaidiwa na zaidi ya mawakala 3,000, ATM 84 inazozimiliki pamoja na zile 350 za mtandao wa Umoja Switch.




Mkurugenzi wa Wateja Wakubwa wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), James Meitaron (kushoto) na Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji na Uwekezaji (UNCDF), Peter Malika, wakibadilishana mkataba jijini Dar es Salam juzi, baada ya taasisi hizo kutiliana saini makubaliano ya kuanzishwa kwa hati fungani za kukusanya fedha kwa ajili ya kuboresha mfumo wa maji katika Jiji la Tanga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Shemdoe ataka watumishi wa halmashauri kuwajibika

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe, amewataka watumishi wa halmashauri kuwajibika katika nafasi zao ikiwamo kusimamia miradi ya maendeleo.

Prof. Shemdoe aliyasema hayo jana alipofanya ziara ya siku moja katika Halmashauri ya Chalinze na kuzungumza na watumishi na kutembelea miradi ya maendeleo ikiwamo soko na ujenzi wa vyumba vya madarasa na Hospitali ya Msoga

Alisema ni vyema wasimamizi wa miradi wakasimamia kwa uadilifu fedha za miradi ya maendeleo ili zitumike kama zilivyolengwa na kuondoa vikwazo kwa wananchi.

Shemdoe aliwataka wakuu wa idara kujenga tabia ya upendo na kushirikiana na kusikiliza wananchi wanaowatembelea kwenye ofisi zao kwa kutatua kero zinazowakabili.

"Wakuu wa idara wekeni utaratibu wa kuwa na vikao vya mara kwa mara. Vikao hivi vitumike kutoa taarifa za maendeleo ya miradi na kushauriana nini kifanyike kwa kushirikiana," alisisitiza.

Akiwa katika Shule ya Sekondari Lugoba, Prof. Shemdoe alipongeza uongozi wa shule kwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa ambavyo vimefika hatua ya umaliziaji tofauti na ilivyo katika maeneo mengine.

"Jengo hili lipigwe picha nitaliweka kwenye website yangu ni la mfano. Uongozi wa halmashauri, shule na kata umeonyesha uwajibikaji kwa vitendo. Hatua hii inatia moyo kwenye utumiaji wa fedha zinazotolewa na serikali. Hapa hakuna mwanafunzi atakayechaguliwa kuja Lugoba na akose nafasi," alisema.

Akikagua ujenzi wa vibanda vya wajasiriamali vinavyojengwa kuzunguka soko la Bwilingu, Prof. Shemdoe alisema mradi huo ukikamilika wapewe wananchi na si viongozi.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Ramadhan Possi, alisema halmashauri imepokea Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule za sekondari ili kuwezesha watakaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wapate nafasi.

# Wahimizwa kilimo misitu kukabili tabianchi

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Charles Meshack, amewataka wadau wa misitu kujikita katika upandaji miti na kilimo cha misitu ili kurejesha uoto wa misitu katika maeneo ambayo imetoweka kutokana na shughuli za kibinadamu.

Meshack ambaye ni Mlezi wa Mtandao wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii Tanzania (MJUMITA) alisema hayo jana kwenye Mkutano Mkuu wa 22 wa MJUMITA uliofanyika mjini hapo.

Alisema upandaji misitu hai ni kitendo cha kuacha eneo lililokosa msitu bila kufanya shughuli yoyote ya kibinadamu na msitu unarejea kwa kukua kwenye hali yake ya kawaida baada ya miaka kadhaa.

Kwa mujibu wa Mweshack, jamii haina budi kuhakikisha ndani ya mashamba yao kuna angalau mti mmoja ili kujinusuru na masuala ya ukame na kutoweka kwa misitu kunakosababisha mabadiliko ya tabianchi na kuleta ukosefu wa maji katika maeneo mbalimbali nchini.

"Sasa maji ni ya mgawo katika maeneo mengi Dar es Salaam. Kenya ng'ombe na wanyamapori wanakufa, wenzetu huko wanakunywa maji wanayokunywa ng'ombe, hivyo tubadilike. Ukiona mwenzio ananyolewa wewe tia maji. Mabadiliko ya tabianchi yatatuadhibu kama hatutabadilika, itakuwa ni kifo kwetu," alisema Meshack.

Mkurugenzi huyo aliitaka MJUMITA kujipanga kurejesha uoto wa asili kwenye vijiji vilivyoko katika maeneo yao kwa kuondoa migogoro ya ushindani wa ardhi baina yao, wakulima na wafugaji.

Hata hivyo, aliagiza wavunaji misitu kuvuna misitu waliyopewa dhamana kwa kufuata utaratibu ili kuweza kuilinda isipotee.

Naye Ofisa Misitu Mkoa wa Morogoro, Joseph Chuwa, aliitaka jamii kusimamia uhifadhi wa misitu wa kutokata miti ovyo kwa sababu ukataji wa mti mmoja ni sehemu ya kupoteza vitu vingi wakiwamo wadudu na wanyama adimu.

Alisema mabadiliko ya tabianchi ni sehemu ya kuharibika mizania ya hali ya hewa inayotokana na uharibifu wa misitu na vyanzo vya maji na kwamba inapaswa kurudisha mizania hiyo na kuilinda kwa maslahi yao.

Akifunga mkutano huo, Ofisa Misitu Mkuu kutoka Idara ya Misitu na nyuki Wizara ya Maliasili Tanzania, Emmanuel Msoffe, aliitaka MJUMITA kutumia mikutano ya hadhara ya vijiji kuelimisha wanajamii umuhimu wa utunzaji misitu ili kulinda misitu ya vijiji ambayo bado iko katika hatari ya kutoweka.



## Wazalishaji wa parachichi waomba kujengewa viwanda

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZALISHAJI wa miche ya zao la parachichi mkoani hapo, wamewaomba wadau na serikali kujenga viwanda vya kuongezea thamani zao hilo ili kuwasaidia kupata soko la uhakika kwa wakulima wanapozalisha.

Ombi hilo lilitolewa jana na wanazalisha wa miche kutoka Kata ya Igawilo ambao walisema licha ya uzalishaji wa miche kwa wingi, lakini wanapata hofu ya wateja kutokana na kukosekana wa uhakika.

Miongoni mwa wakulima, Janeth Mwamlima, alisema shughuli hiyo imewasaidia kumudu gharama za maisha, uwapo wa viwanda vya kutengeneza mafuta ya kupaka yatokanayo na parachichi kusaidia kuongeza mahitaji ya zao hilo sokoni na wazalishaji nao kufaidika.

Alisema kuongezeka kwa mnyororo wa thamani wa zao hilo kwao itakuwa na manufaa makubwa kwa sababu mahitaji ya miche yatakuwa makubwa hivyo wataongeza kiwango za kuzalisha.

James Pilla, alisema kuanzishwa kwa kikundi cha parachichi kwanza mwaka 2021 na kutambuliwa na Serikali ya Mkoa wa Mbeya, kumewezesha kupata tenda mbalimbali kutoka kwa kampuni na wakulima wakihitaji miche ya kupanda.

Hata hivyo, alisema hawana maarifa ya kutosha kuhusu uzalishaji wa miche ya parachichi na kuomba Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Tari, Kituo cha Uyole kuwapatia elimu ya kuzalisha kwa kuzingatia ubora.

"Baada ya kuanzisha kikundi chetu cha kuzalisha miche bado tulikuwa tunashindwa kuzalisha katika ubora unaotakiwa hivyo sisi waoteshaji tuliwaomba wataalamu wa kilimo kutoka Tari Uyole watupatie elimu ya kuandaa vitalu na kuotesha miche kwa kuzingatia kanuni za kilimo bora," alisema Pilla.

"Tuliamua kutembelea kituo cha Utafiti wa Kilimo Tanzania Tari Uyole kwa lengo la kujifunza njia za kisasa za kuzalisha miche bora ya parachichi ukizingatia zao hili ni la kimkakati tumefundishwa mambo mengi ambayo yatasaidia kuzalisha kwa tija," aliongeza.

Alisema zao la parachichi limekuwa ni fursa kwa sababu limetoa ajira kuanzia wazalishaji wa miche, wakulima shambani pamoja na wanunuzi na kwamba wamejipanga vizuri kuongeza ujuzi wa namna bora ya kuzalisha miche itakayotoa matunda mazuri yatakayoweza kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

"Ni fursa kwa Mkoa wa Mbeya na nje ya nchi kulima zao la parachichi ambalo kwa sasa limekuwa dhahabu ya shambani sisi waoteshaji wa vitalu vya miche tunaendelea kuongeza maarifa ya namna bora ya kuzalisha miche ambayo itazalisha matunda yanayohitajika katika soko la kimataifa," alisema Pilla.

Alisema soko la miche linazidi kukua kila siku na kabla ya kujiunga kwenye kikundi cha parachichi kwanza alikuwa na uwezo wa kuzalisha miche 5,000 hadi 7,000 kulingana na mahitaji ya soko la dunia.

# Serikali kurejesha ikolojia Bonde Mto Ruaha

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SERIKALI imeanza jitihada za kujeresha ikolojia katika Bonde la Mto Ruaha ambao unategemea maji yake kutoka Bonde oevu la Ihefu na vyanzo vingine ambavyo kwa kiasi kikubwa vinapatikana wilayani Mbarali Mkoa wa Mbeya.

Kwa mujibu wa Mratibu wa kurejesha Ikolojia Bonde la Mto Ruaha na Ziwa Rukwa, Dk. Damas Mapunda, Dola za Kimarekani milioni 75.5 sawa na Sh. bilioni 16.8 za kitanzania, zimetolewa na Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF).

Alisema mradi huo ni wa miaka mitano na umelenga kurejesha ikolojia iliyoathiriwa na shughuli za kibinadamu kama kilimo na ufugaji hususani kwa Wilaya ya Mbarali. "Mradi huu unalenga kuyafikia maeneo yote yaliyoathiriwa na shughuli mbalimbali za kibinadamu kama kilimo, ufugaji na uvuvi na kusababisha ikolojia kupotea, tutahakikisha tunarudisha na kunusuru upotevu wa maji na uoto wa asili alisema, Dk. Mapunda.

Kadhalika, katika mradi huo watarejesha uoto wa asili, maji kwenye mito na kunusuru Bonde la Usangu, wilayani Mbarali ambalo limepungua kutoka kilometa za mraba 322 mpaka 84 katika kipindi cha kuanzia mwaka 1999 hadi mwaka 2006. Alisema katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira wameweka mikakati ya kujenga skimu za umwagiliaji kwenye maeneo ambayo mradi utapita ili kuepuka athari za kiuchumi kwa jamii ambayo inategemea maji ya mito na mabonde kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika mabonde ya Ruaha Kuu na Rukwa.

Alisema asilimia 15 ya maji yanayozalishwa Bonde la Mto Ruaha, yanategemewa kuzalisha umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere na kuna kila sababu ya kuhakikisha maji yanalindwa ili kuchochea uchumi wa nchi," alisema Dk. Mapunda.

Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alisema utekelezaji wa mradi huo utawahusisha watendaji kuanzia ngazi za vijiji na kata ili kupata matokeo mazuri. Alisema, halmashauri zinapaswa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mradi huo kwa kuhakikisha elimu ya utunzaji wa mazingira, ikolojia na uoto wa asili vinatunzwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye. Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Faraja Ngalageza, alisema mradi huo utafanya kazi kubwa kurejesha ardhi zilizoharibiwa kwa shughuli za kijamii.

Mradi huo unaratibiwa na ofisi ya Rais Makamu wa Rais, Mazingira na utahusisha mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Katavi na Rukwa na kwa sasa wameelekezwa maeneo yatayopitishwa mradi huo ili wakasimamie vyema utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (wa pili kushoto), akipokea tuzo ya heshima kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, iliyoandaliwa na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania jana. (Wa tatu kushoto) ni Shekhe wa Mkoa wa Mbeya, Msafiri Njalabaha.
**PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Watoto 100 wenye ulemavu wapatiwa taulo za kike

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

ZAIDI ya watoto 100 wa kike wenye ulemavu, kutoka shule nane, zikiwamo za msingi na sekondari jijini hapo wamepatiwa taulo za kike na Shirika lisilo la kiserikali la Empower Youth Prosperity (EYP), chini ya mradi wa afya wa hedhi na usafi.

Hatua hiyo ni jitihada za kuhakikisha watoto wenye mahitaji maalum wanasoma kwa amani na furaha ili kutimiza ndoto zao, EYP limewafikia zaidi ya 100 kutoka shule nane zikiwamo za msingi na sekondari.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa EYP, Ipyana Mwakyusa, wanajikita kutoa elimu kwa jamii hususani wazazi na walezi ili kuhakikisha suala la ununuzi wa pedi linakuwa sehemu ya bajeti zao wakati wa kupanga.

Alisema wazazi au walezi kwa kufanya hivyo watamsaidia mtoto wa kike pindi anapokuwa kwenye siku zake, kujiamini na kusoma kwa utulivu kwani tayari atakuwa amejisitiri.

"Tulianzisha mradi huu wa hedhi salama na usafi kwa lengo la kuwajengea ujasiri watoto wa kike hususani walio katika umri balehe kuona kwamba suala la kuvunja ungo ni sehemu ya ukuaji na hedhi haiwezi kuwa kikwazo katika kutimiza ndoto zao za kupata elimu hivyo shirika letu la EYP kwa kushirikiana na wadau mbalimbali linaendelea kutoa taulo za kike kwa mabinti shuleni na katika harambee tuliyoifanya hivi karibuni tulipata pedi za kuwasaidia mabinti 1,000," alisema Mwakyusa.

Aliongeza kuwa shirika hilo lina lengo pia la kuwawezesha mabinti wanaoishi katika mazingira magumu kwa kuwapatia mahitaji muhimu kama vile pedi zinazoweza kutumika tena baada ya matumizi ya awali.

Alisema EYP inaamini suala la hedhi ni mtambuka, wanaume nao wanashirikishwa ili kufanikisha safari ya binti au mwanamke anapokuwa kwenye siku zake kabla na baada ili asikwamishwe wakati wa kutekeleza majukumu yake ya kielimu au kiutumishi.

"Kulingana na utafiti uliofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) chini ya programu ya mpango wa kuongeza kasi ya afya ya uzazi, haki na uwezeshaji wasichana nchini, GREAT ya mwaka 2018 inaonesha asilimia 17 ya wanafunzi wa kike hukosa masomo kipindi cha hedhi," alisema Mwakyusa.

Aliongeza kuwa EYP itaendelea kushiriki kikamilifu kumsaidia mtoto wa kike mkoani Mbeya kusoma kwa utulivu na kutimiza ndoto yake ya kupata elimu bila kikwazo anapokuwa hedhi kwa kupatiwa pedi.





# Waziri aagiza 'ambulance' kukatiwa bima

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameagiza magari yote ya kubebea wagonjwa (ambulance) yakatiwe bima za ajali ili kuisaidia serikali kuacha kuendelea kupoteza fedha nyingi inazotumia kuyanunua.

Ummy alitoa agizo hilo jana jijini hapo baada ya kupokea msaada wa magari manane kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa ajili ya kukabiliana na majanga ya magonjwa yanayoathiri afya ya jamii.

Alisema serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kununua magari kwa ajili ya kubebea wagonjwa lakini yanapopata ajali ndiyo inakuwa mwisho wake.

"Katibu Mkuu, magari haya yanapaswa kutunzwa sana kwani tumekuwa tukinunua magari kwa gharama kubwa. Lazima yakatiwe bima ya ajali sijui sheria ikoje kuhusu magari ya serikali lakini ni lazima tukate bima.

"Kuna 'ambulance' tunanunua hadi Sh. milioni 120 kwa Toyota Landcruiser mkonge siyo Toyota Hiace lakini zikipinduka tu hakuna kazi ndiyo mwisho wake, hivyo naagiza ambulance zote nchini zikatiwe bima ya ajali," alisisitiza.

Pia alisema wizara yake imeanza kuyafanyia maelekezo yalitolewa na Baraza la Mawaziri kuhusu kukabiliana na majanga mbalimbali.

"Wizara yetu inameanza kujitathmini kama ambavyo Baraza la Mawaziri liliagiza hivi karibu baada ya kutokea kwa ajali ile ya ndege kule Bukoba. Tunatoa mafunzo kwa watu wengi kuwa na uwezo wa kukabili majanga kila yanapojitokeza," alisema.

Sambamba na hilo, alisema wizara imepanga kujenga kituo cha umahiri kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wataalamu mbalimbali wa sekta ya afya nchini ili kuwa na uwezo wa kukabili magonjwa ya mlipuko yanayoathiri afya ya jamii.

"Kituo hiki kitakuwa na uwezo wa kufundisha watu wetu kujifunza namna ya kuhudumia wagonjwa wa Ebola, UVIKO-19 na mengine mengi ya mlipuko kama hayo," alisema.

Kadhalika, aliagiza moja ya magali yaliyotolewa lipelekwe wilayani Misenyi kwenye kituo ambacho kulichaguliwa kama cha kijiweka tayari na mlipukko wa ugonjwa wa ebola.

"Ndugu zangu ugonjwa huu wa ebola bado upo kwa majirani zetu Uganda. Sasa hivi kuna kesi moja mpya imeripotiwa lakini hadi sasa kuna wagonjwa 141 wameripotiwa katika wilaya tisa na vifo ni 55," alisema.

Ummy alishukuru WHO kwa msaada huo ambao alisema utasaidia katika kujiandaa na kubaini mlipuko wa magonjwa yanayoathiri afya ya jamii kama vile Ebola, UVIKO-19, kipindupindi na kimeta.

Mwakilishi Mkazi wa WHO, Dk. Zabron Yoti, alisema Tanzania inakuwa nchi ya kwanza kupata msaada huo ambao magari yote manane yamegharimu Sh. milioni 500.

# Aibuka mshindi wa uenyekiti UVCCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUTANO Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Mkoa wa Dodoma, umemchagua Abdulhabib Mwanyemba kuwa Mwenyekiti wa mkoa kwa miaka mitano.

Msimamizi wa uchaguzi, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Sophia Kizigo, akitangaza matokeo ya uchaguzi wa nafasi mbalimbali za umoja huo Mkoa wa Dodoma juzi, alisema Mwanyemba alishinda kwa kupata kura 315 huku Yona Isaya akipata 285.

Alisema uchaguzi huo ulirudiwa mara mbili kutokana na kura zilizopatikana awali kutofikia nusu ya kura zilizotakiwa. Kikanuni, mshindi wa nafasi hiyo anatakiwa kupata zaidi ya nusu ya kura zilizopigwa.

Katika uchaguzi huo, Monyshose Mazanda alishinda nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa na Baraza Kuu la UVCCM Taifa na nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa UVCCM Taifa alishinda Fatuma Rashidy.

"Nafasi ya Ujumbe wa Mkutano Mkuu CCM Mkoa ameshinda Aisha Mduyah, Eunice Mallya ameshinda nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa UVCCM Mkoa, nafasi ya uwakilishi UVCCM kwenda UWT ameshinda Subilaga Biligitio, uwakilishi UVCCM kwenda Wazazi ameshinda Zuheir Masudi,"alisema.

Akizungumza na wajumbe wa mkutano huo, Mwenyekiti Mwanyemba aliwashukuru wajumbe hao kwa kumchagua na kuhakikisha anawatumikia kwa uadilifu kulingana na imani waliyoonesha kwake huku akiwataka walioshindwa kuungana na washindi kuwa kitu kimoja kujenga jumuiya hiyo.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum (wa pili kushoto), akikata utepe kuzindua rasmi programu ya maboresho ya usimamizi wa fedha za umma awamu ya sita, jijini Dodoma juzi. Wengine ni Mwakilishi wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini, Milou Vanmulken (kushoto), Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mpango, Lawrence Mafuru (wa pili kulia) na Kaimu Katibu Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Erick Kitali.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Programu ya maboresho usimamizi wa fedha kuzingatia mabadiliko tabianchi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

PROGRAMU ya maboresho ya usimamizi wa fedha za umma awamu ya sita imezinduliwa huku ikitajwa kuzingatia masuala ya mabadiliko ya tabianchi na usawa wa kijinsia.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa programu hiyo jijini hapo.

Alisema awamu ya sita ya programu hiyo itakuwa ya miaka mitano na itaangalia mabadiliko ya tabianchi kwa sababu yanachangia kurudisha nyuma maendeleo.

"Masuala mengine yatakayotazamwa na mpango huu ni jinsia ili kuweka mikakati ya kuhakikisha kila kundi linashirikishwa ili kufikia malengo husika," alisema. Pia alisema serikali itaendelea kusimamia ukusanyaji na matumizi ya mapato yake ili kuhakikisha inafanikiwa katika malengo mbalimbali yaliyokusudiwa.

Dk. Mkuya alisema serikali inaendelea kusimamia mapato na matumizi ya fedha za umma ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na nchi.

Alibainisha kuwa kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, watahakikisha mapato yanayopatikana yanasimamiwa vizuri ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Kuhusu matumizi ya serikali, waziri alisema imeendelea kuyasimamia kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkuguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema taarifa za CAG zimekuwa zikifanyiwa kazi na serikali kupitia Bunge kwa kuihoji serikali matumizi ya fedha za umma.

Aliwashukuru wadau wa maendeleo waliofanikisha uzinduzi wa programu hiyo na kuahidi kuendelea kuwatumia katika kila hatua za utekelezaji wa mpango huo.

Naye Mratibu wa Pragramu hiyo, Denis Mihayo, alisema programu hiyo ni mwendelezo tangu awamu ya kwanza iliyoanza mwaka 1990.

Mihayo alisema programu hizo zimekuwa zikifanyiwa marekebisho kila baada ya miaka mitano ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Aliitaja awamu ya kwanza kuwa ilianza mwaka 1998 hadi 2004, ya pili ilikuwa 2004 hadi 2008, ya tatu ilikuwa 2008 hadi 2012 ya nne 2012 hadi 2017 na ya tano ilikuwa 2017 hadi 2022.

Kwa mujibu wa Mohayo, katika programu hizo, wamekuwa wakiwashirikisha idara zote za serikali ili kuhakikisha programu hiyo inafanikiwa.

Aliongeza kuwa awamu hiyo prgramu hiyo iliyozinduliwa itakuwa ya miaka mingine mitano ambayo inatazamiwa kuisha mwaka 2026.

Naye Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Erick Kitali, alisema ofisi yake itahakikisha inasimamia malengo yaliyokusudiwa katika programu hiyo ya sita.



# Rais Mwinyi awakaribisha wawekezaji kutoka Kenya

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema wakati umefika kwa wawekezaji kutoka nchini Kenya kuja visiwani humo kuwekeza katika sekta za uchumi wa buluu, hususan katika sekta ya utalii.

Aliyasema hayo juzi alipozungumza na Balozi wa Kenya nchini Tanzania, Isaac Njenga, aliyefika Ikulu kwa ajili ya kujitambulisha.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeweka kipaumbele utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu inayohusisha sekta ya bandari, uvuvi, ufugaji samaki, mafuta na gesi asilia pamoja na usafiri wa baharini, huku utalii ukiwa mhimili mkuu wa kiuchumi.

Alisema Zanzibar yenye wastani wa hoteli za kitalii 600, ina mahitaji ya bidhaa na vyakula kwa ajili ya hoteli hizo na kubainisha fursa pana kwa wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nchini Kenya kuja nchini kuwekeza katika uanzishaji wa viwanda vitakavyozalisha bidhaa mbalimbali.

Dk. Mwinyi aliiomba Serikali ya Kenya kutumia fursa ya kuanzisha usafiri rasmi wa vyombo vya baharini kati ya nchi mbili hizo hatua aliyosema itaimarisha mwenendo wa kibiashara kati ya nchi mbili hizo.

Vile vile, ili kufanikisha dhana ya kuimarisha uchumi kupitia sekta ya uchumi wa buluu, alisema ni muhimu kuzingatia ushauri wa Serikali ya Kenya unaoazimia kuwajengea uwezo vijana wa Zanzibar kwa kuwapatia mafunzo katika ngazi mbalimbali kupitia vyuo vya Ubaharia Utalii College vilivyoko nchini humo.

Alisema kuna haja ya kuimarisha ushirikiano kati ya Kenya na Zanzibar kukabiliana na changamoto mpya za kiusalama katika Ukanda wa Bahari ya Afrika Mashariki.

Alisema ni muhimu kwa vyombo vya usalama kutoka nchi mbili hizo kupanua wigo wa ushirikiano katika kukabiliana na vitendo vya uharamia, usafirishaji wa dawa za kulevya pamoja na ugaidi vinavyojitokeza mara kwa mara katika mwambao wa Bahari ya Afrika Mashariki. Aidha, alisema kuna umuhimu wa kuimarisha ushirikiano wa kibiashara kati ya nchi hizo kwa kurasimisha matumizi ya bandari, wakati shughuli za kibiashara zikiendelea vyema, husussan kwa wananchi wa miji ya Mombasa na vijiji vya Shumba, Mkoa wa Kaskazini Pemba, miji ambayo iko jirani. Alishukuru kwa ushirikiano mwema na wa muda mrefu kati ya Kenya na Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, huku akiwapongeza wananchi wa taifa hilo kwa kukamilisha uchaguzi mkuu katika hali ya salama na amani.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Jamal Kassim Ali, akizungumza na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, ofisini kwake, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# COSTECH yazindua mwongozo utoaji vibali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH), imezindua mwongozo wa utoaji vibali vya utafiti na mwongozo wa kamati za kusimamia maadili ya utafiti Zanzibar ili kuhakikisha utafiti wote unaofanyika unakuwa na ubora na viwango huku vikizingatia sheria, taratibu na kanuni za nchi.

Akizungumza jana katika hafla ya uzinduzi huo uliofanyika mjini hapo, Mkurugenzi wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Tume hiyo imeratibu uanzishwaji wa miongozo inayosimamia uendeshaji wa kamati za maadili ya utafiti katika taasisi nne Zanzibar ikiwamo taasisi ya utafiti wa kilimo, mifugo, afya na uvuvi.

Alisema Tume imewezesha utengenezaji wa mwongozo wa utoaji wa vibali kwa Taasisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu wa shughuli za Baraza la Wawakilishi na Taasisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, lengo ni kuhakikisha utafiti wote unafanyika katika ubora na viwango vya hali ya juu vikizingatia sheria, taratibu na kanuni za nchi.

Alisema katika kufanikisha mchakato wa uandaaji wa miongozo hiyo, COSTECH ilichagua wawakilishi wawili kutoka katika taasisi hizo kusimamia kuundwa kwa miongozo hiyo.

Aidha, kwa kipindi cha mwaka 2018 hadi 2021, serikali imewekeza Sh. bilioni 1.6 kugharamia wawekezaji mbalimbali wa utafiti na ubunifu visiwani humo.

Alisema serikali kupitia COSTECH inatarajia kuanzisha ukumbi wa ubunifu utakao kuwapo katika Ofisi za COSTECH Maruhubi na imetenga Shilingi milioni 250 kwa ajili ya kazi hiyo.

"Tunategemea ifikapo Desemba, mwaka huu, ukumbi wa ubunifu katika ofisi zetu za Maruhubi utakamilika ili vijana kupata usaidizi wa karibu," alisema.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Ibrahim Mussa Haroun, alisema uwapo wa mwongozo huo utaiwezesha wizara hiyo kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa hasa ikizingatiwa kuwa wizara hiyo ni wadau wakubwa wa utafiti.

Alisema katika uchumi wa buluu sekta kuu ni uvuvi na mazao ya baharini na maeneo hayo yanahitaji utafiti ili kupata matokeo sahihi.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shabani Seif Mwinyi, alisema COSTECH inatoa ushirikiano mzuri kwa wizara hiyo kuhakikisha utafiti wa mifugo na kilimo unafuata miongozo ya kiutafiti kwa mujibu wa kisayansi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili, Sera, Utaribu na Shughuli za Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, alisema ili kufanya utafiti wenye ubora na viwango vya juu katika ushindani wa kimasoko ndani na nje ya nchi ni muhimu kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

Aidha, alisema hivi sasa sayansi, teknolojia na ubunifu zinaleta mapinduzi makubwa katika sekta mbalimbali ikiwamo afya, kilimo, mifugo, viwanda na huduma nyingine za kijamii duniani.

# TMEA yaikabidhi wizara mashine uchunguzi magonjwa mlipuko

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuimarisha utayari dhidi ya ueneaji wa maradhi ya kuambukiza, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kushirikiana na Taasisi ya Trade Mark East Afrika (TMEA), imeikabidhi Wizara ya Afya Zanzibar mashine za kisasa za uchunguzi wa awali wa maradhi hayo ikiwamo UVIKO-19, ebola na malaria.

Makabidhiano ya vifaa hivyo yalifanyika jana katika viwanja vya ndege vya Abeid Amani Karume, vifaa hivyo ni kwa ajili ya viwanja vya ndege na bandari.

Akizungumza baada ya makabidhiano hayo, Waziri wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shabani, alisema uwekaji wa vifaa hivyo katika viwanja vya ndege na bandari utaimarisha, juhudi za serikali katika kuifanya mipaka kuwa salama na wazi kwa biashara.

Alisema utalii ndio tegemeo kuu la maisha ya Zanzibar na kufanya wafanyakazi walio mtari wa mbele na jamii kubwa ya Wazanzibari kuwa katika hatari ya kushambuliwa na magonjwa ya kuambukiza.

Alisema ununuzi wa vifaa hivyo ni sehemu ya mpango wa TMEA wa kituo cha dharura cha biashara salama ambao ulizunduliwa ili kukabiliana na kuenea kwa kasi janga la UVIKO-19 ambalo limekumba vivuko vya mashariki na kusini mwa Afrika na kusababisha hali mbaya ya kibiashara.

Alisema mataifa mengi yalikuwa na hofu katika kuzuia mwingiliano wa watu wakati baadhi ya nchi ikiwamo Tanzania imefungua milango biashara ziendelee bila ya vikwazo.


Naye Waziri Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema vifaa hivyo vitasaidia uchunguzi wa maradhi ya kuambukiza kwa wasafiri wanaotumia viwanja vya ndege na bandari na maeneo hayo yana uhaba wa vifaa vya ukaguzi.

Alisema vifaa hivyo vitatunzwa na kuenziwa kwa kuwa vitasaidia masuala ya biashara ikiwamo ya bidhaa na utalii na Zanzibar kuwa sehemu salama ya biashara, utalii na sehemu salama ya kuishi.

Kadhalika, alisema ugonjwa wa UVIKO-19 bado upo ni vyema wananchi wakaendelea kuchukua tahadhari za kujikinga.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TMEA, Monica Hangi, alisema wamejipanga kusaidia watumishi wanaofanya kazi katika viingilio, watumiaji wa mipaka na jamii ili kuhakikisha biashara inaendana na matibabu.

"Vifaa hivi tulivyovitoa vina thamani ya Sh. milioni 700 na lengo ni kusaidia uwezeshaji salama wa shughuli za kibiashara," alisema.





# Wanaume 500 wafanyiwa tohara Bariadi

**Na Ndalike Sonda,** BARIADI

WANAUME 500 Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, wamefanyiwa tohara kinga kwa kipindi cha wiki nne kuanzia Oktoba 17, mwaka huu, katika vituo vinne vilivyotengwa kwa ajili ya huduma hiyo.

Msemaji wa Huduma ya Tohara Kinga kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi, Wilium Sitta, alisema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe. Alisema huduma hiyo inatolewa bure katika zahanati ya Nyamikoma, Banemi na katika senta za Mitindu na Mwashagata. Alisema wanaume wenye umri zaidi ya miaka 25 idadi yao imekuwa ikiongezeka kulinganisha na miaka ya nyuma na kwamba huduma hiyo ni endelevu, hivyo wanaume ambao bado hawajafanyiwa tohara wanaombwa kwenda katika vituo vya afya kwa ajili ya kupata huduma hiyo.

Sitta pia aliwashauri wazazi na walezi wenye vijana walio chini ya umri wa miaka 18 kuwapeleka katika vituo vya afya ili kufanyiwa tohara kinga.

Anania Makores (23), mkazi wa Banemi wilayani Bariadi na Charles Machimu (20) Mkazi wa Ihale, Busega ni miongoni mwa wanaume walionufaika na huduma ya tohara kinga.

Kutokana na kupata huduma hiyo, Makores na Machimu waliwashauri vijana wenzao ambao bado hawajapata huduma hiyo kwenda kufanyiwa tohara kwa kuwa haina madhara kutokana na kuwa salama.

"Nimefanyiwa tohara kinga baada ya kupata ushauri na kufahamu faida zake kutokana na hapo awali nilishindwa kufanyiwa tohara kinga kutokana na kutokuwa na uelewa wa masuala hayo pamoja na uoga," alisema Machimu.

Huduma ya tohara kinga kwa wanaume inatolewa bure katika mkoa wa Simiyu chini ya udhamini wa Shirika la TCDC kwa kushirikiana na AMREF kupitia mradi wake wa afya kamilifu



Mtaalamu wa Jinsia na Maendeleo kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Hans Obote (kulia), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Shilela na Sekondari ya Nyikoboko, wakati akitoa elimu ya namna ya kutoa taarifa ya vitendo vya ukatili vinavyofanyika shuleni na majumbani mwao, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wazazi 18 matatani kwa madai ya kukwamisha watoto kuhitimu msingi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani, ametangaza kuwachukulia hatua za kisheria wazazi wa watoto 18 ambao hawakufanya mitihani ya kumaliza darasa la saba katika kata ya Nyahua wilayani Sikonge mkoani hapo.

Alitoa kauli hiyo juzi katika mkutano wa hadhara ulifanyika kwenye kijiji cha Nyahua wakati wa ziara ya kukagua shughuli za maendeleo katika wilaya mbalimbali za mkoa wa Tabora.

Balozi Dk. Batilda alisema kitendo kilichofanywa na wazazi hao hakiwezi kuvumiliwa kwa kuwa vijana hao wamekosa fursa ya kufanya mitihani ya kumaliza elimu ya msingi ambayo ni muhimu katika maisha yao.

Alisema hatua hiyo ni unyanyasaji dhidi ya mtoto huku akiahidi kuwachukulia hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa wazazi wengine ambao wanatarajia kuwazuia watoto wao katika hatua zao za kielimu. "Serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili watoto wasome bure kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha sita, hivyo ni wajibu wa wazazi kuwapeleka watoto wao shule," alisema.

Awali, Ofisa Elimu wa Wilaya ya Sikonge, Suzan Makoye, alimweleza mkuu wa mkoa kuwa wanafunzi 18 hawakufanya mitihani ya kumaliza elimu ya msingi na hakukuwa na taarifa wala sababu yoyote kutoka kwa wazazi.

Alisema kati ya watoto hao ambao hawakufika kufanya mitihani, 12 wanatoka katika Shule ya Msingi Makibo, watoto watatu Nyahua Station huku wengine watatu wakitokea Nyauhanga.

Dk. Buriani aliutaka uongozi wa elimu wilayani humo kuhakikisha wazazi hao wanakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria ili kujieleza ni kwa nini watoto hao siku ya mitihani hawakufika shuleni kwa ajili ya kufanya mitihani.

# Waonywa kuwapa dawa mvuto mapenzi watoto

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKISHO la Waganga wa Tiba za Asili (SHIVYATIATA) Kanda ya Magharibi, limesema halitawavumilia na kuwalinda waganga wa jadi wanaotoa dawa za mvuto wa mapenzi kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 18.

Kwa mujibu wa shirikishi hilo, dawa hizo zimekuwa zikisababisha kuwapo kwa ndoa za utotoni na watoto kuendelea kunyanyasika.

Mratibu wa Shirikisho hilo, Athumani Waziri, alisema hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili huku akibainisha kwamba tabia hiyo ya kuwaogesha dawa za mvuto wa mapenzi watoto imeenea maeneo mengi ya vijijini na lazima utoaji wa dawa hizo uangalie ni mtu wa aina gani ambaye anapatiwa.

Alisema dawa hizo zimekuwa zikitolewa kwa wingi kwa kundi la watoto wenye umri chini ya miaka 18 na zinasababisha kuwapo kwa ndoa nyingi za utotoni zinazosababishwa na utumiaji wa dawa hizo maarufu 'samba' licha ya kuwapo kwa muda mrefu.

Waziri alisema dawa hizo zina matumizi mengi ikiwamo kutumika katika biashara mbalimbali na haipaswi kutumiwa na watoto au mtu yeyote ambaye yuko chini ya miaka 18 ndiyo maana wamepanga kutowavumilia wala kuwalinda waganga wanaotumia dawa hiyo kinyume na matumizi.

"Sisi shirikisho la waganga wa kienyeji tumetoa angalizo kwa mganga yeyote ambaye atabainika kujihusisha na kutoa dawa ya samba kwa watoto wadogo, hususani wa kike, tutamchukulia hatua kali za kisheria kwa mujibu wa sheria zetu za shirikisho tulizojiwekea,"alisema Waziri.

Aliongeza kuwa kuna operesheni ambayo wataifanya kwa kupita kwa wakuu wa mikoa kwa ajili ya kupata baraka ya kupita katika wilaya ili kuona kama kuna waganga wenye vitambulisho pamoja na wale ambao hawana ili kuwabaini kama walisajiliwa kihalali au la. Waziri ambaye ni msimamizi wa mikoa ya Shinyanga, Kigoma na Tabora, alisema dawa hiyo imekuwa ikishamiri siku hadi siku hasa kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika mikoa hiyo na kwamba wameamua kuzungukia vijiji vyote na kata kutoa elimu kabla ya kuanza kuchukua hatua.

Dedy Elias, mkazi wa Igunda Halmashauri ya Ushetu alisema kwa hatua ambazo shirikisho hilo litakuwa linazichukua kwa waganga wanaokwenda kinyume, itasaidia kupambana na ndoa za utotoni hususani kwa wanafunzi ambao wakati mwingine wanalazimishwa kuozeshwa na wazazi kwa tamaa za mali.

Hata hivyo, aliwashauri kuhakikisha wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa waganga wao na kuwabaini wale ambao hawajasajiliwa kihalali kufanya shughuli hizo kwa kuwa wamekuwa wakiwachafua wenzao.

HABARI KIMATAIFA

## Kikosi cha EAC nchini DRC chaapa kulinda mji wa Goma

**GOMA, DRC**

KAMANDA wa kijeshi wa kikosi cha pamoja cha Jumuiya ya Afrika Mashariki nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Jeff Nyagah, ameapa kuulinda mji muhimu wa Goma.

Mji huo ulioko katika mpaka na Rwanda unatishiwa na waasi wa M23 wanaozidi kusonga mbele.

Kamanda Nyagah, ambaye anatoka Kenya, amenukuliwa jana akisema kwamba hakuna mtu yeyote atakayeudhibiti mji wa Goma na kuongeza kuwa wako tayari kuulinda mji huo na uwanja wa ndege.

Wanajeshi wapatao 100 wa Kenya waliwasili katika mji wa Goma mwishoni mwa juma lililopita, kama sehemu ya operesheni mpya ya pamoja ya Jumuiya ya Afrika mashariki inayokusudia kurejesha utulivu mashariki mwa Congo.

Kulingana na shirika la habari la AFP, askari takribani 60 wengi kutoka Kenya walisambazwa jana huku waasi wa M23 wakiwa kilometa kadhaa kutoka mji wa Goma.

**DW**

## Washirika wa Ethiopia kuondoka Tigray

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

WAZIRI wa Huduma ya Mawasiliano ya Serikali ya Ethiopia, Legese Tulu amesema kuwa vikosi vyote vinavyopigana katika eneo la Tigray ambavyo si sehemu ya jeshi la shirikisho vitaondoka mara tu waasi watakapoweka chini silaha.

Vikosi vya majimbo ya Amhara na Afar, pamoja na wanajeshi wa Eritrea, wamekuwa wakipigana pamoja na vikosi vya serikali katika vita vya miaka miwili dhidi ya waasi wa Tigray People's Liberation Front (TPLF).

Serikali na TPLF walitia saini makubaliano ya amani Novemba 2, mjini Pretoria nchini Afrika Kusini, ili kumaliza vita kaskazini mwa nchi hiyo.

Pia jeshi na makamanda wa waasi walitia saini makubaliano ya kusitisha mapigano jijini Nairobi nchini Kenya, Novemba 12.

Wakati huo huo, chama cha upinzani katika eneo la Tigray, Baytona Tigray, kimepinga makubaliano ya amani, kikisema TPLF haiwakilishi watu wa eneo hilo.

***BBC***

# Marekani, Nato waitetea Russia kuhusu kombora lililoua Poland

**BRUSSELS, Ubelgiji**

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Kujihami ya Nchi za Magharibi (NATO), Jens Stoltenberg, amesema kombora lililoua watu wawili nchini Poland juzi huenda lilitoka Ukraine.

Alisema kuna uwezekano mkubwa kombora hilo ni la ulinzi wa anga la Ukraine, hata hivyo uchunguzi unaendelea kuhusu mlipuko huo uliotokea karibu na mpaka wa Ukraine.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa Russia inaweza kulaumiwa kwa sababu ya uvamizi wake unaoendelea Ukraine.

Ukraine yenyewe inaendelea kusema kuwa Russia ndio ilirusha kombora hilo na si wao.

"Sina shaka kuwa hili sio kombora letu," alisisitiza Rais Volodymyr Zelensky, katika hotuba yake kwenye televisheni.

"Ninaamini kuwa hili lilikuwa kombora la Russia, kulingana na ripoti zetu za kijeshi."Alisema.

Kiongozi huyo alisema ni muhimu kwa Ukraine kuruhusiwa kujiunga na uchunguzi wa mlipuko kwenye shamba la Przewodow, kilomita 6 kutoka mpakani.

Mifumo ya ulinzi wa anga ya Ukraine ilifunguliwa siku ya tukio wakati Russia ilipozindua mashambulizi yake makubwa zaidi ya makombora katika muda wa miezi tisa tangu uvamizi huo wa Februari 24 mwaka huu.

Makumi ya makombora ya Russia yalilenga nchi hiyo lakini Ukraine ilisema ilifanikiwa kudungua mengi kati yao.

Shambulio hilo, lililotokea wakati wa mkutano wa G20 nchini Indonesia, lilisababisha kilio cha kimataifa, huku habari za mlipuko wa kombora ndani ya eneo la Poland mwanachama wa Nato zikizusha hofu kwamba huenda vita hivyo vikiongezeka kuwa hatari.

Stoltenberg alisema Nato iliahidi kutoa mfumo wa hali ya juu zaidi wa ulinzi wa anga kwa Ukraine ambayo si mwanachama wa muungano huo lakini inapokea msaada mkubwa wa kijeshi.

"Leo (jana) nilihudhuria mkutano wa kikundi cha usaidizi cha Ukraine ambapo washirika wa Nato walitoa ahadi mpya kwa mifumo ya juu zaidi ya ulinzi wa anga ili tuweze kusaidia kuangusha makombora ya Russia," mkuu wa Nato alisema.

"Hatuna dalili kwamba hili ni shambulio la makusudi kutoka Russia," alifafanua akizungumza kutoka makao makuu ya Nato huko Brussels.

Aliongeza, kwamba hata hivyo hakuna shaka kwamba Russia inahusika kwa sababu hili lisingetokea ikiwa haingeanzisha mashambulizi ya makombora dhidi ya miji ya Ukraine juzi.

Rais wa Poland, Andrzej Duda alisema hapo awali kwamba ingawa kombora la S-300 lililotengenezwa na Russia na ndio yenye kulaumiwa hakuna ushahidi kwamba nchi hiyo ilihusika kurusha.

Wakati huo huo, Rais Volodymyr Zelensky alisema hana mashaka kwamba Ukraine haikupaswa kulaumiwa kwa shambulio la kombora lililoua watu wawili nchini Poland.

Zelensky alisema amepokea hakikisho kutoka kwa makamanda wake wakuu kwamba halikuwa kombora kutoka kwao.

Pia alitoa wito kwa maofisa wa Ukraine kuruhusiwa kuingia eneo la mlipuko huo na kuwa sehemu ya uchunguzi.

Rais wa Marekani Joe Biden pia alitilia shaka kauli ya Zelensky kwamba kombora hilo halikuwa la asili ya Ukraine, akiwaambia waandishi wa habari kuwa huo sio ushahidi.

***BBC***



Wataalamu wa polisi wakichunguza baada ya shambulio la kombora katika kijiji kimoja, karibu na mji wa Lviv, magharibi mwa Ukraine, juzi. **PICHA: AFP**

# Watatu wafariki dunia baada majengo kuporomoka Kenya

**NAIROBI, Kenya**

WATU watatu wamefariki na wengine wamekwama katika kifusi baada ya majengo mawili ya ghorofa kuporomoka katika mji wa Nairobi nchini Kenya.

Katika tukio la kwanza jengo la ghorofa saba limeporomoka na kusababisha vifo vya watu hao na wengine 10, wakiendelea kutafutwa ndani ya kifusi.

Watu walioathirika na tukio hilo wengi wao wanadhaniwa kuwa mafundi ujenzi.

Ripoti zinasema kuwa watu sita wameokolewa kutoka kwenye kifusi cha jengo hilo la ghorofa saba ambalo lilikuwa bado linaendelea kujengwa.

Hata hivyo, msimamizi wa ujenzi wa jengo hilo mara mbili alipuuza maonyo kutoka kwa wenye mamlaka ya kusitisha kazi ya ujenzi kufuatia wasiwasi kuhusu uimara wake, ripoti ya tovuti ya Nation ilisema.

Mpaka jana asubuhi vikosi vya uokoaji vilikuwa bado kwenye eneo la tukio, huku mashine nzito zikiondoa vifaa vya ujenzi wakijaribu kuwatafuta watu waliofukiwa chini ya vifusi.

Katika tukio lingine, wafanyakazi wa uokoaji nchini humo wanajaribu kuwafikia watu wa familia moja inayoaminika kukwama baada ya jengo la ghorofa sita lililokuwa likijengwa kuangukia nyumba yao alfajiri ya jana. Jengo hilo lilianguka katika eneo la Ruaka katika kaunti ya Kiambu, ambayo ni jirani na mji mkuu wa Nairobi.

Kulingana na kituo cha huduma, St John Ambulance nchini humo, familia hiyo ilikuwa imelala katika nyumba yao wakati jengo jirani liliporomoka.

***BBC***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**SOPHIA ISSA MWANGA,** Anatangaza kupotea kwa vyeti vyake. Cha Kidato Cha nne chenye Index No **s1177-0054** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa mwaka 2013 **MAMIRE SECONDARY SCHOOL.** Cheti Cha chuo cha **INSTITUTE OF ACCOUNTACY ARUSHA** -Basic Technician Certificate in Business Management (NTA Level 4) Reg.No.BTCBM/0620/T.2016. Kwa atakayeviona atoe taarifa polisi kwa namba **ARU/ARU/RB/351409/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA BABATI LILILOPO BABATI**

**MAOMBI MADOGO NA 263 YA 2022**

**SERAPHINE RICHARD.....MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**1. ERIC MMARI.....WAJIBU MAOMBI**
**2. MARK RECOVERIES LTD**

**Wadaiwa popote mlipo.**

Fahamu kwamba mleta Maombi (SERAPHINE RICHARD) ameleta Maombi Na.58/2022 dhidi yenu.

Hivyo basi kama mnakusudia kupinga maombi hayo mnatakiwa kuleta majibu yenu na muwepo Barazani nyie wenyewe,wakili wako au mwakilishi anayekubalika kisheria,Shauri limepangwa kutajwa tarehe 24/11/2022.

Endapo hamtatekeleza shauri litasikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa maamuzi.

Imetolewa na kutiwa Saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 8/11/2022.

THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL * MANYARA *

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) BABATI

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YEMELA ELIAKIM NDIBALEMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 506 BEB – TOYOTA CARDINA.** Chassis namba **ST2104046992.** Engine namba **357977743.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/447646/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - MWANZA**

**SHAURI NA 89 LA 2021**

**1. CHARLES PASCHAL**
**2. LUCAS PASCHAL..........................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**1. MATHIAS JACOB**
**2. GEORGE KUMALIJA**
**3. LAURENT PASCHAL ................................WAJIBU MAOMBI**

**KWA: MATHIAS JACOB, GEORGE KUMALIJA na LAURENT PASCHAL**

Mnafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua Shauri / Ombi dhidi yenu katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza, Ombi hili limepangwa kusikilizwa tarehe 31/01/2023 katika chumba cha Baraza, Barabara ya Makongoro jengo liko mkabala na Mahakama ya Mwanzo Mwanza mjini na mahakama ya Wilaya Nyamagana, Tanzania.

Kwa hivyo mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo ninyi wenyewe, wakili wenu au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria. KAENI- Mkijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila nyie kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 17/11/2022.

MURIRYA N.
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MWANZA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - MWANZA**

**SHAURI NA 177 LA 2022**

**BAGAIRE CHIGUGU.......................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**1. CHRISTINA MAU**
**2. ELIADA PHINIAS MACHUMU**
**3. ROCK CITY TAKERS LIMITED**
**4. CHINGORO MATAGE...................................WAJIBU MAOMBI**

**KWA: ELIADA PHINIAS, ROCK CITY TAKERS LTD na CHINGORO MATAGE**

Mnafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua Shauri / Ombi dhidi yenu katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza, Ombi hili limepangwa kusikilizwa tarehe 08/12/2022 katika chumba cha Baraza, Barabara ya Makongoro jengo liko mkabala na Mahakama ya Mwanzo Mwanza mjini na mahakama ya Wilaya Nyamagana, Tanzania.

Kwa hivyo mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo ninyi wenyewe, wakili wenu au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria. KAENI- Mkijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila nyie kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 17/11/2022.

MURIRYA N.
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MWANZA

---

## KUPOTELEWA NA CHETI



**Datius B. Mutalemwa** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S1689-0087** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Peace Secondary School mwaka 2012. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PWA/MAP/RB/443660/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JACOB MZIRAI NGUSARU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 296 AXT – SHERPA.** Chassis namba **XLRZKNTN8AN838589.** Engine namba **17VC9511D4499.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/447640/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FRANCIS JOSEPH ITENGEJA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA Mark II** yenye namba za usajili **T 754 AKP** LENYE CHASES NAMBA: **SX805072371.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/442994/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOFRAM JOHN MBINGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA NISSAN TERRANO, INAYOTAMBULIKA KWA MAJINA YA JOFRAM JOHN MBINGA. GARI YENYE USAJILI **T.781 B J S,** CHASIS NO. **LD 60000152.** ENG NO **VG 33 EA 0152,** ENG CAPACITY **3270.** YEYOTE ATAKAEBAHATIKA KUOKOTA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. POLISI TAARIFA: **LIN/LIN/RB/446021/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MAGDALENA KULWA MALABA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 742 CUG.** CHASSIS NAMBA: **MD2B15BX8LWJ87271.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **IR/IR/RB/446757/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MELANCE MICHAEL KISOKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 890 APP – SUZUKI VITARA.** Chassis namba **TDOIW202193.** Engine namba **G16A367186.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/445437/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 2222/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MWAJUMA JUMANNE KAPINGA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MWANSITI HAMISI JUMA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 06 Mwezi wa 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 16 Mwezi wa 11 Mwaka 2022.

HAKIMU

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Tupigie 0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# SUGU

## ABANWA TENA NA SIASA

BAADA ya kuzindua kibao cha 'Taita', rapa mkongwe Joseph Mbilinyi 'Sugu', amesema sasa anataka kujikita zaidi kwenye siasa, hasa wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi mwaka 2024/2025.

Mbunge huyo wa zamani wa Mbeya Mjini kupitia CHADEMA, amesema chama hicho kwa sasa kiko kwenye mikakati mbalimbali ya kukiwezesha kuanza harakati za kisiasa.

"Juzi nilikuwa Tarime mkoani Mara na sasa ninaelekea katika maeneo mengine na nitafika kwangu Mbeya, hivyo majukumu haya yatanibana nitakosa muda wa kufanya muziki,"amesema Sugu.

Amefafanua kuwa alitoa wimbo wa Taita ulizinduliwa Mei mwaka huu, kwa kuwa alikuwa na nafasi na muda wa kutosha, na kwamha harakati za sasa hazimpi nafasi ya kutoa nyimbo mpya.

"Mimi bado ni msanii wa muziki wa kizazi kipya, ndio maana nikatoa wimbo wa 'Taita', hivyo harakati za chama ambazo tunaendelea nazo kwa sasa hazimaanishi kuwa nimeachana na muziki huo," amesema.

Rapa huyo mkongwe amesema kuna mikakati kuandaa na kusimamia onyesho la kila msanii mkongwe wa muziki huo, na kwamba atakapokamilisha mikakati hiyo ataweka wazi ni lini ataanza.

## KIMOBITELI AAHIDI KUKOMALIA KIMO BAND



MWIMBAJI wa muziki wa dansi, Khadija Mnoga 'Kimobitel', ambaye amepitia bendi mbalimbali, amesema hatarajii kurudi nyuma katika hatua alizochukua za kuanzisha bendi yake.

'Kimobitel' anamiliki bendi yake aliyoipa jina la Kimo Band ambayo imekuwa ikifanya maonyesho, katika kumbi mbalimbali ndani na nje ya jiji la Dar es Salaam, huku akidai amechoka kuajiriwa.

"Nimeajiriwa kwa miaka mingi imetosha, nimeamua kujitegemea na sitarajii kurudi nyuma, katika uamuzi huu nilioufanya, kwani ninataka nifike mbali kuhakikisha Kimo Band inakuwa bendi kubwa," amesema Kimobitel.

Ametaja moja ya mbinu atakazotumia kuhakikisha bendi yake inaendelea kuwa imara kuwa ni kuandaa nyimbo za kutosha na nzuri ambazo zitaendelea kuitambulisha ndani na nje ya nchi.

"Tangu bendi hii ianzishwe, Februari mwaka huu, hadi sasa tuna nyimbo kadhaa tulizokamilisha kama 'Macho Kodo, Fahmillilah, Mapenzi ya Sasa na Sikutegemea ambazo zinaendelea kuitambulisha Kimo," amesema.

Mwimbaji huyo ameongeza kuwa kwa sasa anaendelea na mikakati ya kutaka kufanya onyesho la utambulisho rasmi wa bendi hiyo kwa waandishi wa habari na wadau wengine wa muziki wa dansi.

## FRESH JUMBE ALIA NA VYOMBO VYA MUZIKI



NYOTA wa muziki wa dansi Fresh Jumbe, anayefanya shughuli za muziki nchini Japan, ameshauri zifanyike juhudi za kuhamasisha upigaji wa vyombo vya muziki ili kuendelea kuwa nao kizazi hadi kizazi.

Amesema wanamuziki wa dansi na wasanii wa muziki wa kizazi kipya wasipohamasishwa kujifunza kupiga vyombo wa muziki kuna hatari ya kukosa wataalam wa vyombo hivyo kwa miaka ijayo.

Jumbe alisema hayo hivi karibuni wakati akihojiwa na kituo kimoja cha redio jijini Dar es Salaam na kufafanua kuwa wanamuziki wengi kwa sasa wanakimbilia kwenye uimbaji badala ya kujifunza kupiga vyombo.

"Kila mtu anakimbilia kwenye uimbaji kwa kuwa huko ndiko ataonekana kirahisi, inatakiwa tuwe na wapiga vyombo wengi kama matarumbeta, magitaa na vingine, ikiwa hivyo ajira zinaweza kuongezeka," alisema Jumbe.

Anafafanua kuwa kwenye muziki wa dansi kuna nafasi nyingi kuanzia uimbaji, upigaji vyombo na hata kucheza na kwamba kubakia kuendelea kuimba tu bila kujifunza kupiga vyombo, ni sawa na kupunguza ajira.

Jumbe alisema kuna haja kwa wanamuziki wa sasa kuchukua hatua za kujifunza kutoka kwa wenzao wa zamani ambao wengi wao walikuwa utaalamu wa ujuzi wa kupiga vyombo mbalimbali vya muziki.

HABARI MICHEZO

# MINZIRO: NILISEMA KUNA MTU ATAKULA NYINGI

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Geita Gold, Fred Felix Minziro, amesema kuwa alifuatilia mechi za Prisons na kugundua kuwa wana udhaifu kwenye sehemu yao ya kiungo, hivyo akaweka mkakati wa kuwashambulia mfululizo kiasi cha kupata idadi kubwa ya mabao, lakini akikumbushia kuwa alishawahi kutabiri timu yake itakuja kushinda mabao mengi.

Akizungumza baada ya mechi iliyochezwa juzi Uwanja wa Sokoine na kushinda mabao 4-2, Minziro alisema kuwa alishawahi kuongea huko nyuma kuwa ipo siku isiyo na jina ataifunga timu yoyote ya Ligi Kuu mabao mengi kutokana na timu yake jinsi inavyocheza kwa sasa.

"Niliiangalia Prisons niligundua madhaifu yao ni kwamba wanatumia sana nguvu, halafu wana udhaifu kwenye eneo lao la kiungo, nilichofanya leo nikaweka watu wa kushambulia na tukawashambulia mfululizo na kweli tukapata ushindi. Nilishawahi hapa kusema kuwa kwa jinsi timu inavyocheza kuna siku mtu atakula goli nyingi na kweli imetokea na si mechi hii tu," alijigamba Minziro.

**Alisema wapinzani wao Geita Gold waliikamata mechi kwa dakika 15 za kwanza, lakini baada ya hapo wakabadilika na kuanza kuwapelekea moto wa mashambulizi.**

Naye Kocha Mkuu wa Prisons, Patrick Odhiambo, amesema kilichoamua mechi hiyo ni kwamba baadhi ya viwango vya wachezaji wa Gaita Gold vilikuwa juu kuliko vya kwao.

"Ni mechi nzuri na tumecheza vizuri sana, lakini nadhani kilichoamua mechi hii leo ni viwango vya wachezaji, wenzetu wachezaji wao leo walikuwa kwenye viwango vya juu sana," alisema Odhiambo.

Kwa matokeo hayo, Geita Gold imepanda hadi nafasi ya sita ikiwa na pointi 17 kwa mechi 12 ilizocheza huku Prisons ikibaki na pointi zake 14, kwenye nafasi ya 10 ya msimamo wa Ligi Kuu ikicheza michezo 12 pia.



Timu ya Riadha ya Mkoa wa Dar es Salaam wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar e Salaam jana kujiandaa na mashindano ya mikoa yanayotarajia kufanyika mwezi huu jijini humo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Karate Dar kushiriki tamasha Binti Makini

Na Shufaa Lyimo

TIMU ya Karate imepata nafasi ya kushiriki kwenye Tamasha la Binti Makini litakalofanyika kesho jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Karate, Levina Molel, alisema ameshukuru timu yao kupata nafasi hiyo.

"Tumefurahi kupata nafasi ya kushiriki katika tamasha hilo tutaonyesha michezo mbalimbali inayochezwa na wanawake," alisema Levina.

Aliitaja michezo ambayo watakayoionesha siku hiyo kuwa ni 'Kamite defence' pamoja na mingine mingi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Taasisi ya Binti Makini, Janeth John alisema lengo la tamasha hilo ni kuonyesha shughuli mbalimbali zinazofanywa na wanawake.

Alisema wataendelea kushirikiana kwenye michezo mingine na kudai mwaka huu wameamua kuanza na mchezo huo.

## Azam yaahidi muziki mnene kwa Namungo

Na Shufaa Lyimo

KIKOSI cha Azam FC kinaendelea kujinoa kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya Namungo FC utakaopigwa keshokutwa mkoani Lindi.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha wa timu hiyo, Kali Ongala alisema wachezaji wanaendelea vema na mazoezi kuelekea kwenye mchezo huo.

"Timu inaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kwenda kukutana na timu ya Namungo lengo letu ni kupata pointi tatu," alisema Ongala.

Kocha huyo alisema makosa aliyoyaona katika mchezo uliopita anaendelea kuyafanyia kazi yasijirudie katika mchezo huo.

"Makosa niliyoyaona katika mchezo wetu uliopita ninaendelea kuyafanyia kazi ili yasijirudie katika mchezo wetu ujao.

Alisema anaupa umuhimu mchezo huo kwani anaamini hakuna timu yoyote ya kubeza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

# Kocha Dodoma afichua siri kuifunga KMC

Na Hadija Mngwai

BAADA ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya KMC, Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Liogope, amesema kuwa walitumia mechi kadhaa kuwachunguza wapinzani wao hivyo kufanikiwa kuwazidi mbinu na kuibuka na pointi tatu katika mchezo huo.

Dodoma ilifanikiwa kupata ushindi wake wa kwanza dhidi ya KMC tangu msimu huu wa Ligi Kuu Bara 2022/23 uanze na kujikuta ikishikilia nafasi ya 14 ya msimamo wa ligi ikiwa imecheza mechi 11 ikiwa na pointi tisa.

Akizungumza na Nipashe, Liogope amesema kuwa walipata nafasi ya kuwachunguza wapinzani wao hao katika michezo iliyopita na kutambua udhaifu wao na kufanikiwa kuibuka na pointi tatu ugenini.

"Mchezo ulikuwa mzuri na mgumu KMC walicheza mpira wa kuweka chini kama sisi, lakini tuliwaangalia katika michezo yao ya mwisho kwenye ligi ambapo tuliwaona full back wao na winga walikuwa na nguvu ya kushambulia hivyo tuliwajua vyema kabla ya kukutana nao.

"Katika mchezo wetu tuliwaona katika kipindi cha kwanza waliacha mwanya upande wa kushoto na katika kipindi cha pili waliacha mwanya upande wa kulia na tulifanya mabadiliko ya haraka na kujipanga hivyo kufanikiwa kushinda.

"Tunajipanga kuhakikisha tunafanya vizuri katika michezo inayofuata ili kujihakikishia nafasi ya kumaliza mzunguko wa kwanza katika nafasi nzuri," alisema Liogope..

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LISBON YAMKANA RONALDO
RAIS wa Sporting Lisbon, Frederico Varandas amekanusha ripoti zinazohusisha klabu hiyo ya Ureno kutaka kumnunua Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, akisema kwamba dau la kumnunua fowadi huyo wa Manchester United na Ureno halijajadiliwa kamwe. ***(RTP3, viaSun)***

### MOUNT SAFI CHELSEA
MAZUNGUMZO ya mkataba mpya kati ya kiungo wa kati wa England, Mason Mount mwenye umri wa miaka 23 na wamiliki wa Chelsea yanaendelea na mafanikio yamepatikana "katika wiki chache zilizopita". (***Athletic)***

### HAZARD KUTUA NEWCASTLE
KUKIRI kwa Eden Hazard kwamba huenda akaondoka Real Madrid Januari kunaweza kuwa habari njema kwa Newcastle United, ambayo hapo awali ilihusishwa na kutaka kumnunua kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 31. (***Express***)

### RABIOT NA MAN UNITED
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 27 amesema anahisi "bahati" kutokamilisha uhamisho kutoka Juventus kwenda Manchester United msimu wa joto. (***Gazzetta Dello Sport, via Metro***)

### ENDRICK ATAKA UEFA
MCHEZAJI anayelengwa na Chelsea, Endrick mwenye umri wa miaka 16 amefichua kuwa anajiandaa kuhamia klabu iliyopo kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya na Mbrazil huyo amekuwa akijifunza Kiingereza. Mshambulizi huyo wa Palmeiras anatakiwa na klabu kadhaa za barani Ulaya. ***(Gazetta)***

### DIAZ ALITAKIWA BARCA
RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amesema klabu yake ilikuwa na nia ya kumsajili fowadi wa Colombia, Luis Diaz mwenye umri wa miaka 25 kabla ya kujiunga na Liverpool kutoka Porto. (***Mundo Deportivo, via 90min)***

### PATINO AFUATILIWA
KIUNGO wa kati wa Arsenal, Charlie Patino mwenye umri wa miaka 19, ambaye mkataba wake utakamilika msimu ujao wa joto na kwa sasa yuko kwa mkopo Blackpool, anafuatiliwa na Barcelona. (Calcio Mercato, via Express)

### MUDRYK EURO MIL 100
KLABU ya Shakhtar Donetsk inataka euro milioni 100 kwa winga wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21, ambaye amekuwa akihusishwa na kuhamia Arsenal, Manchester City na Newcastle United. (***Athletic***)

### DEMICHELIS KOCHA RIVER PLATE
MLINZI wa zamani wa Argentina, Martín Demichelis mwenye umri wa miaka 41, ambaye alikaa kwa miaka mitatu Manchester City, ameacha kazi ya ukocha katika klabu ya Bayern Munich na kuwa kocha mkuu mpya huko River Plate. (***Fabrizio Romano***)

### SILVA NA MAN
KLABU ya Manchester City inapanga mazungumzo na wakala wa kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva wakati wa Kombe la Dunia ili kuamua mpango wa maisha yake ya baadaye. Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England wanafahamu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 anataka kujiunga na Barcelona. (Mundo ***Deportivo)***

### DRAMEH AVUTIWA
MLINZI wa Leeds United, Cody Drameh mwenye umri wa miaka 20 anavutiwa na Newcastle United, pamoja na Lille, Borussia Dortmund na Bayer Leverkusen. (***Fabrizio Romano***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR AMTAKA MESSI NA ARGENTINA FAINALI

**DOHA,** Qatar

**●●● Ni katika Kombe la Dunia Qatar, azitaja timu tatu zenye uwezo wa kubeba huku...**

NEYMAR amefichua kwamba, yeye na mchezaji mwenzake wa Paris Saint-Germain, Lionel Messi walifanya utani kuhusu uwezekano wa kukutana kwenye fainali ya Kombe la Dunia kati ya Brazil na Argentina nchini Qatar.

**Neymar na Messi, pamoja na Kylian Mbappe, wanaunda safu ya utatu wa kutisha kwa PSG, ambayo imewafanya kuongoza kwa pointi tano kileleni mwa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, na kutinga hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.**

Lakini muungano huo utasitishwa kwa muda hadi mchezo unaofuata wa PSG mnamo Desemba 28 mwaka huu, huku nyota hao watatu wakipania kushinda Kombe la Dunia kwa nchi zao.

Ingawa alikuwa akiwapongeza sana Messi na Mbappe, Neymar alidokeza kwa mzaha kuwa anapenda timu yake ya Brazil kupata nafasi katika mechi inayoweza kukabili Messi na Argentina.

"Hatuijadili sana," alisema Neymar akiliambia gazeti la The Telegraph. "Lakini wakati mwingine tunatania juu ya kuvuka njia na kila mmoja kwenye fainali.

"Nilimwambia (Messi) kwamba nitakuwa bingwa na kushinda dhidi yake na tukacheka vizuri.

"Kucheza naye na Kylian ni furaha kubwa. Ni magwiji wawili, huku Messi akichukuliwa kuwa bora zaidi duniani.

"Kylian ni mchezaji mdogo ambaye amekuwa akikua na kuonesha uwezo wake na bado ana mengi ya kukua. Daima ni nzuri kucheza pamoja na wababe, nimekuwa nikipendelea hilo kwa sababu nafasi ya kushinda ni kubwa zaidi."

Neymar anahisi Brazil ni moja ya timu zinazopendwa zaidi, lakini pia aliangazia idadi ya timu zingine ambazo anaamini zinaweza kufuzu kwa fainali mnamo Desemba 18.

"Kombe la Dunia limejaa maajabu,"alieleza. "Unapata timu ambazo bila kutarajia hufika mbali sana hata kwenye mashindano hata kama wengi hawaziamini.

"Lakini ninaamini wanaopewa nafasi kubwa zaidi ni Argentina, Ujerumani, Hispania na Ufaransa. Nadhani hao wanne pamoja na Brazil wana uwezo kamili wa kutinga fainali."

Akiwa na umri wa miaka 30, Kombe la Dunia la Qatar linaweza kuwa la mwisho la Neymar.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,051,2

MECHI KALI
EGYPT
VERSUS
BELGIUM
1 | 9.54
X | 5.07
2 | 1.32

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
BREAKING
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GERRARD: BELLINGHAM ATAKUWA NYOTA WA ENGLAND



**LONDON,** England

JUDE Bellingham atakuwa nyota wa England kwa muongo ujao, kwa mujibu wa Steven Gerrard, huku Simba Watatu hao wakijiandaa kuanza kampeni yao ya Kombe la Dunia nchini Qatar.

Kinda huyo wa Borussia Dortmund atashiriki michuano mikubwa ya pili mfululizo chini ya kocha Gareth Southgate baada ya kusafiri kuelekea Qatar.

Baada ya mwanzo mzuri wa msimu katika Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, na Ligi ya Mabingwa Ulaya, matumaini ni makubwa kwamba Bellingham inaweza kuwa na sehemu kubwa ya kucheza katika harakati za hivi punde za England kusaka utukufu kwenye hatua ya dunia.

Nyota wa zamani wa Liverpool na England, Gerrard anahisi kuna mengi ya kuja kutoka kwa chipukizi huyo ndani ya miaka ijayo, wakati akitathmini nafasi ya timu huko Qatar.

“Mashindano yatajazwa na wachezaji wa kiwango cha juu,” alisema Gerrard.

“Jude, mimi ni shabiki wake mkubwa. Nadhani katika miaka 10 hadi 15 ijayo, atakuwa nyota wa England.

“Nadhani changamoto kubwa kwa England a ni kama tunaweza kupata wachezaji sahihi na kupata ushirikiano sahihi katika ulinzi.”

Southgate anaiongoza England katika michuano yake ya tatu mikubwa , baada ya kufika nusu fainali mwaka 2018 nchini Urusi na fainali kwenye Euro 2020.

Gerrard amesema Simba Watatu hao wanahitaji kujifunza kutokana na mapungufu yao ya kihistoria wakati huu ili kwenda mbali.

“Nadhani tofauti kati yao kufaulu au la itakuwa kama wanategemea uzoefu wa awali,” aliongeza. “Wanapaswa kuwa na imani kubwa kutokana na kuwa karibu na kutwaa Euro.

“Nadhani England ni moja ya timu nne au tano ambazo zinaweza kushinda Kombe hili la Dunia. Hiyo si imani potofu au matumaini. Kuna michezo ya kutosha kwetu kujenga imani na  lolote linaweza kutokea kutoka hapo.”



## Kante awindwa na Inter, Juventus

**LONDON,** England

KLABU za Juventus na Inter Milan zimeingia kwenye mbio moja kuwania saini ya kiungo wa Chelsea, N’Golo Kante, kwa mujibu wa La Repubblica.

Timu hizo mbili zimeripotiwa kuwania kumsajili mchezaji huyo wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Ripoti hiyo inadai kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 hana uhusiano mzuri na bosi mpya wa Blues, Graham Potter na anataka kuondoka hapo Stamford Bridge.

Pia inadaiwa kwamba uhamisho wowote wa Januari utagharimu takriban pauni milioni 18.

Mkataba wa Kante pale Chelsea unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu.

Kante, ambaye hatashiri[...] Kombe la Dunia kutokana n[...] kufanyiwa upasuaji wa m[...] suli ya paja, amecheza ma[...] mbili pekee msimu huu ak[...] wa na The Blues.

Kiungo huyo wa kati w[...] Ufaransa alijiunga na Che[...] sea mwaka wa 2016 akitoke[...] Leicester City baada ya ku[...] waa ubingwa wa Ligi Kuu y[...] England na anaonekana k[...] hama tena.

## HABARI MICHEZO

07,683/-

# MASHABIKI WAPEWA UHONDO KOMBE LA DUNIA

**Na Sabato Kasika**

MASHABIKI wa soka wanatarajia kushuhudia tamasha la BUd x FIFA Fan Festival wakati wakiangalia mechi za Kombe la Dunia mubashara katika eneo la heshima liitwalo Vista, Dubai Harbour.

Mratibu wa tamasha hilo, Ahmed Al Khaja, alisema eneo litakakofanyika tamasha, lina uwezo wa kuchukua mashabiki 10,000 kwa siku, na kwamba kila dakika na kila saa Kombe la Dunia mwaka huu litaonyeshwa mubashara kupitia runinga kubwa za mita mraba 330, zikiwa na uwezo wa sauti wa 4D.

"Dubai inategemewa kuhodhi moja kati ya matamasha sita ya mashabiki wa tamasha hili linalotegemewa kutazamwa mubashara katika eneo la heshima la Vista maeneo ya Dubai Harbour yenye uwezo wa kuchukua mashabiki 10,000 kwa siku,"alisema Al Khaja.

Alifafanua kuwa, kila dakika, kila saa ya mpira wa Kombe la Dunia mwaka huu, utaonyeshwa mubashara kupitia runinga kubwa zilizotengezwa zenye ukubwa wa mita mraba (square meters) 330, zenye uwezo wa sauti wa 4D.

"Kupitia tamasha hili, mashabiki wanategemewa kujihisi kama wapo uwanjani na wataweza kufurahia pamoja na wengine wote wanaotazama duniani kote na kutakuwa na burudani ya mbalimbali na vyakula,"alisema.

Aidha, alisema katika kurahisisha usafiri wakati wa Kombe la Dunia, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) wametoa ofa ya Visa inayokuruhusu kuingia na kutoka zaidi ya mara moja kwa wale wenye kadi maalumu ya Hayya kwa siku 90 ambayo itagharimu kiasi cha shilingi 63,000.

"Dubai inafurahi kuchaguliwa kuwa moja kati miji sita iliyochaguliwa duniani kusimamia FIFA Fan Festival na tunakaribisha mashabiki wote kuhudhuria, tamasha hili limedhaminiwa na kampuni ya Budweiser na mshirika rasmi ni kampuni kubwa ya viatu na mavazi ya Adidas pamoja na Dubai Harbour linalotegemewa kuanza Novemba 20," alisema..



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Nape Nnauye akiimba kwenye halfa ya uzinduzi wa mfumo mpya wa utoaji huduma kupitia CRDB Wakala, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mgunda kufua zaidi washambuliaji Simba

INATOKA UKURASA 32

Clatous Chama, anarejea tena uwanjani kuiwakilisha kwenye mechi ijayo dhidi ya Ruvu Shooting.

Mara ya mwisho kwa Chama kuonekana uwanjani ilikuwa kwenye mchezo dhidi ya Azam FC uliomalizika kwa Simba kupoteza kwa bao 1-0 .

Chama sasa amerejea kikosini baada ya kumaliza adhabu yake ya kufungiwa mechi tatu na Kamati ya usimamizi na uendeshaji wa Ligi Tanzania.

Nyota huyo alikosa mechi ya Singida Big Stars, Ihefu FC na Namungo na sasa ataonekana katika mchezo dhidi ya Ruvu Shooting utakapigwa Jumamosi hii uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kwa upande wake kocha Msaidizi wa Namungo FC, Shadrack Nsajigwa amekiri kuzidiwa na Simba na kutumia makosa waliyoyafanya na kuwapa nafasi ya kuibuka na ushindi katika mchezo huo.

Alisema wanarejea uwanjani kufanyia kazi madhaifu yaliyojitokeza katika mchezo huo kujiandaa na mechi ijayo ambayo watakutana na Azam FC.

## *Phiri kwenye rada kiatu cha dhahabu*

INATOKA UKURASA 32

nawania kiatu cha ufungaji bora kwa msimu huu kutokana na kasi yake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Phiri alisema kikubwa ambacho kinampa nafasi ya kufanya vizuri kwenye mechi anazocheza ni ushirikiano na wachezaji wote wa timu hiyo.

Alisema kila mmoja anapenda kuona wanapata matokeo na hilo lipo kwa wachezaji wote wa Simba wanapokuwa ndani na nje ya uwanja kuhakikisha kufahamu majukumu yao.

"Kinachofanya niweze kufunga ama kutoa pasi ya bao ni ushirikiano, upo kwa wachezaji wote kwani kila mmoja anafanya kazi ambayo tunapewa," alisema Phiri.

Aidha aliongeza kusema kwamba, "bado tunaendelea kupambana kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika kila mchezo na hatimaye kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu."


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/11/22 | 18:00 | Fleetwood Town vs Bolton Wanderers | 3.05 | 3.35 | 2.24 |
| 02. 19/11/22 | 18:00 | Burton Albion vs Plymouth Argyle | 2.65 | 3.40 | 2.50 |
| 03. 19/11/22 | 18:00 | Port Vale vs Charlton Athletic | 2.33 | 3.35 | 2.90 |
| 04. 19/11/22 | 18:00 | Cambridge United vs Accrington Stanley | 2.40 | 3.35 | 2.80 |
| 05. 19/11/22 | 18:00 | Colchester United vs Doncaster Rovers | 2.27 | 3.25 | 3.10 |
| 06. 19/11/22 | 18:00 | Grimsby Town vs Stevenage FC | 3.00 | 3.25 | 2.32 |
| 07. 19/11/22 | 18:00 | Cove Rangers FC vs Greenock Morton FC | 2.55 | 3.35 | 2.60 |
| 08. 19/11/22 | 18:00 | Inverness Caledonian Thistle FC vs Ayr United FC | 2.90 | 3.45 | 2.31 |
| 09. 19/11/22 | 18:00 | Queen of The South FC vs Montrose FC | 2.48 | 3.40 | 2.70 |
| 10. 19/11/22 | 18:00 | Albion Rovers FC vs Stranraer FC | 2.38 | 3.40 | 2.80 |
| 11. 19/11/22 | 18:00 | Annan Athletic FC vs Elgin City FC | 2.31 | 3.40 | 2.90 |
| 12. 19/11/22 | 18:15 | SD Ponferradina vs Real Oviedo | 2.55 | 3.05 | 2.85 |
| 13. 19/11/22 | 20:30 | Sporting Gijon vs CD Leganes | 2.28 | 3.05 | 3.30 |
| 14. 19/11/22 | 22:00 | MVV Maastricht vs Almere City FC | 2.60 | 3.60 | 2.45 |
| 15. 20/11/22 | 19:00 | Sakaryaspor vs Bandirmaspor | 2.80 | 3.30 | 2.45 |
| 16. 20/11/22 | 19:00 | Qatar vs Ecuador | 3.30 | 3.10 | 2.26 |
| 17. 20/11/22 | 21:00 | Racing Santander vs Burgos CF | 2.30 | 2.95 | 3.40 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 18/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1401 | Cameroon vs Panama | 1.91 | 3.48 | 4.03 |
| 13:45 | 1634 | Shams Azar Qazvin vs Chooka Talesh FC | 1.17 | 5.84 | 13.64 |
| 13:45 | 2051 | Shahrdari Astara vs Esteghlal Mollasani | 3.10 | 2.65 | 2.65 |
| 13:45 | 2317 | Saipa Karadj vs Arman Gohar Sirjan | 2.22 | 2.65 | 4.10 |
| 13:45 | 5369 | Fajr Sepasi vs Shahrdari Hamedan | 1.86 | 2.83 | 4.78 |
| 13:45 | 5949 | Mes Shahr-e Babak vs Khalijfars Mahshahr | 1.35 | 4.09 | 8.57 |
| 14:00 | 1246 | Esteghlal Khuzestan vs Chador Malu Yazd | 1.50 | 3.50 | 6.81 |
| 14:00 | 1922 | Neroca FC vs Sudeva Delhi FC | 1.77 | 3.51 | 3.99 |
| 14:00 | 3979 | Zorya Lugansk vs Oleksandria | 2.02 | 3.31 | 3.31 |
| 14:00 | 5509 | Pars Jonoubi Jam vs Darya Babol | 1.81 | 3.25 | 4.80 |
| 15:30 | 1292 | Kustosija vs Solin | 2.21 | 3.21 | 2.97 |
| 16:00 | 1890 | Marines FC Gisenyi vs Etincelles | 3.40 | 2.92 | 2.16 |
| 16:00 | 2575 | Ethiopia Bunna SC vs Bahir Dar Kenema FC | 2.87 | 2.82 | 2.53 |
| 16:00 | 3447 | Gorilla FC vs Bugesera FC | 2.44 | 2.83 | 2.97 |
| 16:15 | 2669 | Kalamata FC vs Panachaiki | 1.66 | 3.25 | 5.25 |
| 17:00 | 4206 | East Bengal vs Delhi Dynamos FC | 3.25 | 3.25 | 2.06 |
| 18:00 | 1144 | Egypt vs Belgium | 9.54 | 5.07 | 1.32 |
| 18:00 | 1237 | Slovacko vs Mlada Boleslav | 1.85 | 3.55 | 3.60 |
| 18:30 | 2632 | Bahrain vs Serbia | 8.30 | 4.96 | 1.36 |
| 19:00 | 4716 | Pogon II Szczecin vs Vineta Wolin | 1.34 | 4.87 | 6.63 |
| 19:00 | 5195 | MFK Karvina vs Slavia Prague | 15.51 | 8.14 | 1.10 |
| 20:00 | 3977 | Yeni Malatyaspor vs Pendikspor | 3.31 | 3.35 | 2.00 |
| 20:45 | 4695 | FC Eindhoven vs Telstar | 2.01 | 3.41 | 3.41 |
| 21:00 | 1345 | FC Arouca vs CD Feirense | 1.81 | 3.30 | 4.07 |
| 21:00 | 2102 | Astoria Walldorf vs Bahlinger SC | 2.43 | 3.41 | 2.53 |
| 21:00 | 3230 | Sonnenhof Grossaspach vs Nottingen | 1.67 | 4.50 | 4.00 |
| 21:00 | 3748 | Skive IK vs Esbjerg | 6.63 | 4.87 | 1.34 |
| 21:00 | 3825 | TSG Balingen-Rot vs Weiss Koblenz | 1.66 | 3.79 | 4.27 |
| 21:00 | 3839 | Reutlingen vs FSV 08 Bissingen | 2.85 | 3.90 | 2.17 |
| 21:00 | 4233 | ASV Cham vs DJK Gebenbach | 5.25 | 4.67 | 1.44 |
| 21:00 | 4315 | Kickers Offenbach vs Eintracht Trier | 1.35 | 4.67 | 6.81 |
| 21:30 | 1357 | Victoria Hamburg vs Niendorfer TSV | 2.34 | 4.09 | 2.34 |
| 21:30 | 3521 | RW Oberhausen vs FC Bocholt 1900 | 1.58 | 3.88 | 4.76 |
| 21:30 | 4959 | Neuchatel Xamax vs FC Wil | 2.27 | 3.69 | 2.57 |
| 21:30 | 5416 | Tura Harksheide vs Hamm United FC | 1.76 | 4.29 | 3.36 |
| 22:00 | 1842 | Spain U21 vs Japan U21 | 1.45 | 4.18 | 5.84 |
| 22:00 | 2024 | Lommel United vs Jong KRC Genk | 2.00 | 3.61 | 3.26 |
| 22:00 | 4324 | Excelsior Virton vs SI16 Football Campus | 1.98 | 3.65 | 3.26 |
| 22:15 | 1488 | Eimsbutteler TV vs TSV Buchholz | 1.23 | 7.00 | 8.80 |
| 22:15 | 4398 | Portugal U21 vs Czech Republic U21 | 1.55 | 3.98 | 4.86 |
| 22:15 | 5067 | AC Bellinzona vs FC Thun | 2.96 | 3.55 | 2.08 |
| 22:30 | 5260 | Lechia Gdansk vs Gornik Zabrze | 2.37 | 3.36 | 2.63 |
| 22:45 | 3791 | Larne vs Dungannon Swifts | 1.03 | 10.68 | 29.12 |
| 22:45 | 3841 | Gap Connahs Quay vs Caernarfon Town | 1.40 | 4.47 | 6.21 |
| 22:45 | 5277 | Ballymena Utd vs Linfield Belfast | 5.44 | 4.27 | 1.47 |
| 23:00 | 2516 | Aberystwyth Town vs Pontypridd Town | 2.32 | 3.46 | 2.63 |
| 23:00 | 2620 | Granada vs Albacete Balompie | 1.87 | 3.22 | 4.26 |
| 23:00 | 3032 | Helmond Sport vs De Graafschap | 3.35 | 3.55 | 1.98 |
| 23:00 | 5802 | Portsmouth vs Derby | 2.34 | 3.28 | 2.88 |
| 23:30 | 1061 | Belenenses vs Boavista | 3.60 | 3.40 | 1.89 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Novemba 18, 2022
Nipashe




Neymar amtaka Messi fainali

UKURASA 29

# Phiri kwenye rada kiatu cha dhahabu



●●● Mwenyewe asifia ushirikiano anaoupata ndani ya kikosi cha Simba, huku akisema kufunga ni jukumu...

**Na Saada Akida**

KASI ya ufungaji ya straika wa Simba, Moses Phiri imeanza kuwatisha wapinzani wake kwenye mbio za ufungaji Bora msimu huu kutokana na namna anavyotupia na kuisaidia timu yake kuondoka na pointi tatu muhimu, huku akisifia ushirikiano anaoupata ndani ya kikosi hicho.

Phiri sasa amefikisha mabao sita aliyoifungia Simba kwenye Ligi Kuu na yupo kwenye mbio za kuwania kiatu cha dhahabu (mfungaji bora), sawa na Idris Mbombo wa Azam FC na Reliants Lusajo wa Namungo FC.

Sixtus Sabilo wa Mbeya City ndio anaongoza kwenye mbio hizo akiwa ametupia nyavuni mara saba.

Phiri alifunga bao pekee kwenye mchezo huo lililoisaidia Simba kupata pointi tatu muhimu katika mchezo dhidi ya Namungo FC uliomalizika kwa ushindi wa 1-0, uliopigwa juzi katika uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Alitupia bao hilo dakika ya 33 baada ya shuti lililopigwa na Mohammed Hussein kupanguliwa na mlinda mlango wa Namungo, Deogratius Munishi kabla ya kumkuta Phiri na kufunga.

Mshambuliaji huyo ambaye ni kinara wa mabao ndani ya Simba sasa ametikisa nyavu mara sita ndani ya kikosi cha timu hiyo, huku akiwa nyota muhimu kwa wekundu hao wa Msimbazi.

Nyota huyo anaumiza kichwa jinsi washambuliaji wa timu pinzani wa

INAENDELEA UK. 31

## Mgunda kufua zaidi washambuliaji Simba

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Juma Mgunda amewapongeza wachezaji kwa kupambana na kuahidi kuboresha zaidi mapungufu ya kikosi cha timu hiyo ikiwemo uwezo wa mchezaji mmoja mmoja ikiwemo safu ya ushambuliaji.

Simba juzi waliendelea kupata pointi tatu dhidi ya Namungo FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa katika uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema mechi ilikuwa na ushindani mkubwa, Namungo FC walicheza vizuri lakini nyota wake walikuwa bora zaidi.

Alisema kikubwa wamepata matokeo mazuri ambayo yanaendelea kuwaweka katika mazingira mazuri kwenye msimamo wa ligi na mwisho kufikia malengo yao.

"Wachezaji wangu wamepambana kupata matokeo mazuri niwashukuru kwa hilo, lakini pia mashabiki nao kujitokeza uwanjani kwa sababu wao ni wachezaji wangu wa 13, tumepata bao 1-0, kikubwa ni kupata pointi tatu muhimu.

"Tumemaliza hii mechi tunarejea uwanjani kwa ajili ya kujipanga na mechi ijayo, kuhusu kufanya mabadiliko ya haraka inategemea na mchezo ulivyo," alisema Mgunda.

Alisema hawezi kufanya mabadiliko ya lazima kwa sababu ya mchezo upoje, mwenendo wa wachezaji kucheza na inategemea na jinsi ya kuanza mashambulizi.

"Lakini kwa staili tunacheza pasi za nyuma na hatufiki mbele hili nalifanyia kazi ikiwa ni madhaifu yetu kwa sababu tunatakiwa kuanza mashambulizi na kufika mbele ili kupata matokeo chanya," alisema.

Kocha huyo alimkingia kifua mshambuliaji wake, Denis Kibu na kudai kwamba bado ni mchezaji mzuri na kuna vitu anajitahidi kumuweka sawa.

Kibu amekuwa akidaiwa kushindwa kutumia vema nafasi zinazotengenezwa za kufunga mabao katika baadhi ya michezo Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwemo dhidi ya Namungo.

Mgunda alisema anatambua mapungufu ya wachezaji wake wote na kwa kuwa ni mwalimu ni jukumu lake kufanyia kazi mapungufu anayoyaona.

Alisema kwa kuwa anafahamu uwezo wa kila mchezaji na madhaifu yao anaimani atafanyia kazi na kuhakikisha wanakuwa imara.

"Ni kweli tumekuwa na mapungufu kuhusu Kibu ni mchezaji mzuri atasaidia timu, mapungufu yake nitayafanyia kazi na kuwafanya kuwa bora zaidi," alisema Mgunda.

Katika hatua nyingine kiungo wa Simba,

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >